# UPOLE NA UTOUPOLE KATIKA *PENDO LA KARAHA*

**NA**


**MUTETI AGNES MUENI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2020**

**UNGAMO**

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kingine, kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Sahihi ________________ Tarehe **_____06/11/2020_______**

**MUTETI AGNES MUENI**

**C50/89810/2016**

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa ili kutathminiwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi  Tarehe **______06/11/2020 ______**

**PROF. EVANS MBUTHIA**

(Msimamizi)

Sahihi _______________________ Tarehe **___06/11/2020_____________**

**DKT. MARY NDUNG'U**

(Msimamizi)

## TABARUKU

Kwa baba Cyrus Muteti na mama Josephine Muteti:

Mlinilea, mkajinyima na kunihimiza niendelee kukazana changamoto za maisha. Maombi yenu yalizaa matunda.

Kwa ndugu:

Elizabeth Kavilu, Mary Mwende, Joyce Nduku, Paul Muli na Peter Mulei

Asanteni kwa kuwa kuwa marafiki wa karibu nilipowahitaji.

## SHUKRANI

Namshukuru mwenyezi Mungu kwa fadhili na rehema zake. Alijalia nguvu hata nilipohisi kulemewa. Sifa na utukufu ni zake daima.

Shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu, Prof. Evans Mbuthia na Dkt. Mary Ndung'u kwa kujitolea kuniongoza na kunitia moyo kumaliza utafiti huu. Mlinifunza mengi kuhusu utafiti. Mlikuwa wavumilivu nami, mkanielekeza na kunipa mapendekezo mazuri kila wakati. Kwa kweli, nyinyi msingi bora wangu kuiga. Mungu awabariki sana.

Ningependa kuwashukuru wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi waliowahi kunifuza. Wahadhiri hawa ni pamoja na: Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Rayya Timamy, Prof. Mwenda Mbatia, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Leonard Sanja. Nimejifunza mengi sana kutoka kwa kila mmoja wenu. Mungu awazidishie hekima.

Shukrani ziwaendee marafiki walionishika mkono katika safari hii kama vile Fred Kitungo, Bw. Edward Agoi, Dkt. Margaret Njoroge, Martha Wafula, Mercy Yego, Ann Ndegwa, Ruth Nzambi, Dan Nyoike, Nancy Tanui, Joseph Nyagetiria, Lucy Gatune, Dickens Obwogi, Rehema Mercy, Violet Anindo na wengine wote tuliosoma pamoja. Kwenu nyote nasema shukrani.

## IKISIRI

Utafiti huu unashughulikia upole na utoupole katika *Pendo la Karaha.* Riwaya hii iliteuliwa kimakusudi ili kupata data iliyoweza kufanikisha malengo ya utafiti huu. Data ya kimsingi ya utafiti ilitokana na uchanganuzi wa kauli mbalimbali za wahusika. Kauli za wahusika zilichanganuliwa katika misingi ya nadharia mbili za kipragmatiki. Kila nadharia ilikuwa na wajibu wake tofauti katika kazi hii. Nadharia ya Upole iliyopendekezwa na Brown na Levinson (1987) ilikuwa na wajibu wa kuchunguza upole katika riwaya yote. Nadharia ya Utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996) nayo ilitekeleza wajibu wa kuchunguza kuwepo kwa utoupole katika *Pendo la Karaha.* Lengo la kwanza la utafiti huu lilihusu kuchunguza upole katika riwaya teule. Ilibainika kuwa mikakati ya upole iliyopendekezwa na Brown na Levinson ilidhihirika kikamilifu katika riwaya teule. Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kubaini utoupole katika *Pendo la Karaha.* Ilibainika kuwa mikakati ya utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996) ilidhihirika kikamilifu katika riwaya teule. Lengo la tatu lililohusu kubainisha matendo yanayoathiri nyuso za wahusika liliafikiwa vilevile. Ilibainika kuwa matendo yaliyoathiri zaidi nyuso hasi za wasikilizaji katika *Pendo la Karaha* yalijumuisha matendo ya msikilizaji kuarifu kuhusu vitendo hasi vijavyo, matendo ya msemaji yaliyoarifu msikilizaji kitendo kilichotarajiwa kuwepo na matendo yaliyoarifu matamanio ya msemaji kwa msikilizaji. Matendo yaliyoathiri nyuso chanya za wasikilizaji yalibainika kupitia matendo yaliyodhihirisha maoni hasi ya msemaji kuhusu uso chanya wa msikilizaji na msemaji kumpuuza msikilizaji.

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA UTAFITI

| | | |
|---|---|---|
| **Upole** | **:** | Matumizi ya lugha au vitendo vinayodhihirisha msemaji kumjali msikilizaji. |
| **Utoupole** | **:** | Matumizi ya lugha au vitendo vinavyodhihirisha kuwa mtendaji hamjali mtendewa. |
| **Mikakati ya upole** | **:** | Mbinu mbalimbali zinatumiwa na wazungumzaji ili kuhakikisha kuwa mazungumzo yameimarishwa. |
| **Mikakati ya utoupole** | **:** | Mbinu ambazo hutumiwa na wazungumzaji na husababisha kuvunjika kwa mazungumzo. |
| **Uso** | **:** | Matamanio ya msikilizaji na msemaji katika mazungumzo, yaani thamani ya kijamii ya mtu anavyotaka kuchukuliwa na wengine. |
| **Vitendo vinavyoutishia uso:** | | Vitendo ambavyo vinaweza kumkasirisha msemaji au msikilizaji na kusababisha kuvunjika kwa mazungumzo yao. |

## VIFUPISHO VYA MANENO YALIYOTUMIWA KATIKA UTAFITI

| | |
|---|---|
| KHJ | : Keshatajwa hapo juu. |
| MCU | : Mkakati chanya wa Upole |
| MHU | : Mkakati Hasi wa Upole |
| MNR | : Mkakati Ndani ya Rekodi |
| MNjR | : Mkakati Nje ya Rekodi |
| MUtNR | : Mkakati wa Utoupole wazi Ndani ya Rekodi |
| MCUt | : Mkakati Chanya wa Utoupole |
| MHUt | : Mkakati Hasi wa Utoupole |
| MUtD | : Mkakati wa Utoupole wenye Dhihaka |
| MKU | : Mkakati wa Kuzuia Upole. |

**YALIYOMO**

**UNGAMO** .......... **ii**
**TABARUKU** .......... **iii**
**SHUKRANI** .......... **iv**
**IKISIRI** .......... **v**
**MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA UTAFITI** .. **vi**
**VIFUPISHO VYA MANENO YALIYOTUMIWA KATIKA UTAFITI** .......... **vii**
**YALIYOMO** .......... **viii**
**SURA YA KWANZA** .......... **1**
1.0 Utangulizi .......... 1
1.1 Tatizo la Utafiti .......... 2
1.2 Maswali ya Utafiti .......... 3
1.3 Malengo ya Utafiti .......... 3
1.4 Sababu za Kuchagua Mada .......... 3
1.5 Upeo na Mipaka .......... 4
1.6 Misingi wa Kinadharia .......... 5
1.6.1 Nadharia ya Upole .......... 5
1.6.1.1 Mikakati Chanya wa Upole (MCU) .......... 6
1.6.1.2 Mikakati Hasi ya Upole (MHU) .......... 6
1.6.1.3 Mikakati Ndani ya Rekodi (MNR) .......... 7
1.6.1.4 Mikakati Nje ya Rekodi (MNjR) .......... 7
1.6.2 Nadharia ya Utoupole .......... 7
1.6.2.1 Mikakati ya Utoupole wazi Ndani ya Rekodi (MUtNR) .......... 8
1.6.2.2 Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt) .......... 8
1.6.2.3 Mikakati Hasi ya Utoupole (MHUt) .......... 9
1.6.2.4 Mkakati wa Utoupole wenye Dhihaka (MUtD) .......... 9
1.6.2.5 Mikakati ya Kuuzuia Upole (MKU) .......... 9
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .......... 10
1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu Upole na Utoupole. .......... 10
1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). .......... 18
1.8 Mbinu za Utafiti .......... 19

1.8.1 Uteuzi wa Sampuli ....................................................................................................19
1.8.2 Ukusanyaji Data .........................................................................................................20
1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data .....................................................................20
HITIMISHO ......................................................................................................................21
**SURA YA PILI**.....................................................................................................................**22**
**UPOLE KATIKA RIWAYA YA *PENDO LA KARAHA*** ........................................................**22**
2.0 Utangulizi ....................................................................................................................22
2.1 Kuwepo kwa Mikakati Chanya ya Upole (MCU)......................................................22
2.1.1 Njia ya kutambua mahitaji ya msikilizaji na kuyashughulikia ...................................23
2.1.2 Njia ya vitambulisho vya makundi. ............................................................................26
2.1.3 Njia ya kutafuta makubaliano na kuepuka mgogoro. .................................................28
2.1.4 Njia ya kuteua na kuchangia mada inayomvutia msikilizaji. ....................................31
2.1.5 Njia ya kujumuisha msemaji katika mambo. .............................................................32
2.1.6 Njia ya kuwa na matumaini .........................................................................................33
2.2 Kuwepo kwa Mkakati Hasi wa Upole (MHU) ...........................................................36
2.2.1 Njia ya kuomba msamaha ............................................................................................37
2.2.2 Njia ya kutaja mambo kwa jumla .................................................................................38
2.2.3 Njia ya kudhihirisha heshima baina ya wazungumzaji ...............................................39
2.2.4 Kuwa bila matazamio ...................................................................................................41
2.3 Kuwepo kwa Mikakati Ndani ya Rekodi (MNR) ........................................................43
2.3.1 Njia ya kushughulikia dharura. ....................................................................................43
2.3.2 Njia ya kukabiliana na tofauti za kimamlaka. ..............................................................44
2.3.3 Muktadha wa kumnufaisha msikilizaji. ........................................................................45
2.3.4 Muktadha wa kutoa ahadi kwa msikilizaji. ..................................................................48
2.4 Kuwepo kwa Mikakati Nje ya Rekodi (MNjR) ............................................................49
2.4.1 Njia ya kutumia maswali ya balagha ili kuzua utata .....................................................50
2.4.2 Njia ya kudokeza mambo ili kuzua utata. .....................................................................51
2.4.3 Matumizi ya kinaya ili kuzua utata. ..............................................................................52
HITIMISHO ......................................................................................................................54
**SURA YA TATU** .................................................................................................................**55**
**UTOUPOLE KATIKA RIWAYA YA *PENDO LA KARAHA*** ...............................................**55**

3.0 Utangulizi ....................................................................................................55
3.1 Mikakati Hasi wa Utoupole (MHUt)....................................................................55
3.1.1 Kumhusisha msikilizaji na maovu ....................................................................56
3.1.2 Msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji ..........................................................58
3.1.3 Kutisha. ...........................................................................................................61
3.2 Mikakati wa Utoupole Ndani ya Rekodi (MUtNR) ..........................................62
3.2.1 Njia ya kutoa onyo ...........................................................................................63
3.2.2 Njia ya kutoa taarifa .........................................................................................64
3.3 Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt)................................................................67
3.3.1 Kutoa kauli zenye matusi....................................................................................68
3.3.2 Kutafuta makabiliano. .......................................................................................71
3.3.3 Kumtenga msikilizaji..........................................................................................73
3.4 Mikakati ya Kuuzuia Upole (MKU) ....................................................................75
3.4.1 Kujizuia kujibu salamu ......................................................................................76
3.4.2 Kujizuia kusalimu...............................................................................................76
3.4.3 Kujizuia kusamahe ............................................................................................77
3.5 Mikakati ya Utoupole yenye Dhihaka (MUtD) ...................................................77
HITIMISHO .........................................................................................................82
**SURA YA NNE .................................................................................................83**
**MATENDO YANAYOATHIRI NYUSO ZA WAHUSIKA KATIKA MAZUNGUMZO KATIKA *PENDO LA KARAHA* ...........................................................................83**
4.0 Utangulizi ..........................................................................................................83
4.1 Uso Chanya..........................................................................................................83
4.2 Uso Hasi ..............................................................................................................84
4.3 Vitisho vya uso.....................................................................................................84
4.4 Matendo yanayodhamiriwa kutisha nyuso hasi za wahusika katika mawasiliano katika *Pendo la Karaha* ...........................................................................................84
4.4.1 Matendo yanayoarifu kuhusu kitendo hasi kijacho. ...........................................85
4.4.1.1 Amri...................................................................................................................85
4.4.1.2 Kukumbushwa mambo .......................................................................................85
4.4.1.3 Kutisha................................................................................................................86
4.4.2 Matendo yanayoarifu kitendo chanya kinachotarajiwa kuwepo .........................88

4.4.2.1 Kutoa ahadi ....88
4.4.3 Matendo yanayoarifu matamanio ya msemaji kwa msikilizaji....89
4.4.3.1 Chuki....89
4.4.3.2 Ghadhabu ....91
4.4.3.3 Ashiki....91
4.5 Matendo yanavyodhamiriwa kutisha nyuso chanya za wahusika katika mawasiliano katika *Pendo la Karaha* ....92
4.5.1 Maoni hasi ya msemaji kuhusu mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji. ....92
4.5.1.1 Kauli za kutoridhia ....93
4.5.1.2 Matusi ....93
4.5.1.3 Dharau....94
4.5.1.4 Makaripio....95
4.5.2 Msemaji kupuuza uso chanya wa msikilizaji....95
4.5.2.1 Nguvu ....96
4.5.2.2 Kuepuka mjadala....96
4.5.2.3 Msemaji kutamka habari hasi na hata kuringa. ....97
4.5.2.4 Kujitenga....98
HITIMISHO ....100
**SURA YA TANO ....101**
**MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO....101**
5.0 Utangulizi ....101
5.1 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti ....101
5.2 Mapendekezo kuhusu tasnifu zijazo ....103
5.3 Hitimisho ....104
**MAREJELEO ....105**
**VIAMBATISHO ....108**
Kiambatisho I: Udhihirikaji wa Upole....108
Kiambatisho II: Udhihirikaji wa Utoupole....114

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Utafiti huu unachunguza jinsi upole na utoupole unavyodhihirika katika riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Katika kuchunguza hali ya upole inavyojidhihirisha, tunafanya hivyo kwa kuziangazia athari zinazojitokeza. Aidha, tunalichunguza suala la utoupole na kubaini athari zitajitokeza. Athari zinazotokana na hali ya upole na hali ya utoupole zinaweza kuwa chanya zikiwa na lengo la kujenga uhusiano mwema baina ya msemaji na msikilizaji au athari hasi zikichangia kuleta mgogoro katika mazungumzo. Hali za upole na utoupole hujidhihirisha katika mazungumzo ya kila siku ya wanadamu huku zikichochewa na sababu mbalimbali. Tunachunguza matendo yanayoathiri nyuso za wahusika mbalimbali katika *Pendo la Karaha* na kusababisha upole au utoupole kutokea.

Utafiti huu unaongozwa na nadharia mbili; Nadharia ya Upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson (1987) pamoja na Nadharia ya Utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996). Katika kila nadharia, tulichunguza mikakati iliyojidhihirisha katika *Pendo la Karaha* kupitia kauli mbalimbali za wahusika.

Katika mahusiano ya kila siku, binadamu hukumbana na changamoto nyingi anapowasilisha ujumbe muhimu kwa msikilizaji. Ujumbe huu unapomfikia mtu wa pili unaweza ukasababisha kuelewana au kutofautiana kwa kiwango fulani. Kuelewana kunaweza kusababisha na athari chanya ilhali kutofautiana kunaweza kukasababisha na athari hasi. Athari za upole na utoupole tunazipata kwa kuchunguza kwa kina kauli za msemaji kwa msikilizaji na kuziegemeza katika miktadha wa mazungumzo yao. Tunashughulikia upole na utoupole kwa pamoja ili kupata picha jumlishi ya namna masuala haya yanavyoweza kujitokeza katika riwaya kwenye juhudi za kuunga, kujenga na kuendeleza mahusiano ya msemaji na msikilizaji.

Mawasiliano huhusisha zaidi ya mtu mmoja au kikundi cha watu, ambapo kuna msemaji na msikilizaji au mtendaji na mtendewa. Utafiti huu unachuguza kauli za msemaji kwa msikilizaji katika riwaya ya *Pendo la Karaha.* Unachunguza namna wazungumzaji wanavyoteua maneno yao kwa ufundi ili kuhakikisha kuwa anayeupokea ujumbe huo amefaidika au ameupitisha ujumbe wake kwa njia wazi. Maneno katika kauli za msemaji huwa na uzito wa aina yake kutegemea

mahitaji ya msikilizaji. Heshima iliyoko baina ya wazungumzaji inatuwezesha katika kutambua kauli zinazokisiwa kuwa za upole na zile zinazokisiwa kuwa za utoupole.

Migogoro mingi inazuka katika mawasiliano kati ya msemaji na msikilizaji. Japo utafiti huu unaangazia fasihi, masuala yanayojitokeza katika *Pendo la Karaha* yanaakisi hali halisi ya wanadamu katika ulimwengu wa sasa. Kutokana na matamshi ya chuki na uhasama migogoro hii inazidi kuongezeka na visa vya majonzi vinazidi kushuhudiwa. Utafiti huu unalenga kuwahamasisha wazungumzaji kuwa wapole kwa wengine kwani wanaotagusana nao huenda wanapitia magumu ya maisha. Utafiti huu unanuia kuchangia katika kupunguza visa hivi vya majonzi, kwa kuwapa wasemaji mikakati ya kuyapima maneno ili kupunguza athari za maneno hayo kwa msikilizaji na wakati huohuo kuwasilisha ujumbe unaonuiwa.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu unachunguza jinsi upole na utoupole unavyodhihirika katika riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Utafiti huu unachunguza mazungumzo ya wahusika ili kutambua kauli zinazodhihirisha upole na utoupole. Aidha, utafiti unabainisha matendo yanayoathiri nyuso za wahusika.

Utafiti huu umechochewa na ukweli suala la upole likiwa pekee limechunguzwa na watafiti wengi na suala la utoupole likiwa pekee vilevile. Hata hivyo, watafiti wengi waliochunguza kazi za kifasihi wameegemea upande wa upole. Kadhalika, kwa uelewa wangu, masuala ya upole na utoupole kwa pamoja katika kazi za kifasihi andishi haswa riwaya hayajachunguzwa kwa pamoja. Kuwepo kwa hali hii kunasababisha pengo tunapojiuliza, Je, upole na utoupole unaweza kudhihirika vipi katika kazi moja ya kifasihi andishi haswa riwaya? Utafiti huu unanuia kuliziba kupitia uchanganuzi uliotanuka. Utafiti huu umedhamiria kutoa utambuzi wa upole na utoupole unavyojitokeza katika riwaya kwa kutumia nadharia za kipragmatiki zinazokamilishana ili kupata picha jumlishi ya mawasiliano katika fasihi andishi. Utafiti huu unaziba pengo la nadharia mbili za kipragmatiki zinazokamilishana zinavyoweza kuhakiki riwaya. Utafiti hii unapata misingi kutokana na pengo la upole na utoupole kutozamiwa kwa pamoja katika riwaya.

Katika kuchunguza kauli za wahusika zinazodhihirisha upole, utafiti umeongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Aidha, katika kuchunguza kauli za wahusika

zinazodhihirisha utoupole, tumeelekezwa na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996). Kila nadharia ina wajibu wake tofauti. Tumeegemeza kila nadharia katika miktadha ya kimazungumzo ili kupata picha jumlishi ya suala la upole na utoupole katika riwaya.

### 1.2 Maswali ya Utafiti

1. Je, upole unadhihirika vipi katika riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014) ?
2. Je, utoupole unajitokeza vipi katika *Pendo la Karaha?*
3. Je, ni matendo gani yanayoathiri nyuso za wahusika katika mazungumzo katika *Pendo la Karaha?*

### 1.3 Malengo ya Utafiti

1. Kuchunguza namna upole unavyodhihirika katika *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014).
2. Kubaini namna utoupole unavyojitokeza katika *Pendo la Karaha*.
3. Kubainisha matendo yanayoathiri nyuso za wahusika mazungumzo katika *Pendo la Karaha.*

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu unahusu upole na utoupole katika riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Tulichagua mada hii kwa sababu inatupa nafasi ya kuchunguza mitazamo miwili ya kipragmatiki inayokamilishana katika kuchambua kazi ya kifasihi ambayo ni riwaya. Utafiti unahalalishwa kwa kutumia nadharia mbili kwa sababu kila nadharia ina wajibu wake tofauti katika *Pendo la Karaha.* Hii ni kwa sababu masuala ya upole na utoupole hujitokeza katika mazungumzo kwa sababu tofauti.

Tulichagua *Pendo la Karaha* na si riwaya nyingine kutokana na upekee wa namna inavyodhihirisha visa vinavyoweza kuzua upole na utoupole katika miktadha mbalimbali. Hali hii imeifanya kuwa kielelezo bora cha kuchanganulia upole na utoupole. Riwaya hii inatoa data toshelevu ya utafiti huu kupitia kwa visa dhahiri vya kuwepo kwa upole na utoupole miongoni mwa wahusika.

Japo kuwa tafiti nyingi zimefanywa kuhusu upole na utoupole na umuhimu wake katika mawasiliano kwenye miktadha mbalimbali, kwa uelewa wetu tunafahamu kuwa hakuna utafiti wa

awali unaochambua upole na utoupole kwa pamoja katika riwaya. Isitoshe, riwaya ya *Pendo la Karaha* haijawahi kuchunguzwa katika misingi ya upole na utoupole.

Utafiti huu ni muhimu katika taaluma ya Kiswahili kwani kutokana na matokeo ya utafiti, watafiti zaidi watapata hamu na kuchunguza upole na utoupole kwa pamoja katika tafiti zijazo za kifasihi. Kutakuwa na ongezeko la marejeo ya Kiswahili kuhusu upole na utoupole. Tasnifu hii itahifadhiwa kwenye maktaba ya chuo na kusomwa na watafiti wengine.

Pili, kuchunguza Nadharia ya Upole na Nadharia ya Utoupole za kipragmatiki kwa pamoja katika fasihi andishi unapanua elimu. Hali zinazowasilisha nadharia hizi zinafanya mawanda ya nadharia zenyewe kupanuka. Utafiti wenyewe unawafaa wasomaji kwa sababu wanaelezwa suluhisho la migogoro ya kimawasiliano kupitia njia mbalimbali za kuimarisha nyuso za wazungumzaji. Msomi anapata mwamko wa kisaikolojia anapohamasishwa kupitia mikakati ya kuboresha mahusiano wakati wa kuzungumza.

**1.5 Upeo na Mipaka**

Mambo ya kimsingi yanayoujenga utafiti wenyewe yamejikita kwenye utanzu wa fasihi andishi. Tumeushughulikia utanzu mmoja wa fasihi andishi ambao ni riwaya. Utafiti huu umejengeka kikamilifu tulipoangazia kipengele kimoja muhimu cha fani ambacho ni wahusika. Utafiti huu unajishughulisha na suala la upole na utoupole katika riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Masuala ya upole na utoupole yameshughulikiwa kwa undani pamoja katika riwaya moja ili kupata picha jumlishi ya namna upole na utoupole unavyoweza kudhihirika katika riwaya. Kauli za wahusika zinazodhihirisha upole na kauli zinazodhihirisha utoupole zimechunguzwa kwa kuegemezwa miktadha wa mazungumzo yao. Vilevile, utafiti huu umechunguza matendo yanayoathiri nyuso za wahusika katika mazungumzo katika *Pendo la Karaha*. Migogoro inayozuka baina ya wahusika imechunguzwa ili kufahamu sababu zinazowafanya wahusika katamka kauli maalum katika mazungumzo. Utafiti umechunguzwa kwenye misingi ya Nadharia ya Upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson (1987) na Nadharia ya Utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996). Tumechunguza mikakati ya nadharia hizi ili kubaini upole, utoupole na matendo yanayoathiri nyuso za wahusikia katika *Pendo la Karaha.*

### 1.6 Misingi wa Kinadharia

Utafiti huu unaongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson (1987) pamoja na Nadharia ya Utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996).

#### 1.6.1 Nadharia ya Upole

Brown na Levinson (1987) wanafafanua upole kama uepukaji wa mzozo wa kimazungumzo na kuyafanya mawasiliano yawezekane katika pande mbili zinazoweza kuzua ugomvi. Wanaeleza upole kuwa ni tukio linalojumlisha pande mbili zenye lengo sawa ambapo kila mzungumzaji hushiriki katika kuyaboresha mawasiliano. Watu hushiriki katika kuboresha mazungumzo na kuchukulia kuwa wenzao watafanya vivyo hivyo. Mihimili ya Nadharia ya Upole ni minne: kujali uso chanya, kujali uso hasi, njia ya kuwasilisha upole ndani ya rekodi na njia ya kuwasilisha upole nje ya rekodi.

Kulingana na Brown na Levinson (KHJ), upole hutokea kukiwa na tishio linaloweza kuathiri mazungumzo na wazungumzaji wanajaribu kudumisha thamani ya wenzao kwa faida ya pande mbili; upande wa msemaji na msikilizaji. Walieleza vitendo vinavyoweza kuathiri hisia za mtu anapozungumza. Vitendo hivi vinachangia katika kusababisha mazungumzo kukatizwa. Kulingana nao, upole una kwa lengo la kupunguza ukali wa vitendo hivi au kuliondoa kabisa tishio.

Nadharia ya Upole ilitanguliwa na Nadharia ya Uso iliyoasisiwa na Goffman (1967). Goffman aliibuni dhana ya uso. Alieleza uso kama thamani ya kibinafsi ya hadharani inayojumuisha mwanajamii kujitukuza kwa kujipa hadhi, majina au sifa nzuri zinazokubalika katika utamaduni wa jamii yake. Kila mwanajamii hutarajia wengine waitambue thamani yake wakati wa mahusiano. Uso hutegemea hisia. Hisia za mwanajamii zikiwa nzuri uso utaimarika na hisia zikikatizwa mwanajamii huhisi kuwa thamani yake imepungua. Kupungua huku husababisha fedheha na uso kuharibika. Vilevile, anachohisi mwanajamii kujihusu hutegemea wanachosema wengine kumhusu kupitia mtazamo wao na mahusiano yake na wengine. Uso unapopotea humaanisha kuwa hisia za muonekano bora wa kijamii huwa zinaumbuliwa na uso unapopatikana, hisia za muonekano mzuri katika jamii huimarishwa. Goffman anapendekeza binadamu wote katika mahusiano kushirikiana katika vitendo vya kuokoa nyuso za wengine pindi tu hisia za kupoteza uso zinapotokea.

Brown na Levinson (KHJ) waliipanua Nadharia ya Uso kwa kuigawa dhana ya uso kuwili; uso hasi na uso chanya. Wanaeleza kuwa iwapo kwa njia moja au nyingine msemaji mwenye busara ataathiri hisia za msikilizaji, ni lazima afanye hivyo kwa mkakati kutegemea uhusiano uliopo baina yake na mpokezi wa ujumbe huo. Brown na Levinson wanapendekeza mikakati ya upole itumike kukabiliana na matatizo ya mazungumzo ili nyuso za wazungumzaji ziimarike, kuhifadhika na hata kuboreka. Mikakati hii inajumuisha mihimili ya Nadharia ya Upole ifuatavyo; mikakati chanya ya upole (MCU), mikakati hasi ya upole (MHU), mikakati ndani ya rekodi (MNR) na mikakati nje ya rekodi (MNjR).

#### 1.6.1.1 Mikakati Chanya wa Upole (MCU)

Mikakati chanya wa upole humpa msikilizaji uso chanya. Mikakati hii inahusu kutambua mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji na kuyatimiza. Wazungumzaji hujaribu kufidia na kupunguza uwezekano wa kupotea kwa nyuso chanya za wengine. Uhusiano kati ya wasemaji huwa wa kutendeana mazuri. Mikakati hii inajumuisha kuepuka kutoa jibu moja kwa moja, kumjumulisha msikilizaji, kuepuka kutofautiana, kutumia ucheshi, kutegemea mazuri kila mara na kutoa ahadi.

#### 1.6.1.2 Mikakati Hasi ya Upole (MHU)

Mikakati hasi ya upole inatambua mahitaji ya uso hasi wa msikilizaji. Mikakati hii inahusu kumpa msikilizaji uhuru na nafasi yake. Msemaji husikika kuwa anajilazimisha kuzungumza na msikilizaji. Inabidi msemaji amtayarishe msikilizaji kwa kumtahadharisha kuwa anataka kuzungumza naye, kwa mfano, “Sitaki kukusumbua ila watumie washikadau wote ujumbe kabla ya mwisho wa siku.” Uso hasi wa msikilizaji hutambuliwa ila, japo kwa maneno fiche, msemaji anajaribu kumshinikiza msikilizaji amtekelezee mahitaji yake. Ulazimishaji huwa umefichwa na msikilizaji hujipata katika hali ambayo hawezi kukataa kumtimizia msemaji mahitaji yake. Wakati mwingine, msemaji huwa na nguvu kuliko msikilizaji na anaweza kutumia hadhira kuudhuru uso wa msikilizaji bila kuupoteza uso wake.

#### 1.6.1.3 Mikakati Ndani ya Rekodi (MNR)

Mikakati ya ndani ya rekodi huhusisha wahusika walio na mahusiano ya karibu au waliozoeana. Wazungumzaji wanaweza kutaniana ila sharti msemaji amakinike kuhifadhi uso wa msikilizaji. Wakati mwingine, mahitaji ya uso huwekwa kando ili kushughulikia tukio la dharura linalohitaji msaada. Vilevile, tishio la uso linaweza kuwa ndogo. Katika mikakati hii, kauli za moja kwa moja hutumika bila kuficha chochote. Msemaji anaweza kuwa na nguvu au mamlaka kumshinda msikilizaji. Mtendaji huwa kwenye rekodi ya kufanya tendo wazi kwa nia ya mawasiliano.

#### 1.6.1.4 Mikakati Nje ya Rekodi (MNjR)

Mikakati nje ya rekodi, hujumuisha kusema kwa maneno fiche kupitia tamathali mbalimbali za usemi na mbinu za kiisimu kama vile semi, maswali ya balagha, kinaya, balagha, sitiari, kutoeleza ukweli wote, takriri, aina mbalimbali za vidokezo, kusema kwa mzunguko ili maana kwa kiwango fulani iweze kujadiliwa. Mikakati hii haimfungi msemaji kwa maneno anayoyasema. Msemaji hawezi kuchukuliwa kuwa aliahidi kufanya jambo fulani kwa sababu hakuna ushahidi. Mahitaji ya msemaji yanatajwa tu na msikilizaji huhitajika kufasiri anachokisema msemaji. Msikilizaji kwa uelewa wake atahisi kuwa ana jukumu la kumtimizia msemaji jambo fulani. Msemaji huagiza kitu kwa kutoa vidokezo kwa njia fiche.

Mikakati hii inapoteuliwa na wazungumzaji katika miktadha ya mawasiliano ya kawaida, inaweza ikaathiri uso kwa njia hasi au chanya kama ilivyoelezwa na Brown na Levinson (1987) wakitumia dhana ya uso chanya na uso hasi. Mikakati hii ikitumiwa kwa njia inayofaa wakati wa mazungumzo, nyuso za wazungumzaji zitaimarika, kuhifadhika na hata kuboreka. Aidha, mikakati hii ikitumiwa kinyume na ilivyokusudiwa kutumiwa, nyuso za wazungumzaji zitaathirika kwa njia hasi.

### 1.6.2 Nadharia ya Utoupole

Nadharia ya utoupole iliasisiwa na Culpeper (1996). Mwelekeo wa kinadharia wa Culpeper unaendeleza mwelekeo wa Nadharia ya upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson (1987). Hii ni kwa sababu Culpeper (KHJ) alihisi kuwa Brown na Levinson (KHJ) hawakuzungumzia upande wa pili wa upole kwa kina. Anaeleza utoupole kama mkakati wa kimazungumzo ulioundwa ili kuuharibu uso na hivyo kusababisha mzozo kwa kuvuruga mwafaka. Kitendo kinachoweza

kutishia uso kikipewa nguvu husababisha changamoto za kimazungumzo na migogoro. Nadharia hii inajumuisha njia mwafaka zinazoweza kutumiwa na msemaji kuudhuru uso wa msikilizaji kimakusudi.

Mihimili ya Nadharia ya Utoupole ni mitano. Mihimili hii ni pamoja na; kusema kauli zenye utoupole wazi ndani ya rekodi, kupuuza mahitaji ya uso chanya, kupuuza mahitaji ya uso hasi, kudhihaki na kujizuia kabisa kutekeleza upole. Culpeper (1996) aliyaunga mkono mawazo ya Brown na Levinson (1987) kuwa ili kuafikia lengo la mawasiliano, mikakati ya upole huteuliwa kwa nia ya msemaji ya kutaka kuuhifadhi uso wa msikilizaji. Aliongeza kuwa pakiwa na upole lazima pawe na miktadha ambamo utoupole unajitokeza.

Culpeper (KHJ) anapendekeza mikakati mitano ya kutekeleza utoupole kutokana na mihimili ya Nadharia ya Utoupole. Mikakati hii ikitumiwa maneno ya msemaji huwa hasi yanayomrejelea msikilizaji kwa kumuumbua. Culpeper anakubali kuwa utoupole ni muhimu kuteuliwa ili kufikia lengo la mawasiliano. Mikakati ya utoupole ni pamoja na; mikakati ya utoupole wazi ndani ya rekodi (MUtNR), mikakati chanya ya utoupole (MCUt), mikakati hasi ya utoupole (MHUt), mikakati ya utoupole yenye dhihaka (MUtD) na mikakati ya kuuzuia upole (MKU).

#### 1.6.2.1 Mikakati ya Utoupole wazi Ndani ya Rekodi (MUtNR)

Msemaji katika mikakati ya utoupole wazi ndani ya rekodi, huwa na lengo la kuudhuru uso msikilizaji. Msemaji hutaja mambo wazi wazi kwa msikilizaji bila kuficha uzito wa maneno. Uso wa msikilizaji haupewi thamani yoyote. Maneno hayo yanaweza kuwa machache ila yanaubeba uzito kwa mpokezi wa ujumbe huo. Nia kuu ya msemaji ni kumkera mpokezi wa ujumbe.

#### 1.6.2.2 Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt)

Mikakati hii huwa na nia ya kuudhuru uso chanya wa msikilizaji kwa kuyapuuza mahitaji ya uso chanya. Mahitaji haya yanaweza kudhihirika ifuatavyo: msemaji asipomjali mtu anayetaka kujaliwa, kumpuuza au kujifanya humuoni mtu ambaye tayari ameshamtambua, kumtenga msikilizaji katika jambo fulani, kukataa kujiunga na msikilizaji, kutumia majina ya lakabu katika mahusiano yasiyo ya karibu, kutumia lugha ya siri isiyoeleweka vizuri na msikilizaji, kutumia msimbo unaojulikana na wengine kwenye kikundi ili kumtenga anayelengwa, kutaja mambo

mwiko kwa hiari kwa msikilizaji ili kuzua vurugu, kumtusi msikilizaji, kumkosesha utulivu miongoni mwa mengine.

#### 1.6.2.3 Mikakati Hasi ya Utoupole (MHUt)

Mikakati hasi ya utoupole huundwa kimakusudi kupuuza mahitaji ya uso hasi wa msikilizaji. Uso hasi hutaka nafasi yake iheshimiwe na kupewa uhuru. Msemaji hutaka kuonyesha uwezo wake na kumdhihaki msikilizaji huku akimshusha hadhi. Mikakati hii inaweza kujitokeza kama ifuatavyo: kumkaribia mwingine kiasi cha kuwa atajihisi kuwa faragha yake imeingiliwa, kutishwa au kuuliza mwenzako mambo ya siri.

#### 1.6.2.4 Mkakati wa Utoupole wenye Dhihaka (MUtD)

Kulingana na Culpeper (1996), mikakati ya utoupole yenye dhihaka unahusisha kutumia upole kwa unafiki. Msemaji hamwambii msikilizaji mambo ya kweli inavyostahili naye msikilizaji hautambui unafiki wa msemaji. Ujumbe anaowasilisha msemaji huwa kinyume na anavyouelewa msikilizaji. Msemaji hufanya vitendo vinavyoutisha uso kwa kuingiza msikilizaji kwenye lawama kwa lengo la kujifaidi. Mara nyingi msemaji hakusudii kumwonyesha msikilizaji upole ila kumkejeli. Msikilizaji anapouliza swali, msemaji hujibu kwa kejeli kupitia kwa kinaya. Aghalabu, msemaji hana hisia dhahiri kwa msikilizaji.

#### 1.6.2.5 Mikakati ya Kuuzuia Upole (MKU)

Mikakati ya kuuzuia upole inahusisha kutojishughulisha kudhihirisha upole kwa njia yoyote ile, kwa mfano; kukosa kushukuru, kukosa kutumia maneno ya adabu kama vile tafadhali, kupuuza salamu hata baada ya kusalimiwa kwa kukosa kuzijibu.

Culpeper (1996) anaeleza kuwa mikakati mbalimbali ya utoupole inaweza kuchanganywa kimakusudi ili kupata matokeo yanayofaa ya utoupole. Tofauti iliyoko kati ya Nadharia ya Upole na Nadharia ya Utoupole ni kuwa Brown na Levinson (1987) wanapendekeza njia za kuokoa nyuso za wazungumzaji ilhali Culpeper anapendekeza njia mwafaka za kuuwasilisha utoupole.

Kama ilivyo katika Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) mikakati ya utoupole vilevile inapotumiwa na wazungumzaji katika miktadha ya mazungumzo inaweza ikaathiri uso kwa njia hasi au kwa njia chanya. Athari chanya au hasi za uso zitategemea lengo la anayetumia mikakati

ya utoupole. Lengo likiwa kuonya, mikakati ya utoupole itakuwa imetumika kwa njia nzuri na uso chanya wa anayedhulumiwa utaimarishwa. Lengo la kutumia mikakati ya utoupole likiwa kumuumbua mpokezi wa ujumbe, uso hasi na uso chanya utaathirika.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Sehemu hii inashughulikia yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya utafiti. Sehemu hii imegawika katika vijisehemu viwili; yaliyoandikwa kuhusu upole na utoupole na yaliyoandikwa kuhusu riwaya ya *Pendo la Karaha.*

### 1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu Upole na Utoupole.

Sehemu hii inajumuisha wataalamu mbalimbali walivyofafanua mawazo tofautitofauti kuhusiana na suala la upole na suala la utoupole. Mjadala wa utafiti unapambwa na tofauti katika michango na makubaliano yao. Sehemu ya kwanza inahusu upole na tasnifu ambazo tayari zimeandikwa kutegemea Nadharia ya Upole. Aidha, sehemu ya pili inajumuisha utoupole pamoja na tasnifu ambazo zimeandikwa kutegemea Nadharia ya Utoupole. Kuhusu upole, mengi yameandikwa kama ifuatavyo:

Lakoff (1973) anaeleza kuwa kuna sheria za utendaji wa kipragmantiki zinazozingatiwa na wazungumzaji wanapowasiliana. Anapendekeza sheria mbili; ya uwazi na ya upole. Katika kaida ya uwazi, msemaji anapaswa kusema mambo kwa inayoeleweka moja kwa moja. Mambo yanayosemwa yanapaswa kuwa ya kweli, yanayoweza kuthibitishwa bila kupunguza au kuzidisha. Kaida ya upole inahusu mambo matatu; kwanza, msemaji hapaswi kumshurutisha msikilizaji kujiunga na mazungumzo. Pili, msikilizaji anapaswa kujihusisha na mazungumzo ya msemaji kwa hiari. Msemaji anauhuru wa kuwasilisha ujumbe na maoni yake bila kudhibitiwa na msikilizaji anapewa uhuru wa kuwasilisha maoni yake. Tatu, msemaji na msikilizaji wanapaswa kumthaminiana katika mazungumzo. Lakoff anafafanua kuwa hitaji la uwazi linaweza kukinzana na hitaji la upole kwa hvyo kanuni hizi hazitumiki kwa wakati mmoja. Kila kanuni inapewa nafasi wake kuhakikisha kuwa mawasiliano yameimarishwa na upole umehisika. Anaeleza kuwa katika mazungumzo yoyote, ni muhimu kuepuka kumuudhi msikilizaji kuliko kupata maelezo wazi.

Kadhalika, Grice (1975) anajihusisha na kueleza maana ya maana hasa kile kinachotokana na mazungumzo. Anaeleza kuwa ili mawasiliano yawe ya kufana, wazungumzaji huwa na kiasi fulani

cha makubaliano yanayotokea kutegemea juhudi zao. Grice alipendekeza kanuni nne za ushirikiano katika mawasiliano yoyote yale. Kanuni hizi ni pamoja na kanuni ya: idadi, jinsi au namna, ukweli na uhusiano. Kanuni ya idadi inahusu kusema mambo kwa kipimo kinachofaa. Kipimo hiki kinadhihirisha idadi ya maneno yanasemwa katika muktadha fulani. Inamhitaji msemaji kusema kwa idadi inayotosha bila kupunguza wala kuzidisha yanayohitajika.

Kanuni ya namna kulingana na Grice (KHJ) inahusu kusema mambo kwa njia inayoeleweka bila utata. Msemaji anapaswa kumwondolea msikilizaji uvulivuli wa kuelewa yale anayoyasema. Kanuni ya ukweli inahusu kusema mambo ya kweli ambayo unaushahidi nayo kiasi kwamba unapohitajika kuyathibitisha unaweza kuyaunga mkono kwa ushahidi thabiti. Katika kanuni ya uhusiano, mambo yanayosemwa yanapaswa kuhusu diskosi fulani. Kulingana na Grice, moja kati ya kanuni hizi nne inaweza kuvurugwa kukiwa na sababu maalum ya kufanikisha ushirikiano ambao sharti udumishwe. Kanuni hizi nne hutekelezwa na wasemaji kwa nia ya kuelewana na kanuni zote nne zikivunjwa maana hupotea na upole haudhihiriki.

Vilevile, Leech (1983) anaeleza upole kama tabia inayomwezesha msemaji na msikilizaji kuelewana na kudumisha mawasiliano katika muktadha maalum. Upole unahitaji kuzidisha wasilisho la dhana zenye upole na kupunguza dhana zinazojumuisha utoupole. Leech alihakiki mtazamo wa Grice (1975) aliyependekeza kanuni nne za mawasiliano. Leech anaeleza kuwa mtazamo wa Grice hautoshi kueleza mitagusano ya binadamu na namna ambavyo akili ya binadamu ni changamano. Anaeleza kuwa ili kuelewana, sharti kuwe na mwingiliano wa utaratibu wa kinaya, dhihaka, ushirikiano na upole. Kupitia kwa maelezo yake, tunapata ufahamu kuwa wakati wa kuzungumza, wasemaji wanaweza kutamka kauli hasi kwa wengine bila kuzidhihirisha wazi.

Leech (KHJ) anapendekeza kanuni sita muhimu za upole ambazo ni kanuni ya: mkakati, huruma, kusifu, kujitweza, kukubaliana na takrima au ukarimu. Kanuni ya mkakati inamhitaji msemaji kuzungumza kwa uangalifu katika heshima inayohitajika. Mambo hayasemwi tu. Kuna utatatibu wa kuyasema kwa udhibiti fulani. Msemaji anapaswa kupunguza gharama na kuzidisha manufaa ya msikilizaji. Kanuni ya huruma inamhitaji msemaji azidishe huruma kwa mpokezi wa ujumbe, kwa mfano, anapotoa rambirambi kwa msikilizaji. Wakati wote, msemaji huonyesha huruma kwa kutaka kujua mtatizo ya msikilizaji ili amsaidie na hivyo kuzua ushirikiano.

Kanuni kusifu anavyoieleza Leech (KHJ) inamhitaji msemaji kumsifu msikilizaji kwa kauli za kumfaidi. Anayoyasema msemaji yanapaswa kumfurahisha na kumvutia msikilizaji. Msemaji hapaswi kumkasirisha msikilizaji kwa vyovyote vile. Msemaji anapaswa kujizuia kujilimbikizia sifa na kutumia tasfida ili kuepuka kumkasirisha msikilizaji. Kanuni ya kujitweza inahusu kunyenyekea kwa msikilizaji anaposifiwa. Msikilizaji badala ya kupokea sifa hujitweza kwa kuwatajia wenzake mambo ambayo hana hakika ameyafanya vizuri. Kanuni kukubaliana inawahitaji wazungumzaji wakati wote kutafuta upenyu wa makubaliano na kuzidisha kauli zinazochangia kukubaliana. Kukubaliana kunaweza kuwa kabisa au kwa kiasi. Leech anapendekeza kuwe na makubaliano kwanza iwapo kutakuwa na kutofautiana na baadaye maelezo ya sababu ya kutofautiana.

Kulingana na Leech (1983), kanuni ya ushirikiano inahusu kuungana katika mazungumzo ili kufanikisha mawasiliano. Kanuni ya takrima au ukarimu inahusu msemaji kugharamika ili kumtoshelezea msikilizaji mahitaji yake. Msemaji anapojitolea kumfanyia msikilizaji jambo fulani hudhihirisha ukarimu na msikilizaji anafaidika kutokana na upole wa msemaji. Kulingana na Leech (KHJ), kanuni hizi zikifuatwa mazungumzo yataonekana kuwa yenye upole sana. Mazingira yanaathiri upole unavyoendeshwa na jukumu la upole ni kudumisha usawa na mahusiano mema yenye ushirikiano.

Pamoja na hayo, Fraser (1990) anaeleza kuwa kila jamii ina seti ya kaida zinazojumlisha sheria zinazoamuru tabia fulani, hali ambayo mambo yanapaswa kuwa na namna ya kufikiria katika muktadha. Upole hutokea iwapo tendo linalingana na kaida za jamii hiyo. Fraser anaeleza upole kama; mkataba wa mawasiliano, njia ya mazungumzo na utaratibu wa kijamii. Upole kama mkataba wa mawasiliano unahusu kanuni na haki za kuzungumza ili kufanikisha mawasiliano vyema. Majukumu ya wazungumzaji yakibadilika, mkataba wa kimazungumzo hubadilishwa. Upole kama njia ya mazungumzo unahusu asasi mbalimbali zilizopo katika jamii. Kanuni zilizowekwa za kijamii hudhibiti mazungumzo katika miktadha mbalimbali ya kijamii, kwa mfano, mazungumzo katika sehemu za kuabudu, kortini, hospitalini au hata shuleni. Kwenye asasi mbalimbali za kijamii, sheria hufuatwa na zikikiukwa basi hakutakuwa na upole. Mtazamo wa mazumguzo hutilia maanani masharti ya maafikiano kwa kutambua wazungumzaji kulingana majukumu yao.

Fraser (KHJ) anaeleza upole kama utaratibu wa kijamii unashirikishwa na utamaduni wa wanajamii mbalimbali. Kila jamii huelekezwa na utamaduni fulani katika miktadha mbalimbali. Utamaduni wa kijamii hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Tamaduni za jamii zikifuatwa, upole utadumishwa na tamaduni hizo zikikiukwa, upole utakiukwa. Fraser anauona upole kama njia ya kuuhifadhi uso kupitia kwa juhudi za wasemaji za kuhifadhi upole. Msemaji anapaswa kuchagua maneno yake vyema ili asimuudhi mpokezi wa ujumbe.

Suala la Upole vilevile limechunguzwa na watafiti mbalimbali ambao wamekita tasnifu zao kwenye tamthilia, filamu na riwaya kama ifuatavyo:

Raitania (2014) alifanya uchunguzi kuhusu Mikakati ya Upole katika kipindi cha runinga: *Mawaidha na Bi. Msafwari* katika runinga ya Citizen. Anaangazia upole unaotumiwa na Bi. Msafwari na watangazaji; Kanze Dena na Lulu Hassan wanapozungumzia suala la ndoa. Raitania anabainisha mikakati ya upole inayojitokeza katika kipindi hicho kupitia kwa Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Matokeo ya utafiti wake ni kuwa mikakati wa upole ndani ya rekodi haikutumika sana katika muktadha wa mazungumzo kwenye vipindi hivyo na mikakati chanya wa upole ilitumika sana. Utafiti wake unatufaa kwa misingi ya nadharia anayoitumia ambayo utafiti huu utatumia. Tofauti iliyopo kati ya utafiti huu na wake ni chanzo cha data ya utafiti. Chanzo cha data cha Raitania ni kipindi cha televisheni na chanzo cha data katika utafiti huu ni kauli za wahusika katika riwaya. Isitoshe, anatumia Nadharia ya Upole pekee ilhali utafiti huu unajihusisha na Nadharia ya Upole na Nadharia ya Utoupole kwa pamoja.

Vilevile, Kinyua (2015) alifanya uchunguzi kuhusu Ukiukaji wa Upole katika *Mhanga Nafsi Yangu* (Mohamed, 2012). Alichunguza matumizi ya lugha kwenye riwaya hiyo na maudhui yanavyojitokeza. Anabainisha wahusika wanaotoa kauli zinazokiuka upole na mambo yanayochochea ukiukaji wa kanuni za upole. Ameongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) na mtazamo wa Grice (1975). Matokeo ya utafiti wake ni; nadharia ya isimu inaweza kutumiwa kuchanganua kazi ya fasihi andishi, ukiushi wa upole huchochewa na muktadha wa mawasiliano na suala linalojadiliwa na wanaozungumza. Kazi ya Kinyua inatufaa sana kwani anachunguza upole katika riwaya, jambo ambalo sisi tunalifanya. Utafiti huu unajikita kuchunguza suala la upole, utoupole, matendo yanayoathiri nyuso za wahusika katika *Pendo la Karaha.* Tofauti

kati ya kazi ya Kinyua na utafiti huu ni kuwa utafiti huu unahusisha Nadharia ya Upole pamoja na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996).

Machira (2015) alifanya uchunguzi kuhusu Mikakati ya Upole kama ilivyotumiwa na wahusika katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* (Walibora, 2014). Alichunguza wahusika wakuu wanavyotumia mikakati ya upole katika maingiliano yao na wahusika wengine ili kufanikisha mazungumzo na athari za matumizi ya mikakati ya upole. Anaongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Matokeo ya utafiti wake ni kuwa wahusika wakuu wanashughulikia nyuso chanya na hasi za wasikilizaji na hivyo upole chanya kujitokeza kwa wingi. Kuna tofuati tatu kati ya utafiti huu na utafiti wake; anawaangazia wahusika wakuu wanavyoingiiana na wengine ila utafiti huu unawaangazia wahusika wote wanavyoingiliana. Chanzo cha data ya utafiti wa Machira ni tamthilia na utafiti huu unapata data kwenye riwaya. Tatu, amejikita katika Nadharia ya Upole pekee ilhali utafiti huu umejikita katika Nadharia ya Upole na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996). Utafiti wa Machira unatufaa tunapochunguza mikakati ya upole inayojitokeza katika kauli za wahusika kwenye riwaya.

Isitoshe, Inziani (2017) alichunguza Mikakati ya Upole kama ilivyojitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* (Arege, 2009). Alichunguza tamathali za usemi zilivyotumika kukiuka au kudhihirisha upole kwa kuchunguza jinsi upole ulivyojitokeza ili kukuza maudhui na mambo yanayochochea ukiukaji wa kanuni za upole. Anawachunguza wahusika wote, kama tunavyofanya katika utafiti huu. Aliongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Matokeo ya utafiti wake yalikuwa ifuatavyo; tamathali nyingi za usemi zilidhihirisha matumizi ya mkakati wa upole nje ya rekodi na hivyo akachanganua kwa undani ili kufahamu kile ambacho mwandishi alidhamiria kukisema. Anapendekeza mikakati ya upole ichunguzwe miongoni mwa wahusika mbalimbali wanavyojengwa kwa kukiuka na kudhihirisha upole. Utafiti wake unatufaa kwa namna alivyoainisha vijimada vya utafiti mzima ili kupata matokeo ya kina. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wa Inziani kwani utafiti wake unatuongozwa na Nadharia Upole ilhali utafiti huu unajumuisha Nadharia ya Upole na Nadharia ya Utoupole ili kupata picha jumlishi ya upole na utoupole.

Pamoja na hayo, Ngisirei (2018) alichunguza kuhusu Upole katika mazungumzo ya vipindi vya *Sobetab Kapchi* katika idhaa ya *Kass FM.* Anachunguza umuhimu wa upole katika mazungumzo

na kuchanganua mikakati ya upole inayotumika kuwasilisha vipindi hivyo, athari na hali za uzingatiaji na ukiukaji wa kanuni za upole. Anaongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Matokeo ya utafiti wake ni; wazungumzaji wametunza nyuso za wengine kwa kusema mambo kwa njia fiche. Athari chanya na hasi zinajitokeza katika utekelezaji na ukiukaji wa kanuni za upole. Utafiti wake unatufaa kwani mikakati upole anayoitumia ni ile tunayochunguza. Tofauti ya tafiti hizi mbili ni kuwa Ngisirei anashughulikia mikakati ya upole kwenye kipindi cha redio pekee ilhali utafiti huu unajikita kwenye mikakati ya upole na utoupole kwenye riwaya kulingana na Nadharia ya Upole na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996).

Kadhalika, utoupole umechunguzwa na kuandikiwa wataalam mbalimbali katika kuieleza na kuiendeleza dhana hiyo kama ifuatavyo:

Eelen (2001) anajikita katika kufafanua hali zinazochangia kuzua utoupole wakati watu wanapozungumza kama vile; kusalimiwa na kukosa kujibu salamu japo kuwa umemsikia mwenzako akikuamkua, kutendewa mema na kulipuuza jukumu lako la kushukuru. Anaeleza matatizo yayojitokeza kutokana na Nadharia ya Upole kwa kutumia vielelezo vya upole vya kimapokeo. Matatizo haya ni pamoja na; kutoweza kueleza utoupole kwa vigezo vile vile vinavyoeleza upole kwenye baadhi ya vigezo vya utoupole, kuchukulia utoupole kama kukosekana kwa upole na kuchukulia utoupole kama kinyume cha upole ili kuupanua msamiati wa upole na sio wa utoupole.

Vivyo hivyo, Culpeper na wengine (2003) wanaeleza kuwa utoupole haujitokezi tu. Utoupole hujumuisha mikakati ya kimazungumzo iliyoundwa kimakusudi ili kuuharibu uso wa msikilizaji. Utoupole hutokea wakati msemaji anapotamka kwa hiari tendo linalotishia uso wa msikilizaji na kusababisha migogoro ya kijamii.

Culpeper (2005) anaeleza utoupole kama mkakati wa kimazungumzo ulioundwa kushambulia uso na kusababisha kutotangamana na mgogoro wa kijamii. Anasema kuwa utoupole hutokea wakati ambapo msemaji anawasilisha tishio la uso kimakusudi au msikilizaji anapounda tabia fulani kwa hiari ili kuutisha uso wa msemaji. Ujumbe unaolengwa kuwasilishwa na msemaji huwa muhimu. Anaeleza kuwa nyenzo za uzungumzaji kiutoupole huenda zaidi ya sarufi na msamiati. Usuli wa matumizi ya lugha kwa ujumla hutekeleza jukumu la kuunda na kutathmini utoupole. Viziada lugha kama vile kiimbo huchangia kuweka wazi kauli za wahusika zinazodhihirisha utoupole.

Anaongeza kuwa mikakati ya kutowasilisha chochote ya utoupole hutokea wakati; msikilizaji anaposalimiwa na kuwa kimya au binadamu anapopokezwa zawadi na kukosa kushukuru.

Kadhalika, Bernal (2008) anaeleza sifa za arudhi ni kama vile toni, mwendo wa sauti au hata kicheko huchangia katika kuamua iwapo tamko lina utoupole kwa hakika au utoupole wenye dhihaka. Katika fasihi andishi, utoupole kupitia sifa za arudhi huweza kutambuliwa kupitia kwa maelezo ya mwandishi.

Vilevile, Bousfield na Locher (2008) wanaeleza utoupole kama tabia inayolenga kuudhuru uso wa mtu kwa kumkasirisha kimakusudi wakati wa mawasiliano. Wanadokeza njia tatu zinazosaidia kukabiliana na tatizo la utoupole kama vile; kunyamaza kimakusudi baada ya kuambiwa jambo linaloudhi, kukubali vitendo vinavyohasiri uso na kupambana na tatizo lenyewe. Wanaeleza kuwa kuna hali zinazochangia kuwepo kwa utoupole kama vile; cheo na nguvu. Wanaamini kuwa utoupole umefungamanishwa na dhana ya madaraka kama vile msemaji kuwaogofya waliochini yake ili afaidike na kuheshimika. Cheo cha msemaji kikiwa cha juu kuliko cha msikilizaji, msemaji wakati mwingi hudhihirisha utoupole wa hali ya juu. Walio na nguvu au mamlaka aghalabu hudhihirisha utoupole kwa kiwango cha juu wanapozungumza na walio chini yao kimadaraka.

Bousfield na Locher (KHJ) wanakubaliana na Culpeper (1996) kuwa kuelewa anachonuia msemaji ni msingi wa kutambua utoupole na hivyo wanaiendeleza Nadharia ya Utoupole. Bousfield na Locher (2008) pamoja na Culpeper wanatofautisha utoupole na kukosa adabu. Wanaeleza kuwa utoupole hutekelezwa kimakusudi ila kukosa adabu sio makusudi na kukosa adabu na utoupole huzua tabia hasi. Mawazo ya Bousfield na Locher yanaufaa utafiti huu tunapotambua kauli za wahusika zinazodhihirisha utoupole ili kupata data sahihi ya utafiti huu.

Culpeper (2011) anaeleza kuwa kuepuka uwazi katika mazungumzo kunaweza kuzua upole ila sio wakati wote. Anasisitiza kuwa baadhi ya vielelezo vya upole vinapatia nafasi utoupole na namna kauli inavyotamkwa huchangia kudhihirisha iwapo ina utoupole au la. Anafafanua suala la utoupole na arudhi kuwa namna tamko linavyosemwa huzua utoupole. Jambo fulani lenye uzito wa kudhihirisha utoupole linaweza kusemwa kwa njia nzuri na likaeleweka bila kuzua athari hasi. Kauli hiyo hiyo inaweza kusemwa kwa namna tofauti na kusababisha utoupole. Arudhi inaweza kujumuisha sauti kubwa, kidatu, kiimbo au hata mwendo wa kuzungumza kupitia kasi mawimbi.

Sifa hizo kutegemea namna zinavyotumika huchangia kwa kiwango kikubwa kuzua hali ya utoupole.

Culpeper (KHJ) anaeleza kuwa kuna seti za kidesturi zinajumuisha mtindo maalum wa kusema mambo. Mitindo ya kuwasilisha utoupole inajumuisha msemaji kumwelekezea msikilizaji matusi kama vile: tamko hasi, madai hasi, maneno hasi, virejeshi hasi katika nafsi ya tatu kwa sababu hawezi akahukumiwa kwa kutaja mtu mahususi. Mitindo mingine ya utoupole ni kuuliza maswali ambayo hayapendezi msikilizaji, kulalamika, kutonesha kidonda, kusisitiza ujumbe, kupuuza, vitisho, vinyamazishi na laana. Anasisitiza kuwa mtindo wa utoupole unaotumiwa hutegemea muktadha katika ukadiriaji wa utoupole. Muktadha unaweza kugeuza tamko lenye utoupole lieleweke kama linalojumuisha upole. Utoupole unapatikana kwa kutumia maneno yanayomtenga msikilizaji mmoja na mwingine kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

Isitoshe, Aydınoğlu (2013) anaeleza kuwa utoupole haujitokezi tu, bali huwa na vyanzo vyake vinavyoutawala. Vyanzo vya utoupole ni pamoja na; hasira, onyesho la nguvu na mamlaka, hitaji la kukera msikilizaji, hitaji la kuburudisha, mzozo, huzuni kubwa, kutaka kuutetea uso wako na onyesho la kukabiliana.

Suala la Utoupole limechunguzwa na watafiti mbalimbali ambao wamekita tasnifu zao kwenye jamii na filamu kama ifuatavyo:

Goro (2014) alichunguza kuhusu lugha ya utoupole inayotumiwa na makondakta katikati mwa jiji la Nairobi hadi mtaa wa Dandora. Alitambua tamko zenye utoupole zinazotumiwa na makondakta, kubaini mikakati ya utoupole wanayoitumia na kuchunguza vipengele vinavyowapa motisha kusema maneno yenye utoupole. Aliongozwa na Nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Matokeo ya utafiti wake yalikuwa: mikakati chanya ya utoupole na mikakati hasi ya utoupole ilitumika kwa wingi, mkakati ya kejeli ulitumika kwa frikwensi ndogo zaidi. Alitambua kuwa utoupole hutegemea muktadha maalum wa mazungumzo. Utafiti wa Goro unatuongoza kutambua kauli za utoupole kama alivyofanya kupitia kwa mikakati ya utoupole. Tofauti iliyopo kati ya utafiti wa Goro na utafiti huu ni kuwa data ya utafiti huu inatokana na tungo za wahusika katika riwaya ilhali chanzo cha data ya Goro ni mazungumzo ya makondakta wa matatu katika sekta ya usafiri. Goro anaangazia Nadharia ya Utoupole pekee ilhali utafiti huu unajumlisha Nadharia ya Utoupole na Nadharia ya Upole.

Kadhalika, Joan (2015) alichunguza kuhusu Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa mikakati ya utoupole katika mfuatano wa kipindi cha Uingereza cha *Sherlock.* Anachunguza kauli za wahusika mbalimbali katika kipindi hicho. Anaongozwa na Nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Matokeo ya utafiti wake ni kuwa hali ya utoupole inajitokeza kwa wingi katika kipindi hicho. Kazi ya Joan inaukaribu na utafiti huu kwa sababu anaichunguza mikatati ya utoupole kulingana na Culpeper (1996) kama tunavyofanya. Tofauti ya kazi ya Joan na utafiti huu ni kuwa utafiti huu unajumuisha Nadharia ya Utoupole na Nadharia ya Upole ya Brown ili kufanikisha utafiti. Joan anachunguza kipindi cha televisheni kubaini hali ya utoupole pekee ilhali utafiti huu unachunguza riwaya kubaini hali ya upole na utoupole kwa pamoja.

Pamoja na hayo, Nyangi (2017) alichunguza Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa Utoupole katika Filamu za Kiswahili. Alichunguza kauli za waigizaji wa filamu husika na namna wanavyokabiliana na hali ya utoupole katika mazungumzo. Anaongozwa na Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996). Matokeo ya utafiti wake ni kuwa: mikakati ndani ya rekodi ya utoupole imejitokeza kwa asilimia kubwa, 45% na mikakati wa kutowasilisha chochote imejitokeza kwa asilimia ndogo, 4%. Tofauti za kimamlaka zimechangia katika matumizi ya mikakati ya utoupole kwa asilimia sitini, 60%. Utafiti wa Nyangi unaufaa utafiti huu kwa misingi ya nadharia utafiti tunayoitumia na namna alivyoichanganua data yake. Tofauti kati ya utafiti huu na wa Lilian kuwa Lilian anachunguza Filamu za Kiswahili ilhali chanzo utafiti huu unachunguza riwaya. Nadharia anayotumia Lilian ni ya Utoupole pekee ilhali utafiti huu unatumia Nadharia ya Upole pamoja na Nadharia ya Utoupole kuchunguza upole na utoupole.

Japo kuwa maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusiana na hali ya utoupole yanatofautiana, wanakubaliana kuwa kuna athari, sababu na vichocheo ambavyo huifanya hali ya utoupole iteuliwe.

### 1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014).

Riwaya ya *Pendo la karaha* iliyochapishwa na Habwe (2014) imefanyiwa utafiti kama ifuatavyo:

Kihara (2016) alichunguza kuhusu Nafasi ya Vijana katika riwaya za *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014) na *Kovu la Moyoni* (Habwe, 2014). Anafanya hivyo kwa kuchunguza nafasi ambazo vijana wamepewa katika riwaya teule, changamoto zinazowakabili vijana katika jamii na kiasi ambacho

uwasilishaji wa maudhui ya nafasi ya vijana umefaulu. Kihara anaongozwa na nadharia ya Uhalisia Hakiki. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa vijana wanachukua nafasi hasi wasizozipenda kutokana na hali ngumu ya maisha na kuishia kupuuza maagizo ya wazazi. Chanzo cha data ya utafiti huu ni Riwaya ya *Pendo la Karaha* aliyochunguza Kihara. Kazi yake inatusaidia tunapoangazia namna wahusika wanavyodhihirisha hali ya upole na utoupole katika riwaya ya *Pendo la Karaha.* Tofauti kati ya utafiti huu na wa Kihara ni kuwa; Kihara ameegemea wahusika vijana ilhali utafiti huu haujafungika kiumri. Tunachunguza wahusika wa aina mbalimbali.

Kadhalika, Gromov (2018) alichunguza kazi za mwanzo tatu za kifasihi za Habwe kuhusiana na uhakiki wa kijamii kupitia kwa mwamko mpya wa uandishi wa fasihi ya Kiswahili. Katika uchunguzi wake, aliigusia riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014), kwa kuijumlisha na kazi nyingine za Habwe. Kazi hizi ni; novela *Maumbile si Huja* (1995), riwaya *Maisha Kitendawili* (2003) na *Paradiso* (2005). Katika kunogeza maelezo yake, aliangazia baadhi ya kazi zake Habwe za baadaye kwa kusema kuwa kazi zilizoandikwa na Habwe zinahakiki jamii kupitia kwa mwamko mpya. Gromov anaeleza kuwa katika riwaya ya *Pendo la Karaha* kuna utumwa wa kisasa uliofunikwa vazi la ajira ughaibuni na madawa ya kulevya miongoni mwa vijana. Anautaja umaskini kama cha matatizo hayo. Kutokana na maelezo yake, suluhu linapatikana mwishowe kupitia kwa mhusika mkuu Kudra kurudi nyumbani. Utafiti wa Gromov unatufaa kwani ametoa muhtasari wa ploti kwa kutaja mambo muhimu yaliyoandikwa katika riwaya nzima. Mambo anayoyataja ni yaleyale tunayoyashughulikia ila kwa kina kwenye misingi ya upole na utoupole.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu ya mbinu za utafiti inahusu njia ambazo utafiti huu unatumia ili kufanikisha utafiti. Mbinu za utafiti huu zimegawika katika sehemu tatu ambazo ni; uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

#### 1.8.1 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ya utafiti huu ni sampuli lengwa. Kulingana na Mugenda na Mugenda (1999), sampuli lengwa huchaguliwa kimakusudi kutumika katika utafiti ili kupata data ya kina kulingana na malengo ya utafiti. Riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014) imechaguliwa kimakusudi ili kupata data inayohitajika. *Pendo la Karaha* imeteuliwa miongoni mwa kazi nyingine zilizoandikwa na Habwe kwa sababu zifuatazo: kuwepo kwa tofauti za wahusika kama uhusiano,

umri na mamlaka zinazochangia kudhihirisha hali ya upole na utoupole. Miktadha mbalimbali inayodhihirisha upole na hali ya upole imejitokeza wazi na kauli dhahiri za wahusika zinadhihirisha hali ya upole na hali ya utoupole.

Nadharia ya Upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson (1987) na Nadharia ya Utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996) zimeteuliwa kimakusudi kutegemea majukumu mbalimbali ya kila nadharia. Nadharia ya Upole inatuwezesha kutambua kauli za upole ilhali Nadharia ya Utoupole inatuwezesha kutambua kauli zilizo na utoupole kutegemea mikakati ya upole na mikakati ya utoupole.

### 1.8.2 Ukusanyaji Data

Utafiti huu ulijikita katika utafiti maktabani. Mtafiti alikagua majarida ya waandishi mbalimbali, tasnifu na vitabu vilivyoandikwa kuhusu suala la upole na utoupole. Riwaya ya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014) ilisomwa na mtafiti ili kupata kauli zinazokisiwa kuwa za upole na utoupole. Tulichunguza namna wahusika mbalimbali walivyodhihirisha hali ya upole na utoupole kupitia kwa kauli zao na kunakili ili kuweka rekodi ya data ya utafiti huu. Kauli za wahusika ziliegemezwa kwa muktadha wa mawasiliano yao. Vipashio hivi vilichujwa na mtafiti na kusalia na kauli muhimu zinazodhihirisha wazi hali ya upole au utoupole. Katika kuchuja kauli za wahusika, tulizingatia mikakati mbalimbali katika Nadharia ya Upole na vilevile mikakati katika Nadharia ya Utoupole. Matendo yaliyokisiwa kuathiri nyuso za wahusika katika *Pendo la Karaha* yalichunguzwa na kunakiliwa vilevile.

### 1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Mtafiti aliainisha kauli alizokuwa amenakili zilizofikiriwa kuwa na upole na utoupole katika sehemu mbili: upole na utoupole. Kauli za wahusika zilizowakilisha upole zilitenganishwa kwanza kutegemea kategoria nne: mikakati chanya ya upole, mikakati hasi ya upole, mikakati ndani ya rekodi na mikakati nje ya rekodi kama ilivyo katika mikakati ya Nadharia ya Upole. Aidha, kauli zinazowakilisha utoupole ziliwekwa kwenywe kategoria tano: mikakati chanya ya utoupole, mikakati hasi ya utoupole, mikakati ndani ya rekodi ya utoupole, mikakati ya utoupole yenye dhihaka na mikakati ya kuzuia upole kama ilivyo katika Nadharia ya Utoupole. Matendo yanayoathiri nyuso za wahusika yaliwekwa katika muktadha halisi wa *Pendo la Karaha*.

Kutokana na migao hii, malengo ya utafiti yalichunguzwa katika kuleta pamoja kauli za wahusika na mikakati mbalimbali ya upole na utoupole. Data iliyokusanywa tuliiwasilisha katika kutegemea malengo matatu ya utafiti wenyewe. Matokeo ya kila lengo la utafiti yalichunguzwa kwa maelezo ya kina ili kuthibitisha iwapo lengo mahususi limeafikiwa au la. Mtafiti alitoa maelezo ya namna upole na utoupole ulivyodhihirika na vilevile matendo yanayoathiri nyuso za wahusika katika *Pendo la Karaha.*

**HITIMISHO**

Sura hii imeangazia usuli wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, misingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwakilishaji wa data, hitimisho na marejeleo. Sura hii ni kitangulizi cha sura zinazofuata.

Sura ya pili inachunguza upole kama unavyodhihirika katika *Pendo la Karaha*. Kutokana na kauli za wahusika mbalimbali, mtafiti anabaini kauli zinazoakisi mikakati ya upole. Aidha, sura ya tatu inahusu kubaini utoupole kama unavyodhihirika. Kauli za wahusika zinazodhihirisha mikakati ya utoupole zinabainishwa kulingana na muktadha wa mawasiliano. Mifano mbalimbali kutoka kwenye *Pendo la Karaha* inatolewa kama ushahidi wa kuwepo kwa mikakati hii.

Kadhalika, sura ya nne inabainisha matendo yanayoathiri nyuso za wahusika mbalimbali kama vichocheo vinavyowafanya kudhihirisha mikakati ya upole na mikakati ya utoupole. Vilevile, athari zinazozuka kutokana na upole na utoupole zinashughulikiwa katika sura hii. Pamoja na hayo, sura ya tano inatathmini malengo ya utafiti na ufafanuzi kutolewa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya utafiti yanaelezwana mapendekezo ya tafiti zijazo yanawasilishwa.

# SURA YA PILI

# UPOLE KATIKA RIWAYA YA *PENDO LA KARAHA*

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tunachunguza namna mikakati ya upole inavyojidhihirisha katika riwaya. Ili kufanikisha hili, utafiti huu unarejelea kauli mbalimbali za wahusika kama zinavyodhihirika katika riwaya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Kutegemea miktadha mbalimbali, kauli za wahusika zinazodhihirisha upole zinaainishwa katika kategoria nne za upole zilizopendekezwa na Brown na Levinson (1987). Kila kategoria inawakilisha mkakati mahususi wa upole. Chini ya kila kategoria kuna njia mbalimbali zinazodhihirika katika juhudi za kutekeleza kila mkakati. Mifano mwafaka kutoka kwa riwaya ya *Pendo la Karaha* inatolewa kuthibitisha jinsi kauli za wahusika zinavyodhihirisha mikakati ya upole. Maelezo ya kina yanatolewa ili kufanikisha uchunguzi katika kila kategoria.

Kulingana na Brown na Levinson (1987), kila mzungumzaji huwa na uso. Uso ni picha ya kibinafsi ya hadharani ambayo kila mtu hujichukulia nayo na hutaka wengine wamtambue kwayo. Picha hii hujumuisha hisia za kibinafsi ambazo huweza kuboreshwa, kudumishwa na hata kupotezwa. Aidha, upole unajumuisha kauli za msemaji zinauimarisha uso wa msikilizaji kwa lengo la kushughulikia hisia zake. Katika kushughulikia hisia hizo, Brown na Levinson (KHJ) wanapendekeza Mikakati chanya ya Upole (MCU), Mikakati hasi ya upole (MHU), Mikakati Ndani ya Rekodi (MNR) na Mikakati Nje ya Rekodi (MNjR). Mikakati hii inashughulikia mahitaji ya uso wa msikilizaji ili kuhakikisha kuwa mazungumzo yameendelea vyema bila kukatizwa na kuudhuru uhusiano wa wazungumzaji.

### 2.1 Kuwepo kwa Mikakati Chanya ya Upole (MCU)

Mkakati Chanya wa Upole (MCU) inahusu kupunguza vitendo vinavyotishia uso kwa msemaji kumhakikishia msikilizaji kuwa anathaminiwa na anahitajika. Msemaji anajichukulia kuwa katika kiwango sawa na msikilizaji na kumjumuisha katika mambo.

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa MCU hutumika iwapo wazungumzaji wana uhusiano wa karibu. Uhusiano huu unaweza kuwa kati ya wazungumzaji katika familia kama vile kati ya baba na mama, mzazi na mtoto, shangazi na mjomba au dada na kaka. Uhusiano huu vilevile unaweza kuwa kati ya marafiki wa karibu wanaoshirikiana katika mambo. Aghalabu,

wazungumzaji wanapowasiliana huwa na nia ya kushughulikia mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji. Msemaji hujaribu kwa hiari kushughulikia mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji ili kuendeleza mazungumzo. Baadhi ya mahitaji ni pamoja na msikilizaji kutambuliwa, kusifiwa, kupendwa na kushirikishwa katika mambo. Msikilizaji hapendelei kuaibishwa na kuudhiwa.

Katika *Pendo la Karaha,* njia sita zinachunguzwa ili kufanikisha uchunguzi wa MCU zikiwemo; njia ya kuwa na matumaini, kutambua mahitaji ya msikilizaji na kuyashughulikia, njia ya vitambulisho vya makundi, kutafuta makubaliano na kuepuka migogoro, kujumuisha wasemaji katika jambo na njia ya kuteua na kuchangia mada inayomvutia msikilizaji.

### 2.1.1 Njia ya kutambua mahitaji ya msikilizaji na kuyashughulikia.

Kipengele hiki kinahusu msemaji kutambua mahitaji ya msikilizaji na kutafuta namna ya kumtimizia mahitaji hayo. Kupitia kwa njia hii, msemaji hujaribu awezavyo kuyashughulikia mahitaji ya msikilizaji. Katika mawasiliano, msemaji hutambua kitendo kinachoweza kumkasirisha wa msikilizaji na kukiepuka. Vilevile, msemaji hutambua athari ambazo zinaweza kutokea iwapo hitaji fulani halijashughulikiwa. Msemaji anaweza kumshirikisha msikilizaji kwa kumpongeza, kumsifu na kumdhihirishia kuwa anamjali mpokezi wa ujumbe.

Katika riwaya ya *Pendo la Karaha* tunapata kwamba baadhi ya wahusika wanapowasiliana wanatambua mahitaji ya wenzao na kuwashughulikia kama ifuatavyo:

(1) **“Tunamwombea kila la heri, dadangu.** Habari za huko?” Subira alimwuliza Riziki huku akimtathmini na kushangaa jinsi pesa zinavyoweza kumpiga mtu msasa. Kweli pesa sabuni ya roho. “Huko ku salama ila hayo matatizo yetu ya kila siku,” Riziki alimweleza mwenzake ambaye ashavuka huo ukuta wa ukata na kuingia ulimwengu mwingine wa ukwasi; dunia ya kwanza. **“Yepi tena?”** Subira aliuliza huku amemtilia mwenzake makini yote. “Matatizo ya kukosa maji na huo umeme wao wa kupima, vyoo ambavyo twalalamikia kila kukicha, na hilo jinamizi la dawa, kokuteli, ‘unga’, bangi…si wewe unayajua…tena mbivu na mbichi. Hatulali wala hatuli, wasiwasi wetu ni juu ya wanetu. Kizazi kizima chafa na nduli ni dawa zinazowanunulia watu mashangingi na mitaa ya kifahari,” Riziki alimweleza Subira. **“Poleni, Mungu hamsahau mja wake, atakuja kuwaauni. Siku ya Mungu haijulikani dadangu,”** Subira alimshauri mwenzake. (Uk.15)

Kutokana na mfano wa (1), Subira katika mazungumzo yake na Riziki anaonekana kutambua kuwa Riziki alihitaji kusikilizwa na kutiwa moyo. Baada ya Rukia, bintiye Subira, kupata kazi ughaibuni, alimtumia mama yake fedha nyingi zilizomwezesha kuboresha maisha yake. Riziki kwenye upande wake alisalia kwenye umaskini. Mumewe Riziki, Mzee Sanga alikuwa ameuliwa baada ya kufichua siri kuhusiana na dawa za kulevya. Ilimbidi Riziki atie bidii zaidi ili kumlipia Kudra karo na kumtimizia na mahitaji ya kibinafsi. Riziki anapotaja matatizo yao ya kila siku, Subiri anamdadisi kwa swali, **"Yepi tena?"** ili atambue zaidi kile ambacho Riziki anakihitaji. Riziki naye anayataja matatizo yote anayokumbana nayo. Umaskini ulikuwa umemzidia, maji yalikosekana, walikoishi walikuwa wakipimiwa umeme na vyoo vyao vilikuwa katika hali duni. Katika eneo waliloishi, vijana walikuwa wameathirika sana na madawa ya kulevya yakiwemo bangi na kokuteli. Maisha haya yanaonekana kumsononesha Riziki. Subira anatambua kusononeka huku na kuamua kumshauri kwa kusema, **"Poleni, Mungu hamsahau mja wake, atakuja kuwaauni. Siku ya Mungu haijulikani dadangu,"** Subira anayashughulikia mahitaji ya Riziki. Anampa tumaini kwa kumjuza kuwa Mungu atawasaidia. Subira alimweleza Riziki kuwa alihitaji kuamini ya kwamba maisha yangebadilika na kuwa mazuri.

Vivyo hivyo, Rehema, wakala aliyewapeleka wasichana ughaibuni kutafuta ajira anaonekana kutambua mahitaji ya Kudra, bintiye Riziki kama ifuatavyo:

> (2) **"Karibu mwanangu,"** Kudra alikaribishwa na Rehema. **"Ahsante, bibi,"** Kudra alisema. **"Nikusaidie vipi mwanangu?"** Rehema alimwuliza Kudra. "Nimekuja kuulizia nafasi ya kazi huko Uarabuni," Kudra alijibu. …Rehema alizunguka ndani ya nyumba akifanya hili na lile. Baadaye, Kudra alimuaga. "Haya mama, mimi ninaondoka." Kudra alisema akiangalia giza nje. **"Sawa, mwanangu. Niandikie jina lako hapa,"** Rehema alisema. **"…Kumbuka kuniachia nakala ya kitambulisho chako,"** Rehema alimweleza Kudra. **"Nitafanya hivyo mama."** Kudra alisema kwa sauti legevu iliyolengwa kuonyesha utiifu kwa wakala wake. (Uk.22-25)

Kutokana na mfano wa (2), Rehema anamdadisi Kudra anapomuuliza, **"Nikusaidie vipi mwanangu?"** ili kufahamu kwa nini Kudra alikuwa amemtembelea. Kudra anajieleza kwa kutaja kuwa alikuwa anatumai kupata nafasi ya ajira uarabuni ili wakala aielewe nia yake kumtembelea. Rehema anayatambua mahitaji ya Kudra kuwa alihitaji ajira na kumshughulikia vilivyo. Rehema alijumuisha jina Kudra kwenye orodha ndefu aliyokuwa nayo ya wasichana waliotamani kupata

kazi. Rehema anatumia maneno haya, **"Sawa, mwanangu. Niandikie jina lako hapa."** Ombi la Kudra lilikuwa kupata ajira kama wasichana wengine ili ayabadilishe maisha yake na ya Riziki, mama yake. Riziki alimwelezea Kudra kuwa alihitaji kitambulisho chake aliposema, **"Kumbuka kuniachia nakala ya kitambulisho chako."** Rehema anadhihirisha kuwa alikuwa ameyachukulia mahitaji ya Kudra kwa umuhimu alipoagiza kitambulisho. Alikuwa amepiga hatua ya kwanza ya kumtayarishia Kudra safari ya Dubai. Kwa kufanya hivyo, Rehema anaonyesha kuwa ameyatambua mahitaji ya Kudra na yuko tayari kumtimizia Kudra ombi lake.

Mazungumzo kati ya Kidawa na Riziki yanaonyesha kuwa Riziki anayatambua mahitaji ya rafiki yake na kuyashughulikia kama ifuatavyo:

> (3) **"Pole Kidawa mwenzangu. Mambo ya kazi. Nina vikazi naona vinanizidia na huu uzee nilionao,"** Riziki alisema. **"Kazi ni maisha dadangu. Bila kazi mtu haishi. Sote tunategemea kazi. Hapana ubaya ukiishika pindi Mungu amekupa uzima,"** Kidawa alisema**. "Alhamisi hukuja dadangu,"** Riziki alimweleza Kidawa. **"Ni kweli. Hiyo Alhamisi kulikuwa …"** Kidawa alisema. (Uk.142)

Kutokana na mfano wa (3), maisha ya Riziki yalikuwa yamebadilika baada ya Kudra, bintiye Riziki, kupata kazi Dubai. Kudra alimtumia Riziki pesa zilizomwezesha kuhamia katika eneo jipya kwa jina *New Horizon.* Riziki alikuwa ameanza kuupuuza urafiki wake na Kidawa wa takriban miaka thelathini. Kidawa alipomtembelea Riziki, Riziki alijishughulisha kwa simu na bintiye Kudra. Siku moja Kidawa alikuwa amemtembelea rafikiye ila Riziki akampuuza waziwazi. Hatimaye, Riziki alitambua kosa lake na kumshirikisha Kidawa. Riziki alitambua kuwa hakumshughulikia rafiki yake ifaavyo. Aliamua kumwomba Kidawa radhi kwa kusema, **"Pole Kidawa mwenzangu. Mambo ya kazi. Nina vikazi naona vinanizidia na huu uzee nilionao,"** Riziki alitoa sababu ya tabia yake ili kufidia vitendo vyake. Kidawa alihitaji kutambuliwa na Riziki kama siku za awali. Riziki kwenye upande wake alitambua kuwa Kidawa alitaka wapige gumzo na akamshughulikia ipasavyo kwa kumjumuisha. Riziki anajishirikisha katika gumzo huku akimdadisidadisi Kidawa ili kujua sababu iliyomfanya kususia kufika kwake Alhamisi iliyopita. Kidawa alishirikiana na Rehema katika gumzo kwa kusema, **"Ni kweli. Hiyo Alhamisi kulikuwa na…"** Kidawa aliona juhudi za Riziki za kutaka kumshughulikia baada ya Riziki kuomba radhi na akampa maelezo zaidi ya kile kilichomfanya asifike kwake siku hiyo.

### 2.1.2 Njia ya vitambulisho vya makundi.

Njia ya vitambulisho vya makundi inahusu msemaji kumweka msikilizaji kwenye kategoria fulani kutegemea uhusiano wao. Makundi haya yanaweza kugawika katika misingi ya uhusiano wa kiukoo kumtajia mama, baba, ndugu, mjomba, bibi au hata shangazi. Vilevile kategoria hizi zinaweza kuwa za watu walio na uhusiano wa kirafiki au wenye tofauti za kiumri, ili kudhihirisha heshima. Katika kutumia njia hii, msemaji huonyesha uhusiano uliopo kati yake na msikilizaji kwa kutaja kikundi anachomjumuisha. Baadhi ya maneno yanayoweza kutumiwa kama vitambulisho makundi ni; dadangu, kakangu, mwanangu, mamangu, mke wangu miongoni mwa mengine.

Katika *Pendo la Karaha* vitambulisho makundi vinadhihirika katika mazungumzo kati ya Riziki na Subira ili kuwasilisha MCU kama ifuatavyo:

(4) “Niambie siri ya uganga huu,” Riziki alimchokoza. **“Siri dadangu wajua. Ni yule mwanangu Rukia…”** Subira alisema huku uso wake ukianza kutia urembo wa wazi, uking’ara kama lulu. **“Hongera dadangu**, Mungu amhifadhi huko Dubai aliko. Rukia ni mtoto mwema mwenye nemsi, atachuma tende atuletee nyumbani,” Riziki alisema akilikumbuka ombi la Kudra. (Uk.14-15)

Kutokana na mfano wa (4), uhusiano kati ya Riziki na Subira ulikuwa wa kirafiki. Japo kuwa wahusika hawa wawili hawana uhusiano wa kinasaba, Subira alipoulizwa swali na Riziki alijibu kwa kusema, **“Siri dadangu wajua. Ni yule mwanangu Rukia…”** Subira anamrejelea rafiki yake kwa kitambulisho makundi cha **dadangu** ili kuonyesha kuwa anamtambua. Kwa kutumia kitambulisho hicho cha makundi, kiwango fulani cha heshima kinazuka baina ya Riziki na Subira. Wanaitana dada. Riziki anajichukulia kuwa mmoja katika familia ya Subira. Riziki alimsifu Rukia, bintiye Subira na kumpongeza Subira kwa kusema, **“Hongera dadangu…”** Vilevile, Riziki alimpa Subira matumaini kwa kutamka kuwa Rukia angewaletea mazuri nyumbani. Kitambulisho makundi cha dada kinadhihirisha urafiki na ushirikiano wa karibu kati ya Riziki na Subira.

Kadhalika, mbinu ya vitambulisho vya makundi inajidhihirisha katika mazungumzo kati ya Rehema na Kudra kama ifuatavyo:

(5) **“Karibu mwanangu,”** Kudra alikaribishwa na Rehema. **“Ahsante, bibi,”** Kudra alisema. **“Nikusaidie vipi mwanangu?”** Rehema alimwuliza Kudra. “Nimekuja kuulizia nafasi ya kazi huko Uarabuni, Kudra alijibu. “Je, mama na baba wameridhia hilo?” “Mama hana neno. Mimi

> ni mtu mzima sasa …" Kudra alisema. **"Ni kweli mwanangu, lakini ni vizuri kukubaliana na wazazi ili mambo yaende sawasawa; yaani radhi za wazee, mama. Ukikosa utaburutwa na maisha."** Rehema alishauri akitabasamu. **"N'kutilie chai mwanangu?"** Rehema alimwuliza Kudra. **"Usijisumbue, mama,"** Kudra alijibu. "Keziah?" Rehema aliita. "Naam," **"Mletee mgeni angalau maji ya limau. Mwanangu usikatae kula au kunywa. Mimi ni mamako."** (Uk.22-24)

Kutokana na mfano wa (5), Kudra alikuwa amemtembelea Rehema kwa sababu alihitaji kuomba nafasi ya kazi za ughaibuni. Rehema alimkaribisha Kudra kwa kusema, **"Karibu mwanangu."** Rehema alimrejelea Kudra kama mwana, japo kuwa Rehema hakuwa mamake mzazi. Rehema alitumia kitambulisho makundi cha mwanangu alipomdadisi Kudra katika kauli hii, **"Nikusaidie vipi mwanangu?"** Rehema alidhihirisha kuwa alikuwa tayari kumsaidia Kudra. Riziki alitaka kujua iwapo Kudra alikuwa amemjuza mama yake kuhusiana na hitaji lake la kufanya kazi ughaibuni. Kudra aliweleza Rehema kuwa alikuwa tayari mtu mzima na hakuhitaji kuomba ruhusa kila wakati. Rehema alitafuta makubaliano na Kudra aliposema, **"Ni kweli mwanangu…"** Hata hivyo, baada ya Rehema kukubaliana na Kudra, alimshauri kuhusiana na kutafuta radhi za wazee huku akitabasamu. Aidha, Rehema alimdhihirishia Kudra ukarimu wa kutaka kumtilia chai kwa kusema, **"N'kutilie chai mwanangu?".** Rehema alijaribu kumrai Kudra akubali kula na kumweleza kuwa yeye ni mamake, **"…Mwanangu usikatae kula au kunywa. Mimi ni mamako."** Rehema alitumia maneno mwanangu na mamako ili kumdhihirishia Kudra kuwa alimchukulia kama bintiye. Vilevile, Rehema alijichukulia kama mama yake. Kwa kufanya hivyo, Kudra alijihisi kuwa amejumuishwa. Kwenye upande mwingine, Kudra anapomjibu Rehema anamrejelea kwa kitambulisho makundi cha bibi na kusema, **"Ahsante, bibi,".** Baada ya Rehema kujitolea kumtilia Kudra chai, Kudra vivyo hivyo alimtambua Rehema kwa kutumia neno la heshima aliposema, **"Usijisumbue, mama."** Kudra alijaribu kumjumuisha Rehema kwa kumtambua kwa jina la heshima, mama.

Isitoshe, njia ya vitambulisho makundi vilevile inajidhihirisha katika salamu kati ya Kudra, Bi. Fatila na Bwana Suleiman. Fatila, dada yake Nayrat na mumewe Suleiman, walikuwa wameitembelea familia ya Aminii, mwajiri wake Kudra. Kudra alikuwa amejibidiisha na kuwaandalia vyakula vya aina mbalimbali. Walipowasili nyumbani, Kudra aliwapokea kwa furaha na kudhihirisha heshima kama ifuatavyo:

(6) **“Salama Siti,”** Kudra alimwamkua Fatila. **“Salama,”** Fatila alijibu kwa tabasamu. **“Hujambo Seyyid?”** Kudra alimwamkua Suleiman huku akishuka na kuinama kwa heshima. **“Sijambo binti,** Suleiman alijibu huku akijaribu kumtathmini Kudra. (Uk.96)

Kutokana na mfano wa (6), Kudra aliwaamkua wageni kwa heshima. Kudra alimrejelea Fatila kwa jina la heshima la siti aliposema, **“Salama Siti.”** Fatila, baada ya kuona uchangamfu wa Kudra alimjibu kwa tabasamu. Kudra vilevile alimtambulisha Bwana Suleiman kwa kitambulisho makundi cha Seyyid aliposema, **“Hujambo Seyyid?”** Suleiman kwenye upande wake alimtambua Kudra kama binti aliposema, **“Sijambo binti”** japo kuwa hawakuwa na uhusiano wa kiukoo. Kudra, Fatila na Suleiman walirejeleana kwa majina ya heshima sana. Mazungumzo yao yalidhirisha ushirikiano kama alivyopendekeza Grice (1975). Ushirikaino huu na heshima kupitia kutumia vitambulisho makundi unachangia kudhihirisha MCU.

### 2.1.3 Njia ya kutafuta makubaliano na kuepuka mgogoro.

Kulingana na Brown na Levinson (1987), makubaliano katika mazungumzo hupatikana kupitia kwa kuwasilisha mambo yanayokubalika na wazungumzaji. Msemaji hutambua mambo yanayoweza kuridhiwa na msikilizaji na kuyatekeleza. Mambo hayo yanapotekelezwa, uhusiano kati ya wazungumzaji unaimarika. Makubaliano yanatokea ikiwa mahitaji ya msemaji ni sawa na yale ya msikilizaji katika mazungumzo. Mchakato mzima wa makubaliano unapotokea, MCU hudhihirika.

Katika *Pendo la Karaha***,** njia ya kutafuta makubaliano na kuepuka mgogoro inajitokeza katika mazungumzo kati ya Kudra na Riziki kama ifuatavyo:

(7) **“Mwanangu, chakula chako ni kitamu,”** Riziki aliusifu upishi wa binti yake. **“Kweli mama?”** Kudra aliitikia kwa swali. “Naona utampikia mkwe wangu chakula kizuri ukiolewa,” Riziki alimchokoza binti yake. **“Sipendelei kuolewa mama,”** Kudra ilimtoka kauli ambayo ilimkaa moyoni ila hakutaka mamake aijue. “Kwa nini? Mwanamke kuolewa ndio hatima yake, mama,” Riziki alimwambia mwanawe huku akijiongeza mchuzi wa nguru. **“Sidhani hivyo mama. Si kwa ubaya. Mimi ninataka kazi kwanza. Mambo ya kuolewa ni ya baadaye,”** Kudra alimweleza mamake msimamo wake. **“Utakavyo mwanangu. Mungu akujaaliye fungu la Baraka. Akufikishe utakako. Akupe**

> **hitaji la moyo wako. Mimi kama mamako nakupa radhi zangu mimi na za marehemu baba yako Mzee Sanga,"** Riziki alisema. (Uk.28-29)

Kutokana na mfano wa (7), Riziki aliusifu upishi wa bintiye kwa maneno, **"Mwanangu, chakula chako ni kitamu."** Riziki alitumia kanuni ya kusifa iliyopendekezwa na Leech (1983). Kudra alitafuta makubaliano na mama yake kwa kujitweza alipouliza swali, **"Kweli mama?"** ili Riziki amthibitishie. Wakati wa mazungumzo, Riziki alijishughulisha kuuongeza mchuzi wa nguru. Kudra alikuwa amejikakamua kukitayarisha chakula ili kumfurahisha mama yake. Riziki alianza kumdadisi Kudra kuhusiana na suala la kuolewa. Uhusiano kati ya Riziki na Kudra ulikuwa umejengeka. Kudra kwa uangalifu, alimjibu mama yake kuwa hakupendelea kuolewa, **"Sipendelei kuolewa mama."** Japo kuwa maoni ya Riziki na Kudra yalikuwa tofauti, wote walitafuta makubaliano. Riziki aliimarisha uso chanya wa Kudra alipompa uhuru kwa kumwambia, **"Utakavyo mwanangu…"** Riziki alimpa Kudra uhuru wa kuchagua kuolewa au kuyaboresha maisha yake kwanza na kumwondolea ulazimishaji. Pamoja na hayo, Riziki alimpa bintiye baraka kwa kusema, **"…Mungu akujaaliye fungu la Baraka. Akufikishe utakako. Akupe hitaji la moyo wako…"** Maneno ya Riziki yanadhihirisha kuwa hatutaka makabiliano kati yake na Kudra. Aliuepuka kauli zilizo na uwezekano wa kuzua mgogoro. Isitoshe, Riziki anamtajia Kudra kuhusiana na baba yake, **"…Mimi kama mamako nakupa radhi zangu mimi na za marehemu baba yako Mzee Sanga."** Uso chanya wa Kudra uliimarika baada ya Riziki kumtajia kuwa hakupata baraka za mama yake tu, bali pia baba yake, Mzee Sanga. Maneno hayo yanadhihirisha kuwa Kudra na Rehema walikuwa wamefikia makubaliano.

Katika hali nyingine, mazungumzo bungeni yanadhihirisha njia ya kutafuta makubaliano na kuepuka kutokubaliana. Mheshimiwa Kajembe, Spika na Mhesimiwa Jumbe ni washiriki katika mazungumzo hayo kama ifuatavyo:

> (8) **"Order! Order!"** Spika alisema huku akisimama. **"Bw. Ndugu Spika, naomba radhi kwa tabia yangu lakini imetokana na uzito wa jambo nililokuwa nikichangia,"** alisema Mheshimiwa Kajembe. Wabunge wengine walichangia vilevile kwa hasira na ghamidha. **"Tukate mahusiano na nchi hizi,"** alisema Mhesimiwa Jumbe. **"…Mimi binafsi Bw. Spika naona serikali imezembea jukumu lake" "Wewe unaona serikali ingefanya nini?"** Spika alimwuliza Jumbe. **"Jambo la kwanza… Mwisho ni kusema na nchi za Uarabuni waziwazi kuwa hao vijana**

> **wanaokwenda katika nchi zao si watumwa, ni watu…"** Jumbe alisema huku akipangusa jasho lililokuwa limetanda kwenye uso wake. **"Yee! Yee! Yee!"** Bunge lilivamia kwa **sauti za kumhimiza Jumbe.** "…Haki ya Mwafrika lazima iheshimiwe…," Jumbe alieleza huku uso wake ukionyesha ghadhabu. (Uk.173)

Katika mfano wa (8), Serikali inaonekana kupuuza kilio cha vijana waliokuwa wakienda ughaibuni kutafuta ajira. Mheshimiwa Kajembe alitoa maoni yake kuhusiana na mapuuza hayo ila akavuka mipaka. Katika kutafuta makubaliano, Spika alimsimamisha kwa kusema, *"***Order! Order!"** Spika alimtaka Mheshimiwa Kajembe aombe msamaha kwa kupuuza agizo la kuzungumza utaratibu bungeni. Bila kusita, Kajembe alifanya hivyo kwa kusema, **"Bw. Ndugu Spika, naomba radhi kwa tabia yangu…"** Baada ya kuomba msamaha, mgogoro bungeni ulipungua. Wabunge wengine walionekana kughadhabika kama alivyokuwa Mheshimiwa Kajembe. Spika alimteua Mheshimiwa Jumbe ili atoe mchango wake. Jumbe aliwasilisha kauli zake kwa kudhihirisha upole alipotamka, **"Tukate mahusiano na nchi hizi…"** Jumbe aliwasihi wakome kuhusiana na nchi zilizowadhulumu wafanyakazi wa Kiafrika kama njia ya kutafuta maridhiano na kuwapoza ghadhabu.

Kadhalika, Mheshimiwa Jumbe alitamka maoni yake kwa utaratibu katika kutafuta makubaliano aliposema, **"…Mimi binafsi Bw. Spika naona serikali imezembea jukumu lake."** Maneno Jumbe yalidhihirisha lugha ya adabu kwa kumtambua Spika kwa nukuu ya heshima, Bw. Spika. Jumbe vilevile alitumia neno naona, alipokuwa akidhihirisha maoni yake. Spika alimshirikisha kwa kumuuliza, **"Wewe unaona serikali ingefanya nini?"** Njia aliyoitumia Spika ni njia ya ujumuisho kwa sababu alitaka kupata maoni zaidi kutoka kwa Jumbe. Spika alitaka kujumuisha maoni ya Mheshimiwa Jumbe ili hoja zake zijadiliwe bungeni. Jumbe alitoa maoni yake kwa ufasaha aliposema, **"Jambo la kwanza… Mwisho ni kusema na nchi za Uarabuni waziwazi kuwa hao vijana wanaokwenda katika nchi zao si watumwa..."** Mheshimiwa Jumbe alihitimisha kauli zake kwa kuwasihi wabunge wenzake watafute mikakati ya kusema na mataifa ya Uarabuni. Hoja ya mwisho ya Jumbe ilihusu kuzungumza na nchi za ughaibuni ili kuwe na mkataba kuhusiana na wafanyakazi. Maoni ya Jumbe yalichangia sana katika kuleta makubaliano na wabunge wenzake. Mgogoro wa kuilaumu serikali ulikoma na wabunge wote wakaamua kuchukua hatua zaidi. Wabunge walimshabikia Jumbe na kufikia makubaliano kwa sauti moja, **"Yee! Yee! Yee!"** huku wakimhimiza. Kutokana na maneno ya Mheshimiwa Jumbe, bunge

liliungana kwa sauti moja na kutambua hatua ambazo zinahitajika kuchukuliwa. Mheshimiwa Jumbe hatimaye alimshukuru Spika kwa kumpa muda wa kuzungumza.

### 2.1.4 Njia ya kuteua na kuchangia mada inayomvutia msikilizaji.

Njia hii inahusu kuchagua na kushiriki katika mada inayomvutia msikilizaji. Kwa kufanya hivyo, msemaji anaudumisha uso chanya wa msikilizaji. Mada hizi zinapochaguliwa, uwezekano wa msemaji kumuudhi msikilizaji unakuwa nadra sana kwa sababu yanayozungumzwa ni yanaendana na mahitaji ya msikilizaji.

Katika *Pendo la Karaha,* njia ya kuteua na kuchangia mada inayomvutia msikilizaji inadhihirika katika mazungumzo kati ya Kudra na Riziki kama ifuatavyo:

> (9) **"Dadangu habari za Kudra?"** Kidawa alimwuliza. **"Kudra hatumsikii. Hupiga mara chache. Mkubwa wake hataki awasiliane na watu nyumbani sasa,"** Riziki alisema akiwa amejishika tama. "Kisa?" Kidawa alimwuliza akijaribu kumchua mgongo kwa maji ya mikoko. **"Nitajuaje dadangu?** Mambo ya uarabuni unayajua?" Riziki alisema akikunja uso kwa uchungu, Kidawa akimchua mgongo ili kuulainisha. … "Kwa nini? Kwani ana wazimu?" Riziki alilalamika. "Hana wazimu. Ndivyo dunia ya sasa ilivyo. Anakuchukua, anakuchezea kisha baadaye anakutupa," Kidawa alisema. Sasa alikuwa ameanza kumpikia Riziki uji wa mtama hapo jikoni. (Uk.122-123)

Kutokana na mfano wa (9), Kidawa anadhihirisha kuwa anayafahamu matatizo ya Riziki. Baada ya Kudra kupata ajira Dubai, Riziki alihitaji rafiki wa kumsaidia katika kazi za nyumbani na kumuuguza. Vilevile, Riziki alipatwa na upweke baada ya Mzee Sanga, mumewe, kuaga dunia na Kudra kuondoka nyumbani. Kidawa alimjumuisha Riziki kwa kutenga muda kumtembelea na kumpa nafasi ya kujieleza. Mara kwa mara, Riziki alipatwa na majonzi kwa sababu hakufahamu hali ya bintiye. Mwajiri wa kwanza wa Kudra, Bi. Nayrat hakutaka Kudra kuwasiliana na Riziki mara kwa mara kama alivyofanya awali. Hali ya upweke ilimzidia Riziki na afya yake ikaanza kuwa mbaya. Maumivu ya mgongo wa Riziki yalikuwa yamemzidia kiasi cha kutoweza kujipikia, kujipa dawa au hata kuchota maji. Kidawa alijaribu awezavyo kumshirikisha Riziki katika mazungumzo ili kumliwaza. Siku moja maumivu ya Riziki yalizidi. Kidawa aliamua kumsugua Riziki mgongo na kuchagua mada ya kuhusu Kudra. Kidawa alimshirikisha Riziki kwa kujaribu kujua habari ya Kudra huku akimuuliza, **"Dadangu habari za Kudra?"** Wakati wa mazungumzo,

Kidawa alizidi kumsugua Riziki mgongo ili apate nafuu kutokana na maumivu. Riziki alishiriki kwa kumweleza Kidawa mambo yalivyokuwa, **"Kudra hatumsikii. Hupiga mara chache…"** Mada kuhusu Kudra ilimvutia Riziki sana. Aliichangia kwa kumweleza Kidawa kuwa habari za Kudra zilimhuzunisha. Isitoshe, Riziki alimfichulia Kidawa kuwa mambo hayakuwa mazuri aliposema, **"…Mkubwa wake hataki awasiliane na watu nyumbani sasa."** Kutokana na mada hii, Kidawa aliweza kufahamu kilichokuwa kikimkabili Riziki. Pamoja na hayo, Riziki aliliwazwa na Kidawa kutokana na majonzi ya kukosa bintiye. Walizungumza kwa muda mrefu hadi mawazo ya kumkosa Kudra yakampungua.

### 2.1.5 Njia ya kujumuisha msemaji katika mambo.

Kujumuisha msikilizaji katika mambo kunaiteka makini ya msikilizaji na kuhakikisha kuwa muktadha wa mazungumzo umeeleweka vizuri. Msemaji akimjumuisha msikilizaji katika jambo huwa na lengo la kuzua ushirikiano kupitia kwa kitendo fulani.

Katika *Pendo la Karaha*, ili kudhihirisha ujumuishaji huu, kiambishi tu- cha wingi kimetumiwa katika mazungumzo kati ya Kidawa na Riziki kama ifuatavyo:

> (10) "Dadangu habari za Kudra?" Kidawa alimwuliza. "Kudra ha**tu**msikii. Hupiga mara chache. Mkubwa wake hataki awasiliane na watu nyumbani sasa," Riziki alisema akiwa amejishika tama. "Kisa?" Kidawa alimwuliza akijaribu kumchua mgongo kwa maji ya mikoko. "Nitajuaje dadangu? Mambo ya uarabuni unayajua?" Riziki alisema akikunja uso kwa uchungu, Kidawa akimchua mgongo ili kuulainisha. (Uk.122)

Kutokana na mfano wa (10), kiambishi **tu-** kimetumiwa na Riziki anapomwelezea Riziki kuhusiana na habari za Kudra. Riziki alisema, "Kudra ha**tu**msikii…" ili kumjumuisha Kidawa kama mtu mwenye ukaribu naye anayeweza kutaka kujua habari za Kudra. Riziki alimtambua Kidawa kama mmoja wa familia yake ili Kidawa ajihisi kuwa alithaminiwa. Kitendo cha Riziki kumtambua Kidawa kinachangia katika kudhihirisha MCU.

Mazungumzo kati ya Riziki na Subira vilevile yanadhihirisha njia ya kujumuishana katika mambo kama ifuatavyo:

> (11) "Niambie siri ya uganga huu," Riziki alimchokoza. "Siri dadangu wajua. Ni yule mwanangu Rukia. Tangu apate hicho kikazi chake Dubai, ame**tu**weka vizuri. Lakini yote ni

> ya Mungu. **Tu**namshukuru Maulana," Subira alisema huku uso wake ukianza kutia urembo wa wazi, uking'ara kama lulu. "Hongera dadangu, Mungu amhifadhi huko Dubai aliko. Rukia ni mtoto mwema mwenye nemsi, atachuma tende a**tu**letee nyumbani," Riziki alisema akilikumbuka ombi la Kudra. **"Tu**namwombea kila la heri, dadangu. Habari za huko?" Subira alimwuliza. (Uk.14-15).

Kutokana na mfano wa (11), kiambishi tu- cha wingi kimejitokeza katika usemi wa Subira, "…ame**tu**weka vizuri." Subira anapotumia kiambishi **tu-** anamjumuisha Rizika kama mmoja katika familia yake. Vilevile Subira alisema, "**Tu**namshukuru Maulana." Maisha ya Subira yalikuwa yamebadilika baada ya Rukia, bintiye, kupata kazi ughaibuni. Riziki naye alipotambuliwa kama mmoja wa familia ya Subira, alijijumuisha kwa kusema, "…Rukia ni mtoto mwema mwenye nemsi, atachuma tende a**tu**letee nyumbani." Riziki alimpa Rukia sifa tele na kusema kuwa angewatafutia mazuri na kuwaletea nyumbani. Riziki alitumia kiambishi *tu*- katika kujijumuisha Subira aliposema, **"Tu**namwombea kila la heri, dadangu." Riziki alijishirikisha kwa kumtakia Rukia mazuri. Alimtambua Subira kama dada yake, ilhali tunafahamu kuwa hawakuwa na uhusiano wowote wa kiukoo. Kama ilivyopendekezwa na Grice (1975), ushirikiano unaozuka baina ya Riziki na Subira unachangia kufanikisha mawasiliano yao. Riziki na Subira wanapojumuishana katika mazungumzo, MCU wa upole uliopendekezwa na Brown na Levinson (1987) unadhihirika wazi.

### 2.1.6 Njia ya kuwa na matumaini

Njia ya kuwa na matumaini inahusu msemaji kuwa na matarajio wakati wa mazungumzo. Njia hii huchangia msemaji kuuhifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kumpa tumaini kuwa anaweza kupata anachotamani. Msemaji anajihisi huru kumfanya msikilizaji jambo na kuamini kuwa matokeo yatakuwa mema. Aghalabu, uwezekano wa msikilizaji kuhisi kuwa ameshurutishwa kufanya jambo ni finyu kwa sababu anaamini kuwa anayotamani yanaweza kuafikika.

Katika *Pendo la Karaha*, njia ya kuwa na matumaini inachangia kudhihirisha MCU katika mazungumzo kati ya Kudra na Riziki kama ifuatavyo:

> (12) **"Ni hicho kikazi cha Dubai mama,"** Kudra alisema. **"Kila mtu mwanangu ana bahati yake. Usione bahati ya Rukia itakuja kuwa bahati yako, nao wakati ukifika Mungu atakuinua."** Mipango, mama, ni muhimu maishani.

> “**Hakuna werevu katika kukaa kutegemea majaaliwa. Lazima nifanye jambo hata kama ni dogo,”** Kudra alisema. “Naelewa mwanangu. Kufanya jambo ni muhimu lakini wakati ukifika. Si vizuri kuwa na pupa mwanangu wajua,” Riziki alieleza. (Uk.22)

Kutokana na mfano wa (12), Kudra anatumia maneno, **“Ni hicho kikazi cha Dubai mama,”** kuonyesha jinsi alivyokuwa akiitamani kazi hiyo. Kudra alikuwa amechoshwa na umasikini wa hapo nyumbani kwao. Kulingana na *Pendo la Karaha,* baba yake, Mzee Sanga alikuwa ameuliwa na kundi hatari kwa jina *Kuklax Klan* baada ya kufichua washirika wa madawa ya kulevya. Riziki aliachiwa jukumu la kumlea binti yao. Kudra alijihisi kama mzigo kwa mama yake na kuanza kutamani kazi za Ughaibuni. Kudra alitamani kazi hizo ili amwondolee mama yake hali ya umaskini. Riziki aliitambua nia ya Kudra na kumjuza kuwa lilikuwa jukumu lake kumtunza hadi ahitimishe masomo yake ya sekondari. Riziki alimpa bintiye matumaini aliposema, **“Kila mtu mwanangu ana bahati yake. Usione bahati ya Rukia itakuja kuwa bahati yako, nao wakati ukifika Mungu atakuinua.”** Riziki alimweleza bintiye kuwa bahati yake ilikuwa njiani ila Kudra alihitaji kuwa na matumaini kuwa mambo yangekuwa bora kuliko yalivyokuwa. Isitoshe, Riziki alimweleza Kudra kuwa Mungu angemwinua wakati wake ukifika kwa hivyo alihitaji kuwa mvumilivu. Matumaini ya Riziki kwa Kudra yalimchochea kutia bidii huku akitamani maisha mazuri. Vilevile, Kudra aliamini kuwa si lazima kutegemea majaaliwa alipotamka, **“Hakuna werevu katika kukaa kutegemea majaaliwa. Lazima nifanye jambo hata kama ni dogo,”** Kudra aliamini kuwa alihitaji kutia bidi maishani, sio tu kutegemea majaliwa. Pamoja na majaaliwa, Kudra alitia bidii na kutamani kuwa maisha yangebadilika. Hatimaye, wakati ulipotimia, maisha ya Kudra yalibadilika.

Katika hali nyingine, mazungumzo kati ya Kudra na Rehema yanadhihirisha njia ya kuwa na matumaini mema katika kama ifuatavyo:

> (13) **“Nina kazi nzuri mwanangu. Utaifanya miaka miwili tu kisha utatajirika. Utaweza hata kuwasaidia jamaa zako,” Rehema alisema. “Naomba iwe hivyo mama. Mzee wangu hawezi kujimudu. Ananitegemea mimi kwa kila kitu; chakula, dawa na kodi ya nyumba,”** Kudra alisema. (Uk.63)

Kutokana na mfano wa (13), maneno yanayotamkwa na Kudra yanadhahirisha matumaini. Kabla ya Kudra kumtembelea Rehema kwa mara ya pili, alikuwa amehangaika sana kutafuta ajira eneo

la Mombasa. Ukosefu wa ajira nzuri ulimfanya aanze kufikiria kazi za ughaibuni tena. Kudra alipokea habari kuwa wasichana walioenda Dubai walirudi nyumbani na pesa nyingi. Aliamua kurudi kwa Rehema na kumwomba nafasi nyingine ya kazi. Nafasi ilipotokea, Rehema alimwita Kudra na kumfahamisha. Rehema alimpa Kudra matumaini aliposema, **"Nina kazi nzuri mwanangu…"** Maneno aliyoyatamka Rehema mwanzoni yalimpa Kudra mwanga wa matumaini. Rehema alizidi kueleza, **"…Utaifanya miaka miwili tu kisha utatajirika…"** Kudra alitamani kutajirika. Alichukizwa na hali ya umasikini iliyowazunguka na kupania kuwa angeibadilisha hali hiyo. Rehema alimtajia Kudra jambo alilokuwa akilitamani kufanya kwa kusema, "…**Utaweza hata kuwasaidia jamaa zako."** Kudra alikuwa mwingi wa matumaini. Alitazamia kazi nzuri yenye mapato ya juu ili kumwezesha kuyabadilisha maisha ya Riziki, mamake. Katika kudhihirisha furaha na matumaini yake, Kudra alisema, **"Naomba iwe hivyo mama. Mzee wangu hawezi kujimudu. Ananitegemea mimi kwa kila kitu; chakula, dawa na kodi ya nyumba."** Kudra alitamani kuibadilisha hali ya umaskini katika familia yake. Kupitia kwa maneno ya Rehema, tumaini lilijengeka kwenye mawazo ya Kudra kuamua kujisajilisha upya ili aende ughaibuni kuzumbua riziki.

Vilevile, mazungumzo kati ya Almasi na Kudra yanadhihirisha kuwa Almasi alikuwa mwingi wa matumaini kama ifuatavyo:

> (14) "Hata mimi ni vivyo hivyo. Ila mimi ninapewa elfu mbili za Kenya." "Hizo nazo utafanyia nini?" Kudra aliuliza. **"Afadhali wewe. Mimi ninaomba nipewa hata shilingi moja tu,"** Almasi alisema. "Shilingi moja itakufaa aje nawe?" Kudra alimwuliza Almasi aliyecheka kama kizuka. "**Za kutuliza roho yangu tu, yaani, nafsi yangu ili nisijione kama mtumwa dadangu." "Pole dadangu.** Labda wanalipa maajenti, ajenti wako ni nani?" "Anaitwa Rehema," Almasi alisema. (Uk.113)

Kutokana na mfano wa (14), Almasi alikuwa amemjuza Kudra kuhusiana na madhila aliyopitia kwa Abdulla. Kudra alijaribu kumtuliza. Almasi alitamani kupata maisha mema aliposema, **"Afadhali wewe. Mimi ninaomba nipewa hata shilingi moja tu…"** Japo kuwa Almasi alifanya kazi vyema, mwajiri wake hakumpa hata senti. Almasi alitamani kupewa hela za kujisaidia. Hali duni ya Almasi ilidhihirika alipomtajia Kudra kuwa angefurahisha na hata shilingi moja. Kudra alishangaa kuona Almasi akiwa mwingi wa matumaini hata baada ya kumtajia matatizo aliyopitia. Almasi alisema, **"…Za kutuliza roho yangu tu, yaani, nafsi yangu ili nisijione kama mtumwa**

**dadangu."** Almasi alitamani kujihisi kama mfanyakazi anayepata mshahara na wala sio mtumwa. Kudra na Almasi walikuwa katika mazingira mabaya ya kazi ila walikuwa na matumaini kuwa maisha yangebadilika. Almasi alitamani kupata kipato chochote kizuri ili roho yake itulie. Katika mazungumzo yao, Kudra alitambua uzito wa mambo yaliyomkabili Almasi na kumpa pole katika misingi ya udugu.

Kadhalika, njia hii ya kuwa na matumaini inajitokeza katika *Pendo la Karaha* kwa lengo la kuendeleza MCU katika mazungumzo kati ya Riziki na Kudra kama ifuatavyo:

> (15) **"Sielewi mwanangu,"** Riziki alimwambia Kudra. "**Duka la ususi katika kitengo kimoja mtakuwa na watu wa kukanda. Hata huduma ya hina, mama tutaitoa papo hapo,"** Kudra alieleza huku akipima athari za maneno yake kwa mama yake. **"Sawasawa mwanangu, kipendacho roho ni dawa,"** Riziki alimkubalia mwanawe huku akimpa shime. (Uk.182)

Kutokana na mfano wa (15), Kudra alikuwa ameondoka Dudai baada ya kuteseka kwa miaka minne na Riziki alikuwa amempokea kwenye uwanja wa ndege huko Mombasa. Walikumbatiana kwa furaha na kuelekea nyumbani huku wakisimuliana mipango yao ya siku zijazo. Mfano huu unadhihirisha sifa ya Kudra kama mwenye matumaini kupitia anavyomweleza Riziki mipango ya biashara yao mpya. Kudra alimweleza mama yake kuhusu mipango hiyo huku akiupima uzito wa maneno yake kwa Riziki. Kwa upole, Kudra alimweleza Riziki hatua kwa hatua aliposema, **"Duka la ususi katika kitengo kimoja mtakuwa na watu wa kukanda. Hata huduma ya hina, mama tutaitoa papo hapo."** Kudra alimshirikisha Riziki kwa kusema kuwa wangeitoa huduma ya hina kwenye duka lao la ususi katika matamanio yake. Riziki aliyasikiliza matumaini yaliyowasilishwa na Kudra na kumpa shime aliposema, **"Sawasawa mwanangu, kipendacho roho ni dawa."** Riziki alitaka mwanawe atimize ndoto yake ya kuyabadilisha maisha yake. Kwa miaka mingi, Kudra alikuwa ameusubiri wakati ambao maisha yao yangebadilika. Matumaini ya Kudra yalizaa matunda kwa sababu aliweza kurudi nyumbani baada ya muda na kuanzisha biashara akishirikiana na Riziki. Kupitia Riziki kumpa Kudra matumaini, MCU unadhihirika katika *Pendo la Karaha*.

### 2.2 Kuwepo kwa Mkakati Hasi wa Upole (MHU)

Kulingana na Brown na Levinson (1987:129), Mikakati Hasi wa Upole (MHU) humpa msemaji uhuru wa kujiwasilisha. Msikilizaji huwa huru kuchagua, kukubali au kukataa jambo fulani wakati wa mawasiliano. MHU inahusu kutambua mahitaji ya uso hasi wa msikilizaji. Mahitaji haya ni

uhuru wa msikilizaji wa kutotaka kujihusisha na wengine. Faragha ya msikilizaji inapoingiliwa atahisi kuwa anasumbuliwa. Msemaji hapendelei kushirikishwa katika maswali, kupewa ushauri, kuombwa au hata kuelezwa mambo. Msikilizaji atataka nafasi yake iheshimiwe na asijumuishwe kwa lolote bila yeye kuridhia. Msikilizaji anatamani kuwa anachokusudia kufanya kisipate vizuizi kutoka kwa wengine. Uso hasi unahusisha msemaji kupunguza mahitaji na matamanio yake kutoka kwa wengine. Kilicho na umuhimu kwa msikilizaji ni anachokihitaji kutoka kwa wengine kama vile kuthibitishiwa mambo. Vilevile, msikilizaji hutaka aeleweke na kukubaliwa anaposema jambo bila kudadisiwa na wanaomzingira waonyeshe kuwa wamthamini na kumpenda.

Tofauti za kimazungumzo wazungumzaji wanapowasiliana aghalabu huwa dhahiri kwa sababu msemaji hutaka kuzungumza na msikilizaji ilhali msikilizaji huhisi kuwa faragha yake imeingiliwa. Msemaji akizidisha malalamishi kwa msikilizaji, msikilizaji anaweza kughadhabika na hata kumsababishia msikilizaji aibu. Katika *Pendo la Karaha,* MHU umejidhihirisha kupitia njia zifuatazo: kuomba msamaha, kutaja mambo kwa ujumla, kudhihirisha heshima baina ya wazungumzaji, kuwa bila matazamio na kutoa ubashiri wa matokeo mabaya.

### 2.2.1 Njia ya kuomba msamaha

Kuomba msamaha ni njia ya msemaji kuomba radhi baada ya kutambua kuwa amemkosea mpokezi wa ujumbe. Msemaji akimwomba msikilizaji msamaha atakuwa ameuhifadhi uso hasi wake. Kwa kufanya hivyo, msemaji amtazuia mpokezi wa ujumbe kuzidi kuwasilisha kauli ambazo zinaweza kumsababishia aibu au machukizo.

Katika *Pendo la Karaha,* njia ya kuomba msamaha inadhihirika katika mazungumzo baina ya Kudra na Nayrat kama ifuatavyo:

> (16) "Hakuna ruhusa kusema na majirani isipokuwa kama nimekutuma mimi mwenyewe," Nayrat alisema kwa sauti ya ukali huku mishipa ikiwa imemtoka shingoni. "Nilikuwa namwamkua tu yule jirani." Kudra alisema. "Ulikuja kufanya kazi ama kuamkuana?" Nayrat aliuliza. **"Pole, sitarudia tena,"** Kudra aliomba radhi. "Singependa urudie kosa hilo tena," Nayrat alimweleza. (Uk.94).

Kutokana na mfano wa (16), Nayrat alikuwa mwajiri wa Kudra. Wakati wote, Nayrat alimnyima Kudra uhuru wa kuzungumza na majirani bila ruhusa yake. Siku moja, Kudra alienda kinyume na

agizo la Nayrat na kumjulia hali. Nayrat alitambua kuwa Kudra alikuwa ameikiuka amri yake na kughadhabika. Kudra alifahamu kosa lake la kuzungumza na jirani ila hakutaka kutishiwa uso wake hasi. Nayrat alipoanza kumkabili, Kudra alimwomba msamaha ili kuupunguza uwezekano wa makabiliano mengine kuzuka. Kudra alisema, **"Pole, sitarudia tena."** Ombi hili lilimpoza Nayrat hasira na kumweleza Kudra kuwa hangependa alirudie kosa.

### 2.2.2 Njia ya kutaja mambo kwa jumla

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa kutaja kauli kwa jumla ni kusema kwa kujumlisha ili kuwasilisha kikundi mahususi cha watu. Kauli za msemaji hazinuiwi kumlenga mtu yeyoye mahususi moja kwa moja. Kwa kutumia ujumla, msikilizaji atapokea ujumbe bila kutiwa aibu mbele ya wengine.

Katika *Pendo la Karaha*, njia ya kutaja kwa jumla inadhihirika katika mazungumzo kati ya Rehema na Kassim kama ifuatavyo:

> (17) **"Mwanangu, ni mimi Rehema mamako,"** Rehema alisema huku pumzi zikimtoka. **"Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi? Mama yangu yuko Ujerumani,"** Kassim alisema. "**Nisikilize tu, sikukatizi kunywa wala kufanya lolote la utashi wako. Lakini rudi nyumbani."** Rehema alimrai Kassim aliyetokwa na ute mdomoni. **"Nyumbani sirudi. Kaeni na huo utajiri wenu wa kunadi watu ugenini. Mungu atawahukumu vibaya sana,"** Kassim alisema akitia tembe fulani nyeupe mdomoni. (Uk.80)

Kutokana na mfano wa (17), Kassim anahisi kuwa Rehema anamkatizia uhuru wake. Kassim alikuwa ameondoka nyumbani kwa sababu hakufurahia ubinafsi wa mama yake kupitia alivyokuwa akiendesha biashara yake. Baadaye, Rehema alianza kuugua na hisia za kumkosa mwanawe zilianza kumjia. Alianza juhudi za kumtafuta Kassim. Baada ya miezi minne, Rehema alimpata ila Kassim hakutaka kusumbuliwa wala kujihusisha naye wala utajiri wake. Kassim alitumia kauli za jumla ili kujizuia kumkosea mama yake heshima. Kassim alisema, **"Nyumbani sirudi. Kaeni na huo utajiri wenu wa kunadi watu ugenini…"** Kassim alitumia maneno, **kaeni** na **wenu** bila kumrejelea mama yake waziwazi ili asimkosee heshima. Katika kutamka kwake, Kassim alidhihirisha kanuni ya mkakati iliyopendekezwa na Leech (1983). Kassim alitimia namna ya kuufikisha ujumbe ule ule aliokuwa akiunuia bila kumtia aibu mama yake. Kassim alizidi

kutumia mkakati aliposema, **"…Mungu atawahukumu vibaya sana."** Alitumia kiambishi cha wingi **wa-** kutaja kwa jumla kwa sababu angetumia umoja, Rehema angehisi kuwa ameshambuliwa. Baadaye, maneno ya Kassim kuwa yeye ni mtu wala si shetani yalimfanya Rehema kujuta na kuanza kujihukumu. Rehema alianza kufikiria yale aliyokuwa akiwafanyia wasichana na akapania kuyabadilisha mambo.

### 2.2.3 Njia ya kudhihirisha heshima baina ya wazungumzaji

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), njia ya kudhihirisha heshima inajumuisha msemaji kuiweka thamani ya msikilizaji mbele wakati wa mazungumzo. Thamani hii inawekwa kwenye misingi ya tofauti za kiumri, uhusiano, cheo, nguvu na mamlaka. Ulazimishaji unachukua nafasi ya heshima katika muktadha wa mawasiliano na uso hasi wa wazungumzaji unahifadhiwa. Naye Yule (1996), msemaji mwenye hadhi ya chini hudhihirisha tofauti kubwa kati yake na msikilizaji katika hadhi ya juu. Uhusiano wa wazungumzaji hunachangia sana wanachokisema. Sifa za ukaribu wa wazungumzaji ni muhimu kuchunguzwa. Sifa hizi zinajumuisha uhusiano wa kiumri na nguvu. Msemaji anaweza kutumia majina ya heshima.

Katika *Pendo la Karaha,* heshima inadhihirika kwenye misingi ya nguvu katika mazungumzo kati ya Salim na Kudra katika kuendeleza MHU kama ifuatavyo:

> (18) **"Mambo yote nimesema kwenye hiyo barua. Usinisumbue kwa lolote…"** Salim alisema. *"***Tafadhali Kudra, tuheshimiane. Saa moja jioni isikupate ndani ya nyumba yangu. Ikikupata itabidi niite polisi wanisaidie kukuburuta." "Nakushauri uondoke salama. Usichukue chochote au ufanye jambo lolote la ujinga litakalokutia katika matatizo."** (Uk.146)

Kutokana na mfano wa (18), Salim alikuwa mwajiri wa pili wa Kudra huko Dubai. Salim mwanzoni alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na bintiye, Hanawi. Kudra alipoanza kufanya kazi kwa Salim, uhusiano kati ya Salim na Hanawi ulipungua. Salim alianza kumtaka Kudra kimapenzi na hatimaye uhusiano wao wa kimapenzi ukaanza. Hanawi alifahamu kuwa Kudra na baba yake walishirikiana kimapenzi na uadui kati yake na Kudra ukaanza. Salim alipoona kuwa chuki kati ya Kudra na Hanawi ilizidi, aliamua kumwachisha Kudra kazi. Salim hakuweza kumkabili Kudra ana kwa ana kwa hivyo aliamua kumwandikia barua. Kudra hakuwa radhi kuondoka kwa hivyo alimsubiri Salim ili amwombe nafasi zaidi ya kazi. Salim kwenye upande wake hakutaka kusumbuliwa na kujisumbua kumkaripia Kudra. Salim alitamka, **"Mambo yote nimesema**

**kwenye hiyo barua. Usinisumbue kwa lolote…"** Salim aliiandika barua ili Kudra aisome na afuate maagizo. Kudra hakuamini kuwa Salim hakumtaka kwenye nyumba yake hata baada ya uhusiano wao. Kudra alizidi kuomba nafasi nyingine ila Salim alihisi kuwa anasumbuliwa. Salim alitamka, **"Tafadhali Kudra, tuheshimiane. Saa moja jioni isikupate ndani ya nyumba yangu. Ikikupata itabidi niite polisi wanisaidie kukuburuta."** Salim alitaka heshima kudumisha baina yao. Uhusiano wao ulibadilika. Salim alitarajia kuwa Kudra angemtii na kuondoka bila vurugu. Salim alikuwa na nguvu zaidi kuliko Kudra na alikuwa na uwezo wa kuwaita polisi. Salim alitamka kwa uwazi hitaji lake huku akijaribu kuuhifadhi uso wake hasi. **"Nakushauri uondoke salama. Usichukue chochote au ufanye jambo lolote la ujinga litakalokutia katika matatizo."** Salim alimtisha Kudra kwenye misingi ya mwajiri na mwajiriwa kuwa iwapo angeiba chochote, angejipata kwenye matatizo. Kudra aliyaheshimu mahitaji ya uso hasi wa Salim na kuondoka.
Isitoshe, heshima kati ya wazungumzaji katika juhudi za kuendeleza MHU inajitokeza kati ya Mheshimiwa Kajembe na Spika kama ifuatavyo:

(19) **"Order! Order!"** Spika alisema huku akisimama. **"Bw. Ndugu Spika, naomba radhi kwa tabia yangu lakini imetokana na uzito wa jambo nililokuwa nikichangia,"** alisema Mheshimiwa Kajembe (Uk.172)

Kutokana na mfano wa (19), mazungumzo yanatokea bungeni. Awali, Mhesimiwa Kajembe aliposimama kutoa kauli yake, alidhihirisha wazi ghadhabu yake. Kajembe alienda kinyume na ustaarabu wa kuzungumza bungeni alipoelekezwa na Spika kunyamaza na kupuuza. Spika alijaribu kumtuliza kwa kusema, **"Order! Order!"** ila kutokana na ghadhabu, Mheshimiwa Kajembe hakuweza kumskia. Isitoshe, Kajembe alipiga vidoko bungeni. Majadiliano bungeni kwa kawaida, huwa na ustaarabu wa hali ya juu. Baadaye, Mheshimiwa alitambua kuwa alikuwa amelivujia bunge heshima. Spika alipomtaka Kajembe kuomba msamaha alifanya hivyo bila kusita huku alisema, **"Bw. Ndugu Spika, naomba radhi kwa tabia yangu lakini imetokana na uzito wa jambo nililokuwa nikichangia."** Kitendo cha Kajembe kuomba Spika msamaha kilipunguza hamaki bungeni. Uso wa Spika pia kama kiongozi wa bunge ulidumishwa. Heshima ya wasemaji inadhihirika wazi Mheshimiwa Kajembe anapomtambua Spika kwa nukuu ya heshima, **"Bw. Ndugu Spika…"** na kutii amri aliyopewa.

### 2.2.4 Kuwa bila matazamio

Kulingana na Brown na Levinson (1987), njia ya kukosa matazamio ni mkakati wa msemaji kupoteza hamu ya kupata vitu au mambo. Msemaji akidhihirisha kuwa bila matazamio atakuwa ameuhifadhi uso wake hasi kwa sababu hataathirika iwapo jambo halitatokea alivyotarajia.

Katika *Pendo la Karaha,* njia hii inajitokeza kudhihirsha MHU katika mazungumzo kati ya Kudra na Riziki kama ifuatavyo:

> (20) "Mwanangu, chakula chako ni kitamu," Riziki aliusifu upishi wa binti yake. "Kweli mama?" Kudra aliitikia kwa swali. **"Naona utampikia mkwe wangu chakula kizuri ukiolewa,"** Riziki alimchokoza binti yake. **"Sipendelei kuolewa mama,"** Kudra aliitoa kauli ambayo ilimtoa moyoni ila hakutaka mamake aijue. **"**Kwa nini? …" Riziki alimwambia mwanawe huku akijiongeza mchuzi wa nguru. **"…Mambo ya kuolewa ni ya baadaye."** Kudra alimweleza mamake msimamo wake. **"Utakavyo mwanangu…"** Riziki alisema. (Uk.28-29)

Kutokana na mfano wa (20), Riziki alitaka kujua msimamo wa bintiye kuhusu kuolewa. Riziki alianza kwa kusifu Kudra kwa upishi wake ili aweze kufahamu habari zaidi iwapo Kudra angependelea kuolewa au la. Riziki alitamka, **"Mwanangu, chakula chako ni kitamu,"** Kudra naye anajitweza kwa kuuliza, **"Kweli mama?"** Kudra alihitaji hakikisho kutoka kwa mama yake. Riziki na Kudra walidhihirisha mkakati wa kusifu uliopendekezwa na Leech (1983). Japo Riziki alidhamiria kuzungumzia mada suala nyeti, alitumia mkakati mwafaka kuhakikisha kuwa mwanawe hangehisi kuwa ameingiliwa sana. Riziki alizidi kumsifu Kudra kwa kutamka, **"Naona utampikia mkwe wangu chakula kizuri ukiolewa."** Kudra alitambua mbinu aliyotumia Riziki kupata habari na kuamua kumweleza msimamo wake aliposema, **"Sipendelei kuolewa mama."** Kudra alimwelezea Riziki kuwa hakutamani kuolewa. Aliyasema maneno hayo kwa ufasaha ili kumtayarishia mama yake kwa habari aliyonuia kuipitisha. Kudra alimweleza Riziki kuwa alitamani kazi kwanza alipotamka, **"…Mambo ya kuolewa ni ya baadaye."** Kudra alimweleza mama yake kuhusiana na msimamo aliouchagua kwa uangalifu. Hakutaka kutamka neno linaloweza kumuudhi Riziki. Kudra alijizuia kuwa na matazamio ya kumpata mume kabla ya kupata kazi. Riziki naye alidhihirisha kuuheshimu msimamo wa Kudra alipotamka, **"Utakavyo mwanangu…"** Maneno ya Riziki yanadhihirisha kuwa aliuheshimu msimamo wa bintiye na kamwe hakutaka kumvuruga.

Katika hali nyingine, njia ya kuwa bila matazamio kunajitokeza katika mazungumzo kati ya Rehema na Kudra kama ifuatavyo:

> (21) **"Hutaki kwenda mwanangu? Nimekuchukulia hadi viza mwanangu,"** Rehema alimwambia Kudra kwa tena kwa sauti nzito akimrai. **"Sitaki,"** Kudra alionekana kama kizuka aliyemweleza bila kutaka kumsikiza kwa muda mrefu. **"Kisa mwanangu? Nina mwajiri tayari. Nauli ya ndege ishalipwa…"** Rehema alisema. **"Sitaki kwa sasa mama. Samahani."** Kudra aliruka nje ya nyumba ya Rehema. (Uk.55-56)

Kutokana na mfano wa (21), kiu ya Kudra ya kusafiri kuelekea Dubai kusaka ajira ilikuwa imekatika ghafla baada ya kifo cha Rukia. Kudra alimtafuta Rehema ili kumweleza badiliko lake na azipate stakabadhi zake. Rehema alimrai Kudra ili aubadili msimamo wake aliposema, **"…Nimekuchukulia hadi viza mwanangu... Nina mwajiri tayari. Nauli ya ndege ishalipwa"** Kudra alishikilia msimamo wake. Hakutaka Rehema azidi kumrai kwa sababu matamanio yake ya kusafiri yalikuwa yamepotea. Ili kuhifadhi uso wake hasi, Kudra alisema, **"Sitaki kwa sasa mama. Samahani."** Kudra alijizuia vilevile kuudhuru uso chanya ya Rehema kwa kumrejelea kama mama kisha kwa haraka akajiondoa kwenye nyumba ya Rehema. Kudra alifahamu kuwa Rehema angejaribu kumrai abadilishe msimamo wake na hakutaka waanze kuvurugana.

Isitoshe, mazungumzo kati ya Mwadime na Riziki vilevile yanadhihirisha MHU kupitia kwa njia ya kuwa bila matazamio kama ifuatavyo:

> (22) **"Mwadime, kaka mimi ni mtu mzima."** Riziki alisema. "Uzima unakuzuia nini?" Mwadime alimwuliza taratibu huku amemtia jicho. **"Kaka, tunaweza kusaidiana lakini si hilo la kuoana,"** Riziki alisema kidogo akiwa na uzito. Mwadime anaonekana kama anayetaka kulia. **"Lifikirie kwa tuo nawe."** Mwadime alisema. **"Hata nikifikiria jibu langu litakuwa lilo hilo,"** Riziki alimweleza Mwadime (Uk.73)

Kutokana na mfano wa (22), Riziki haonyeshi matazamio yoyote ya kushirikiana kimapenzi na jirani yake Mwadime. Mumewe Riziki, Mzee Sanga alikuwa ameaga dunia. Vilevile, Mkewe Mwadime, Mwajuma naye alikuwa tayari ameaga. Mwadime alitamani kumwoa Riziki na kuwasilisha ombi lake. Riziki hakutaka kusumbuliwa kwa mada za ndoa. Riziki alihisi kuwa ametishiwa uso wake hasi baada ya kumweleza Mwamba kuwa hakutaka kujishirikisha katika

mambo ya ndoa na Mwamba kuzidi kumrai. Riziki alitamka, **"Mwadime, kaka mimi ni mtu mzima."** Mwadime alizidi kumrai Riziki kiasi cha kumkera na kuingilia faragha yake. Riziki aliamua kumpa Mwamba maelezo zaidi aliposema, **"Kaka, tunaweza kusaidiana lakini si hilo la kuoana."** Mwadime alizidi kumrai Riziki amkubalie ombi lake ila msimamo wa Riziki haukubadilika. Riziki alimwambia, **"Hata nikifikiria jibu langu litakuwa lilo hilo,"** kwa msisitizo. Riziki aliliweka wazi jambo alilolipa kipaumbele ambalo ni kuyaboresha maisha ya bintiye, Kudra na wala sio ndoa.

### 2.3 Kuwepo kwa Mikakati Ndani ya Rekodi (MNR)

Kulingana na Brown na Levinson (1987), Mikakati Ndani ya Rekodi (MNR) inahusu kutilia maanani mahitaji ya uso wakati wote. Mahitaji ya uso yanaweza kuwekwa kando iwapo kuna jambo linalohitajika kushughulikiwa kwa dharura. Mikakati hii inadhihirika aghalabu iwapo wazungumzaji wana uhusiano wa karibu. Wazungumzaji wanaweza kuwa wanafahamiana vizuri au wamezoeana kwa kiasi fulani. Lengo kuu katika MNR ni kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Mahitaji ya uso yakiwekwa kando msikilizaji huweza kunufaika kupitia ahadi zinazotolewa na msemaji na heshima wanayodhihirishiana. Msemaji huwasilisha ujumbe anaokusudia kwa msemaji moja kwa moja bila utata wowote. Ushirikiano unadhihirika kati ya wazungumzaji wakati wa kupitisha ujumbe muhimu. MNR ni mkakati unaoweza kudhihirika katika muktadha wa dharura, kimamlaka na muktadha wa kutoa ahadi kwa lengo la kumfaidi msikilizaji.

#### 2.3.1 Njia ya kushughulikia dharura.

Kushughulikia dharura kunatokea iwapo katika mazungumzo jambo linalotokea halikuwa limetazamiwa. Dharura ya kushughulikia jambo inawasababisha wazungumzaji kuyaweka mahitaji yao kando ili kuishughulikia. Msikilizaji ananufaika ikiwa tishio la uso linaloweza kutokea ni ndogo. Msemaji anaweza kutekeleza MNR kwa kumwonya msikilizaji dhidi ya kitu kinachoweza kumsababishia uchungu au mateso.

Katika *Pendo la Karaha,* dharura imeshughulikiwa katika kuendeleza MNR katika mazungumzo kati ya Rehema na Mzee Choka kama ifuatavyo:

> (23) **"Mzee, karibu,"** Rehema ilimtoka kauli na tabasamu midomoni. **"Asante, nimekaribia."** Mzee Choka hakuamini hayo ni maneno ya Rehema. Ni kama asali iliyotoka mdomoni mwa nyoka! Mzee Choka alikuwa mtu

> mpole. Mara nyingi watu walimchukulia kuwa mjinga kwa ajili ya upole huu. "Analonifikiria mtu kwangu halinidhuru," alipenda kusema. **"Karibu ukae,"** Rehema alisema huku amekaa kochini. **"Ahsante," "Ngoja nipumzike kidogo tutasema, jisikie uko nyumbani. Hapa ni kwako Mzee Choka,"** Rehema alitema maneno yaliyomshtua mzee wake, wa hapo zamani. **"Jisikie uko nyumbani,"** tena akaongeza na tabasamu yake iliyofanya yale macho yake makubwa kama tochi kuwaka. **"Hapa ni kwako."** (Uk.81-82)

Kutokana na mfano wa (23), Rehema alikuwa amezidiwa na hali ya upweke na maradhi. Awali, Rehema alikuwa amemfukuza mumewe Mzee Choka naye Kassim, mwanawe wa kipekee alikuwa ameondoka nyumbani. Rehema hakuweza kumshawishi Kassim kurudi nyumbani. Rehema aliamua kuchukua hatua ya dharura na kumtafuta mumewe na mwanao baada ya muda wa upweke. Hatimaye, Mzee Choka alirudi nyumbani. Rehema alikabiliwa na jukumu la kupunguza mahitaji yake kwa manufaa ya mumewe ili dharura yake ishughulikiwe. Rehema alitoa kauli, **"Mzee, karibu," "Karibu ukae,"** ili kumkaribisha mumewe. Mzee Choka alielewa dharura ya Rehema na kumshughulikia. Alikubali kukaa nyumbani kwa kusema, **"Asante, nimekaribia," "Ahsante."** Rehema alijaribu awezavyo kumjumuisha Mzee Choka ili kufidia kosa lake la awali alipokuwa amemfukuza. Rehema alitamka, **"…jisikie uko nyumbani. Hapa ni kwako Mzee Choka," "Jisikie uko nyumbani," "Hapa ni kwako.".** Rehema alikabiliwa na dharura ya upweke. Ili kupungukiwa na upweke, alimhitaji Mzee Choka. Rehema alimhakikishia Mzee choka kuwa hapo palikuwa kwake na hangemfukuza tena. Kassim naye aliwahitaji wazazi wake pamoja. Rehema na Mzee Choka walielewa kuwa hali ya Kassim ilihitaji kushughulikiwa kwa dharura. Wote walishirikiana ili kumsaidia Kassim kurudi nyumbani na kujenga maisha yake upya.

### 2.3.2 Njia ya kukabiliana na tofauti za kimamlaka.

Kulingana na Brown na Levinson (1987), tofauti za kimamlaka kati ya msemaji na mpokezi wa ujumbe huwa muhumu katika kudhihirisha upole katika mazungumzo. Tofauti za wazungumzaji zinajitokeza kupitia kwa maneno wanayotamkwa wahusika mbalimbali. Katika kudhihirisha MNR, aliye chini kimamlaka wakati mwingi atadhihirisha heshima kwa anayemshinda cheo au nguvu.

Katika *Pendo la Karaha,* tofauti za kimamlaka zinajitokeza kati ya bosi, Aminii na mwajiriwa, Kudra kama ifuatavyo:

(24) **“Nina jambo, samahani,”** Kudra alisema huku mikono yake ameiweka nyuma na kuinika uso kama inavyompasa kijakazi kama yeye. “Jambo gani?” Aliuliza Aminii huku akionyesha wasiwasi wa aina fulani. **“Ningependa muwe mkinikata nusu ya mshahara wangu ili niweze kumsaidia mama,”** Kudra alitoa ombi. “Lakini nilikwambia lazima nilipe madeni ya pesa ulizotumia kwanza” Aminii alifafanua tena. **“Pole kama nitakuudhi bwana mkubwa, lakini pia mimi ningependa kumsaidia mama yangu,”** Kudra alisema bila kutaka kuwaangalia wenyeji wake machoni asije akaambiwa hawaheshimu. **“Nitafikiria,”** Aminii alisema. (Uk.92- 93)

Kutokana na mfano wa (24), Kudra anapata ujasiri wa kuzungumza na waajiri wake, Aminii na Nayrat anapotamka, **“Nina jambo, samahani.”** Kudra aliongeza neno samahani katika usemi wake ili kudhihirisha wazi heshima aliyowapa waajiri wake. Kudra alizidi kuwasilisha ombi lake huku akiepuka ulazimishi aliposema, **“Ningependa muwe mkinikata nusu wa mshahara wangu ili niweze kumsaidia mama,”** Kudra aliwaeleza hali yake waziwazi kwa uangalifu asiwakosee heshima. Riziki, alikuwa amezidiwa na maumivu ya mgongo na hangeweza kujifanyia kazi yoyote. Aghalabu, Riziki alimtegemea Kudra kwa ufadhili wa pesa ila waajiri wake hawakumlipa mshahara wa kutosha kumtimizia Riziki mahitaji. Kudra alimweleza Aminii kwa heshima alipotamka, **“Pole kama nitakuudhi bwana mkubwa, lakini pia mimi ningependa kumsaidia mama yangu.”** Kudra alitumia maneno ya heshima, **pole** na **bwana mkubwa** ili kumdhihirishia Aminii kuwa alimshinda kimamlaka. Kutokana na unyenyekevu Kudra, hatimaye Aminii alimjuza kuwa wangelifikiria ombi lake. Aminii alikubali kumpa Kudra shilingi elfu moja za Kenya ili aweze kumsaidia mama yake.

### 2.3.3 Muktadha wa kumnufaisha msikilizaji.

Kumnufaisha msikilizaji katika mazungumzo kunahusisha msemaji kutoa usemi kwa lengo la kumfaidi mpokezi wa ujumbe. Juhudi za mazungumzo hulenga kumfaa msikilizaji kwa kudhihihirisha wazi ukarimu. Msemaji anaweza kujitolea kumsaidia msikilizaji kwa kumwonyesha ukarimu kama alivyoeleza Leech (1983) katika kanuni ya takrima. Isitoshe, maneno yanayosemwa yanahitaji kuwasilishwa kwa idadi tosha na kwa namna inayoepuka utata kama alivyopendekeza Grice (1975). Njia hii ya kumnufaisha inajitokeza ambapo msemaji huwa na lengo la kumdhihirishia msikilizaji kuwa anamjali.

Katika *Pendo la Karaha,* unufaishaji kwa msikilizaji unadhihirika katika mazungumzo kati ya Riziki na Kidawa kama ifuatavyo:

> (25) **"Pole Dadangu,"** Riziki alimweleza Kidawa aliyekuwa taabani walipofika nyumbani kwake. "Nishapoa dadangu. Ndivyo dunia ilivyo. Ndiyo jaza yangu," Kidawa alisema huku gharika la machozi likimshuka. (Uk.30)

Kutokana na mfano wa (25), mazungumzo kati ya Kidawa na Riziki yanatokea baada ya Lindo, mwanawe Kidawa kufariki. Riziki, Kudra na Mwadime walikuwa wameandamana hadi kwa Kidawa kumpa pole. Kidawa alionekana kuwa taabani kwa huzuni ya kumpoteza mwanawe. Japo kuwa Kidawa alikuwa amempoteza mtoto wake, alijaribu kujikaza ili awasiliane na majirani wake. Riziki alijaribu kumnufaisha Kidawa alipomwambia, **"Pole Dadangu,"** Maneno ya Riziki yalichangia pakubwa katika kumfariji Kidawa na majonzi yakapungukia.

Mazungumzo kati ya Kassim na wazazi wake yanadhihirisha kuwa Rehema na Mzee Choka wanatia bidii kumnufaisha mwanao kama ifuatavyo:

> (26) **"Karibu nyumbani,"** Rehema alimweleza bila kuamini mtoto huyo alikaa katika tumbo lake miezi tisa. "Sawa sawa," Kassim alisema na kucheka na kuyaweka wazi meno yake yaliyotanda ugaga mweusi. Nywele zake hazikuwa zimechanwa kabisa kwa miaka yote ya utoro wake. Hata Mzee Choka alishangaa kumwona mwanawe katika hali ile ya kutisha. **"Badilisha ndara uvae nyingine,"** "Niko sawa," Kassim alisema akicheka bila kizuio. **"Mwanangu, hauko sawa,"** Mzee Choka alimweleza kwa kumrai. (Uk. 83)

Kutokana na mfano wa (26), shughuli ya kumrejesha Kassim nyumbani baada ya kumpata ilimchukua Rehema muda. Rehema aliwatuma marafiki wa Kassim walioshiriki naye mihadarati wazungumze naye. Vilevile, Mzee Choka, baba yake Kassim alizidi kumrai mwanawe ili arudi nyumbani. Hatimaye, Kassim alirejea nyumbani kama alivyotaka Rehema. Kwa furaha, Rehema anamkaribisha mwanawe nyumbani kwa kutamka, **"Karibu nyumbani."** Maneno hayo yalichangia kumfanya Kassim ahisi kuwa amekubalika nyumbani. Kwenye upande wa pili, Mzee Choka anadhihirisha kumshughulikia mwanawe alipotamka, **"Badilisha ndara uvae nyingine."** Kassim hakuona tatizo na hali yake ilivyokuwa. Katika kumnufaishaKassim, Mzee Choka alimweleza, **"Mwanangu, hauko sawa."** Mzee Choka alitamka maneno hayo kwa lengo la kumzindua Kassim arejee katika hali yake ya awali. Rehema na Mzee Choka walishirikiana ili

kumfaidi Kassim. Rehema alimpeleka Kassim katika eneo la kurekebisha tabia za waraibu wa madawa ya kulevya. Baada ya kurejea hali yake ya awali, Rehema alimtuza kwa kumpa jukumu la kuiendeleza biashara yake.

Katika hali nyingine, jukumu la kumnufaisha msikilizaji linadhihirika kupitia kwa Kassim na Rehema anapozungumza na Rehema kama ifuatavyo:

> (27) **"Mama, kufanya faida si lazima uingie katika pato la mtu. Mimi ningependa tupate wasichana wengi zaidi iwezekanavyo na tujaribu kuwaeleza uhalisia wa maisha ya ughaibuni. Wenyewe wakiridhia ni sawa. Kisha waeleze jinsi wewe kama ajenti au wakala utakavyonufaika."** Kassim alimwambia Rehema. "Vipi? Mbona sikuelewi mwanangu?" **"Ninasema mama, tungependa kuwasaidia hawa wasichana kweli. Tupate watu ughaibuni walio na kandarasi za sawa, tupate watu ambao wanataka wafanyakazi wa kweli si watumwa mama. Pole mama kama ninakukosea heshima lakini hivyo ndivyo ninavyofikiri,"** Kassim alimweleza. "Haya panga. Kisha unaelewa? Bora biashara isishuke bwana," Rehema alisema. (Uk.103)

Kutokana na mfano wa (27), Rehema alikuwa amepokea onyo kutoka kwa Kassim kuhusiana na ubinafsi na alijaribu awezavyo kurekebisha makosa yake. Kassim akimweleza mama yake waziwazi walichohitajika kufanya katika kampuni yao. Kassim alimkumbusha Rehema kuhusiana na uadilifu alipotamka, **"Mama, kufanya faida si lazima uingie katika pato la mtu…"** Kassim alimweleza Rehema hayo huku akijilinda asimkosee heshima. Tamaa ya pesa ilimkabili Rehema, jambo ambalo lingemfanya ajipate kwenye mkono mbaya wa sheria. Ili kumnufai Rehema, Kassim alijikaza kupata ushauri kuhusu usimamizi mzuri wa kandarasi. Kassim alimpa Rehema maoni ya namna alivyotaka waiendeshe biashara aliposema, **"…Mimi ningependa tupate wasichana wengi zaidi iwezekanavyo na tujaribu kuwaeleza uhalisia wa maisha ya ughaibuni…"** Kassim alimweleza Rehema kwa utaratibu kuwa iwapo walihitaji kuleta mabadiliko katika biashara yao, walihitaji kubadilisha mtindo wao wa kuwasajilisha wasichana ughaibuni. Pamoja na hayo, walihitaji kuwafahamisha wasichana hao wazi kuhusiana na maisha ya ughaibuni yalivyo ili maisha yakiwa magumu kwao wasiwalaumu.

Katika juhudi za kumnufai Rehema, Kassim alisema, **"Ninasema mama, tungependa kuwasaidia hawa wasichana kweli. Tupate watu ughaibuni walio na kandarasi za sawa, tupate watu ambao wanataka wafanyakazi wa kweli si watumwa mama."** Rehema hakuelewa

wazi kile alichomaanisha Kassim. Hatua kwa hatua, Kassim alimweleza Rehema kuwa huko ughaibuni walihitaji kutafita waajiri ambao wana kandarasi zinazokubalika kisheria. Isitoshe, waajiri hao walihitaji kuchunguzwa kwa makini kuhakikisha kuwa wasichana wanaotumwa huko hawafanywi watumwa. Kassim aling'ang'ana ili Rehema asijipate katika mtego wa kulaghai tena. Alihakikisha kuwa kampuni hiyo inafuata taratibu za kisheria zilizohitajika. Kassim kwa uwazi alitamka maneno hayo ili kumwelimisha Rehema. Kassim alipoona kuwa ametamka zaidi, aliomba radha kwa kusema, **"… Pole mama kama ninakukosea heshima lakini hivyo ndivyo ninavyofikiri."** Kassim alimnufaisha Rehema kwa kumzuia kujipata katika mkono mbaya wa sheria. Kassim alidhamiria kuyaboresha maisha ya wasichana kwa manufaa yao na ya kampuni bila ubinafsi.

Vivyo hivyo katika kuendeleza MNR, mbinu ya kumfaidi msikilizaji inajitokeza katika mazungumzo kati ya Subira na mama yake, Shemsha Mpilipili kama ifuatavyo:

> (28) **"Vipi utokako, mwanangu?"** Mama yake Subira alimwuliza. "Sikuambulia lolote," Subira alisema na kuishiwa na nguvu huku akianguka mikononi mwa mama yake. (Uk. 53)

Kutokana na mfano wa (28), Subira alikuwa ametembea kwenye ubalozi wa United Arab Emirates, kupata habari kuhusiana na kifo cha Rukia, bintiye pamoja na mwili wake. Subira hakuweza kusaidika hivyo akaamua kurudi nyumbani kwake Mombasa, mtaa wa Amsterdam. Alipofika nyumbani, Subira aliwapata jamaa pamoja na mamake wakimsubiri. Shemsha Mpilipili anadhihirisha kumshughulikia Subira alipomuuliza, **"Vipi utokako, mwanangu?"** Subira alikuwa amevunjikiwa na moyo. Maneno ya Shemsha yalimfaa Subira kwa sababu aliweza kuzungumza nao kuhusiana na kilichokuwa kinamsibu. Subira alianguka mikononi mwa Shemsha, aliyemfariji. Jamaa waliomtembelea walimfaa katika kipindi hicho cha maombolezo.

### 2.3.4 Muktadha wa kutoa ahadi kwa msikilizaji.

Kulingana na Brown na Levinson (1987), kutoa ahadi na njia mojawapo ya kutekeleza MNR. Kutoa ahadi kunahusisha sharti ambalo msemaji hujipa ili kulitimiza. Katika mazungumzo, anayeahidi anakabiliwa na jukumu la kutekeleza agano kwa manufaa ya anayeahidiwa.

Katika *Pendo la Karaha*, muktadha wa kutoa ahadi unajitokeza katika mazungumzo kati ya Rehema na Rukia kama ifuatavyo:

(29) Rukia alibanduka shuleni akawa anafanya kazi ya kuuza leso kwa Rajiv hapo bondeni, Mombasa. Hapo ndipo alipokutana na wakala akamtia maneno, **“Njoo mwanangu nikupe kazi.”** Alisema Rehema kwa tabasamu tele midomoni. “**Kazi gani mama?”** Rukia alimuuliza Rehema. **“Kazi ya Uarabuni, Bi. Mdogo. Kazi wala sio huu utumwa wa Rajiv usiokufaidi.”** (Uk.5)

Kutokana na mfano wa (29), Rehema anaahidi kumpa kazi Rukia. Rehema alitumia maneno ya kuvutia ili kumrai Rukia aliposema, **“Njoo mwanangu nikupe kazi.”** Rehema alimwelezea Rukia kuwa alikuwa na nafasi ya kazi baada ya baba yake, Bw. Kipanga kuaga. Umaskini ulikuwa umemsonga Rukia akiwa na mama yake Subira. Katika kutoa ahadi yake, Rehema alisisitiza uzuri wa kazi aliyompendekezea Rukia kwa kusema, **“Kazi ya Uarabuni, Bi. Mdogo. Kazi wala sio huu utumwa wa Rajiv usiokufaidi.”** Kazi ambayo Rukia aliifanya kwa mwajiri wake Rajiv ilikuwa yenye kipato cha chini sana. Rukia hakuweza kumtimizia Subira mahitaji yake kwa kipato chake duni. Rehema alimnufaisha Rukia kwa kumpa nafasi bora ya kazi ughaibuni. Rukia hakuwa na budi kukubali nafasi hiyo na hatimaye maisha yao yakabadilika.

### 2.4 Kuwepo kwa Mikakati Nje ya Rekodi (MNjR)

Brown na Levinson (1987: 211) wanaeleza kuwa Mikakati Nje ya Rekodi (MNjR) inahusu uhuru wa wazungumzaji katika mawasiliano. Maneno ya msemaji hayamfungi kwa kile anachokisema kwa sababu anasema kwa mzunguko, bila uwazi. Mahitaji ya uso aghalabu hayatiliwi maanani. Msemaji anasema kwa mdokezo na kumsababishia msikilizaji utata wa kuamua kile haswa anachokirejelea. Msemaji anampa msikilizaji uhuru wa kuyawacha mawazo yake yatande katika uelewa wa kile anachodhani msemaji anakimaanisha. Namna ambavyo msikilizaji atafasiri ujumbe anaousikia inategemea uelewa wake. Msikilizaji anaweza kuufasiri ujumbe tofauti na namna msemaji anavyomaanisha. Katika kudhihirisha MNjR, ugomvi unaweza kuepukika katika mazungumzo. Aghalabu, hakuna ushahidi wazi wa jambo mbaya alilolisema msemaji kwa sababu msemaji husema kwa kufumba.

Katika *Pendo la Karaha*, MNjR inadhihirika katika; kutumia maswali ya balagha, mdokezo na kinaya kwa lengo la kuzua utata.

### 2.4.1 Njia ya kutumia maswali ya balagha ili kuzua utata

Maswali ya balagha ni aina ya maswali yanayodhihirika katika mazungumzo ila hayahitaji majibu kutoka kwa wazungumzaji. Maswali haya yanapojitokeza yanajenga mawazo ya msikilizaji na fasili ya anachomaanisha msemaji. Mkazo na ukweli wa maneno ya msemaji unadhihirika wazi. Maswali haya yanazua utata unaomfanya msikilizaji kuyaona mambo kupitia muona ulimwengu wa msemaji.

Katika *Pendo la Karaha*, ili kudhihirisha MNjR, maswali ya balagha yamejitokeza katika mazungumzo kati ya Zinduna na Rehema kama ifuatavyo:

> (30) "Tunamtafuta Kassim," Rehema alisema kwa taklifu kubwa. "Kassim hamumutoboi! Ni waangu, yaani miimi. Ziindunaa unaelewa? Eeeh? Eeeeh wangu mimi," Zinduna alisema, nusu hai, nusu mfu kwa ulevi. "Hatumtafuti masuala kwa hayo. Mimi ni mamake. Ni siku nyingi sijamwona," Rehema alisema. "Hayuko leo, ametookaa. **Ati wewe ni nani? Maama yake? Mbona ulii…muacha? Amesema hana maama?"** Zinduna alisema kisha akalala (Uk.79)

Kutokana na mfano wa (30), Rehema alikuwa amepatwa na maradhi ya moyo na hivyo ikambidi apumzike kutokana na kazi ya kuwalaghai wasichana ughaibuni. Rehema alishikwa na upweke uliomlazimu kuanza kumsaka mwanawe Kassim aliyepotelea katika matumizi ya mihadarati. Kassim aliishi na ajuza wa miaka sitini kwa jina Zinduna. Rehema alifika kwa Zinduna kutambua habari ya Kassim ila Zinduna alimuuliza, **"Ati wewe ni nani? Maama yake? Mbona ulii…muacha? Amesema hana maama?"** Maswali haya yanamfikirisha Rehema na kumpa shinikizo la kung'ang'ana ili ampate Kassim na ayabadiishe maisha yake. Licha ya Zinduna kuwa katika hali ya ulevi, maswali hayo yalimfanya Rehema kuona ukweli wa alivyomtekeleza Kassim. Katika hali nyingine, maswali ya balagha yanadhihirika katika kuendeleza MNjR katika mazungumzo kati ya Rehema na Kassim, kama ifuatavyo:

> (31) "Mwanangu, ni mimi Rehema mamako," Rehema alisema huku pumzi zikimtoka. **"Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi? Mama yangu yuko Ujerumani,"** Kassim alisema. **"…Nisamehe Mwwaaaa…"** Rehema pumzi zilimwisha. **"Nikusamehe nini? Jisamehe mwenyewe kwanza.** Sitamani haya mavolvo yenu. Mimi ninatumia baiskeli kama ndio kudura yangu toka kwa Mola. Mimi ni

mtu, si shetani," Kassim alimweleza George na mamake walioduwaa kwa maelezo yake. (Uk.80)

Kutokana na mfano wa (30), Rehema alikuwa amempata Kassim baada ya kumtafuta kwa muda mrefu. Rehema alijitambulisha kwa Kassim kuwa yeye ndiye mama yake mzazi. Rehema alikuwa amemtelekeza sana kwa hivyo Kassim hakutaka kumsikiliza wala kumkosea heshima mama yake. Kassim alimuuliza Rehema, **"Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi? Mama yangu yuko Ujerumani."** Kutokana na maswali hayo, Kassim alikuwa anaupitisha ujumbe kuwa Rehema hakuwajibika kama mama. Rehema aliomba msamaha ila Kassim alikabiliwa na ugumu kumsamehe. Kassim alitaka kuupitisha ujumbe kwa Rehema kuwa alihitaji kubadili mienendo yake aliposema, **"Nikusamehe nini? Jisamehe mwenyewe kwanza…"** Hili lilimaanisha kuwa iwapo Rehema angebadilisha tabia ya kuwadanganya wasichana, angemsamehe. Maswali haya yanadhihirika kwa mzunguko kuonyesha ugumu wa Kassim kumsamehe na kumfanya Rehema atambue makosa yake.

### 2.4.2 Njia ya kudokeza mambo ili kuzua utata.

Kulingana na Senkoro (2011), mdokezo ni njia ya msemaji kukatiza maneno ambayo ni wazi na yanaweza kuhitimishwa na msikilizaji. Msemaji anadokeza jambo hatua kwa hatua bila kulisema bayana. Kusema huku kunajenga utata. Mbinu ya kudokeza inahusu msemaji kumtayarisha msikilizaji kuupokea ujumbe unaoweza kuudhuru uso wake. Njia ya mdokezo inafanikishwa iwapo msikilizaji atashirikiana na msemaji katika kutatua utata unaoundwa na vidokezo hivyo.

Katika *Pendo la Karaha,* mdokezo unatumiwa na Dele pamoja na Kele wakimrejelea Kudra kama ifuatavyo:

(32) "Nyinyi washenzi kweli," Kudra alipasua maneno. **"Sisi washenzi? Tutakuja kuona washenzi ni nani,"** Kudra anakumbuka Dele na Kele wakimweleza. (Uk.148)

Kutokana na mfano wa (32), Dele na Kele wanatumia kidokezo cha swali la balagha walipouliza, **"Sisi washenzi?"** Vilevile, walidokeza kwa kusema, **"…Tutakuja kuona washenzi ni nani."** Kabla ya maneno hayo, Dele na Kele walimcheka Kudra alipowaeleza kuwa Salim alinuia kumuoa. Wawili hawa walijaribu kumjuza Kudra kuwa Salim hakuwa na nia ya kumwoa ila hawakutaka kumwambia Kudra waziwazi. Salim alikuwa na mazoea ya kushirikiana kimapenzi na waajiriwa wake na kuwafuta kazi hatimaye. Kudra alikiona kicheko chao kama cha kumkejeli

ila walikichukulia kama kidokezo kumtahadharisha. Kudra alitambua kuwa kicheko chao kilikuwa na maana baada ya kufurushwa na Salim.

**2.4.3 Matumizi ya kinaya ili kuzua utata.**

Wamitila (2008) anaeleza kinaya kama njia ya msemaji kutumia ya maneno ili kuzua maana inayopingana na yale anayonuia kuwasilisha kwa msikilizaji. Aghalabu, msemaji husema kinyume na anavyotarajia msikilizaji ili kudhihirisha kinaya. Msikilizaji huwa na jukumu la kushirikiana na msemaji ili kutambue kinyume cha kile anachomaanisha msemaji. Ushirikiano kati ya wazungumzaji ni muhimu ili kutambua kinachosemwa.

Katika *Pendo la Karaha*, njia ya kinaya inadhihirika katika kudhihirisha MNjR kwenye mazungumzo kati ya Lindo na Jannete kama ifuatavyo:

(33) **"… Unataka niharibu wewe bangi, na mimi ni mtoto wa pekee wa mama yangu,"** Jannete alitua maneno akavuta moshi wa sonyo ile. **"… Ninataka niwe mwana mtulivu kama mtewa. Sitaki kufanya ujanja maishani,"** Jannete alimaliza kuishauri ile bangi. "Ni nini hii?" Lindo alimwuliza Jannete. "Ni soda," Jannete alisema huku akicheka. "Mbona ni kali hivi?" **"Ina dawa kidogo ya kuulaza mwili ili uwe sawa lakini ni soda. Kwani unaogopa dawa?"** Jannete alimwuliza Lindo. (Uk. 33-35)

Kutokana na mfano wa (33), Lindo na Jannete ni waraibu wa madawa ya kulevya. Maneno ya Jannete kwa Lindo yanadhihirisha kinaya aliposema, **"…Unataka niharibu wewe bangi, na mimi ni mtoto wa pekee wa mama yangu."** Jannete alitumia neno la kuharibiwa na bangi, kama kwamba hakuwahi kuivuta. Maneno ya Jannete yanadhihirisha kinaya kwa sababu tayari alikuwa ameshaivuta na alikuwa na uzoefu wa kuitumia. Iwapo ni kuharibiwa, tayari bangi aliyoivuta kwa muda huo wote ilikuwa imeshamharibu. Vilevile, Jannete alitamka **"… Ninataka niwe mwana mtulivu kama mtewa. Sitaki kufanya ujanja maishani."** Jannete alisema kuwa hakutaka kuwa na ujanja wowote maishani ilhali maisha yake ya kila siku aliyaishi kwa ujanja. Jannete alijipata katika matatizo mengi kiasi cha kunusurika kifo waandamanaji walipovamia alikoishi. Ni kinaya kuwa Jannete alisema kuwa aliutaka utulivu maishani ila wakati mwingi matokeo ya bangi huzua vurugu. Isitoshe, Jannete alimdanganya Lindo aliposema, **"Ina dawa kidogo ya kuulaza mwili ili uwe sawa lakini ni soda."** Lindo alitaka kujua aina ya kinywaji alichokunywa Jannete. Kulingana na Lindo kinywaji hicho kilikuwa na ukali. Kinaya ni kuwa, Janette alimweleza Lindo

kuwa ilikuwa soda. Tunafahamu kuwa kwa kawaida soda huwa na utamu wa kiasi fulani ila soda hii aliyompa Lindo ilikuwa na ukali.

Kadhalika, njia ya kutumia kinaya vilevile inadhihirika katika kudhihirisha MNjR kupitia kwa maneno ambayo Kidawa anamwelekezea mwanawe Lindo kama ifuatavyo:

> (34) **“Kama unataka kulewa, lewa kabisa hiyo dawa ya unga ikuue, tutakuzika maana huna faida,”** Kidawa alimweleza Lindo kwa ghadhabu. **“Usimwambie hivyo dadangu,”** Riziki naye alimshauri mwenzake aliyekarambuka kwa fundo la hasira moyoni. **“Ana faida gani? Hayawani huyu hasa. Alewa kokuteli. Alewa ‘unga’.”** (Uk. 11)

Kutokana na mfano wa (34), Kidawa alimwambia Lindo maneno hayo baada ya kung’ang’ana kumshauri aachane na madawa ya kulevya bila mafanikio. Kidawa alitoa kauli kali kwa Lindo aliposema, **“Kama unataka kulewa, lewa kabisa hiyo dawa ya unga ikuue…”** Kidawa alimweleza Lindo waziwazi kuwa iwapo alitaka kulewa aendelee. Kidawa alimtamkia Lindo kuwa madawa hayo yangemuuwa. Kidawa alizidi kusema kwa ghadhabu, **“… tutakuzika maana huna faida.”** Kidawa alimweleza Lindo kuwa ikiwa yu tayari kufa afe ili azikwe kuwa hakudhihirisha faida yoyote. Kidawa aliyatamka maneno hayo kinyume na alivyomaanisha. Riziki alimshauri Kidawa dhidi ya kutamka hivyo aliposema, **“Ana faida gani? Hayawani huyu hasa. Alewa kokuteli. Alewa ‘unga’.”** Kidawa alinuia kuwa kutokana na uzito wa maneno yake, Lindo angehofia matokeo ya kutumia mihadarati. Kauli za Kidawa zinadhihirika kama kinaya kwani baada ya kifo cha Lindo, Kidawa alilia kwa uchungu wa kupoteza Lindo. Kidawa hangejishughulisha kulia iwapo hakumthamini mwanawe. Kadhalika, Kidawa alimpenda Lindo licha ya kubadilika na kuchukua mkondo uliosababisha na mauti yake.

**HITIMISHO**

Sura hii imejikita katika kuchunguza kuwepo kwa upole katika *Pendo la Karaha.* Uchanganuzi wa kauli zinazodhihirisha upole umefanywa kulingana na mikakati ya utoupole iliyopendekezwa na Brown na Levinson (1987). Uchanganuzi huu ulichunguzwa kwenye mikakati ifuatayo: Mikakati Chanya ya Upole (MCU), Mikakati Ndani ya Rekodi (MNR), Mikakati Nje ya Rekodi (MNjR) na Mikakati Hasi ya Upole (MHU). Kutegemea mifano ya kauli zinazodhihirisha upole katika sura hii, imebainika kuwa mikakati yote minne ya upole imedhihirisha kikamilifu.

Vivyo hivyo, imebainika kuwa MCU ndiyo mikakati uliopendelewa na wahusika katika kuendeleza mawasiliano kupitia kauli za wahusika zinazodhihirisha msemaji kutambua mahitaji ya msikilizaji, kutafuta makubaliano na kujumuishana katika mambo. Imebainika kuwa wahusika mbalimbali walidhihirisha mikakati hii ya upole kupitia kauli walizozitamka kwa lengo la kuimarisha na kudumisha mazungumzo yao. Tofauti za mamlaka, umri, uhusiano na urafiki zinachangia wahusika kuteua mikakati mbalimbali ya upole. Vilevile, hali ya maisha inayowakabili wahusika kama vile umaskini inachangia mhusika kuteua mkakati wa upole anaouona bora.

Pamoja na hayo, imebainika kuwa kuna baadhi ya wahusika wanaoshindwa kudhihirisha kauli fulani zinapoelekezwa kwao. Majibu yao yanapoenda kinyume na matarajio ya msemaji, utoupole unazuka. Kutokana na matokeo haya, sura ya tatu itachunguza hali ya utoupole inavyojidhirisha katika *Pendo la Karaha.*

# SURA YA TATU

# UTOUPOLE KATIKA RIWAYA YA *PENDO LA KARAHA*

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tunachunguza namna mikakati ya utoupole inavyojidhihirisha katika riwaya. Ili kufanikisha hili, utafiti huu utarejelea kauli mbalimbali za wahusika kama zinavyodhihirika katika riwaya *Pendo la Karaha* (Habwe, 2014). Kutegemea miktadha mbalimbali, kauli za wahusika zinazodhihirisha utoupole zitaainishwa katika kategoria tano za utoupole. Kila kategoria inawakilisha mkakati mahususi wa utoupole. Chini ya kila kategoria kuna njia mbalimbali zinazodhihirika katika juhudi za kutekeleza kila mkakati. Mifano mwafaka kutoka kwa riwaya ya *Pendo la Karaha* itatolewa kuthibitisha jinsi kauli za wahusika zinavyodhihirisha mikakati ya utoupole. Maelezo ya kina yanatolewa ili kufanikisha uchunguzi katika kila kategoria.

Kulingana na Culpeper (1996), utoupole unategemea upole kwa sababu katika kuutekeleza utoupole vyema, msemaji anahitaji ufahamu wa upole na kudhamiria kufanya kinyume cha anavyopaswa kufanya. Utoupole unajumuisha kauli za wahusika zinazoushambulia uso wa msikilizaji kwa lengo la kuvunja mawasiliano. Huenda, majibu yanayotarajiwa katika mazungumzo si yale yanayotolewa na msemaji. Culpeper (1996) anabainisha mikakati mitano ya utoupole ambayo ni; Mikakati ya Utoupole Ndani ya Rekodi (MUtNR), Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt), Mikakati Hasi ya Utoupole (MHUt), Mikakati ya Utoupole wenye Dhihaka (MUtD) na Mikakati ya Kuuzuia Upole (MKU). Kutokana na mikakati hii, tutachunguza njia mbalimbali ambazo wahusika wanatumia kudhuru nyuso za wengine.

### 3.1 Mikakati Hasi wa Utoupole (MHUt)

Kulingana na Culpeper (1996:358), Mikakati Hasi ya Utoupole (MHUt) ni mipango ilioundwa na msemaji ya kutumia maneno yanayodhamiria kuushambulia uso hasi wa msikilizaji. Shambulizi hili linahusu mazingira ya msikilizaji na haki zake za kuwa huru. Katika kudhihirisha mikakati hii msemaji humchokoza msikilizaji kwa lengo la kumuudhi huku akienda kinyume na matarajio ya uso hasi wa msikilizaji. Njia mbalimbali zinazoweza kutumiwa kutambua kauli za wahusika na ambazo zinawasilisha MHUt katika *Pendo la Karaha* ni pamoja na; msemaji kumhusisha

msikilizaji na maovu, kumpa msikilizaji vitisho au hata faragha ya msikilizaji kuingiliwa. Lengo kuu la kutekeleza mkakati huu ni kumdunisha msikilizaji.

### 3.1.1 Kumhusisha msikilizaji na maovu

Kulingana na Oruka (1990), maovu ni mambo ya kuchukiza yanayotendwa kwa lengo la kusababisha uchungu au kumdhulumu kisaikolojia mpokezi wa vitendo hivyo. Mambo haya yanaweza kujitokeza kupitia kwa tabia hasi ambazo msemaji anampa msikilizaji kwa lengo la kuudhuru uso wake hasi. Msemaji anatoa ushahidi kumhusisha msikilizaji na mambo hasi kwa kutumia uongo anapotumia kiwakilishi *wewe,* kumrejelea msikilizaji.

Katika *Pendo la Karaha*, njia ya kumhusisha msikilizaji na maovu inajitokeza katika mazungumzo kati ya Kudra na Suzzy kama ifuatavyo:

> **(1)** **"Hapa hapana mwizi, mgeni aliyekuja ndiye,"** Suzzy alisema. "Si mimi," Kudra alisema. **"Ni wewe,"** wote walisema kwa kauli moja. Suzzy alimkodolea macho na kumweleza **"Wewe wizi umekuleta Dubai, mwanamke gani wewe? Unataka kutajirika mara moja?"** "Si mimi, dadangu," Kudra alisema na kuangua kilio. (Uk.150-151)

Kutokana na mfano wa (1), Suzzy ananuia kuudhuru uso hasi wa Kudra kupitia maneno yake. Kudra hakutaka kuingiliwa wala kuvunjiwa heshima. Baada ya kuteswa na mwajiri wa kwanza na wa pili, Kudra alipata kazi ya kuwatunza wazee katika *The Home for The Old*. Kudra hakujihusisha na mambo yasiyomhusu katika eneo jipya la kazi. Kudra alijitenga na wasichana wengine na kufanya kazi yake kwa ufasaha. Katika kujipatia riziki, Kudra alidhihirisha mkakati wa huruma uliopendekezwa na Leech (1983) kwani alijitolea kuwasaidia wazee. Kudra alikuwa akiwapikia na kuwalisha wazee hawa. Vilevile, aliwaosha wale ambao hawakuwa na uwezo. Wazee walimpenda kwa sababu alikuwa mwenye huruma kwao. Wahudumu wenzake walimwonea Kudra wivu kwa sababu wazee hao walimtaka Kudra awahudumie.

Siku hiyo, Niri, mmoja kati ya wahudumu aliibiwa pesa. Wote walimshuku Kudra kwani ndiye aliyekuwa mgeni wa mwisho kuajiriwa katika nyumba hiyo, hivyo alikuwa bado mgeni kwao. Suzzy alimhusisha Kudra na tendo hilo la wizi aliposema, **"Hapa hapana mwizi, mgeni aliyekuja ndiye."** Kudra alijaribu kujitetea kuwa siye aliyeiba pesa za Niri. Kwa sababu walimchukia Kudra, wasichana wote walimshambulia kwa kusema, **"Ni wewe."** Suzzy naye alitoa kauli inayodhihirisha uhakika kuwa alifahamu kuwa Kudra alikuwa ameiba huku akisema, **"Wewe wizi**

**umekuleta Dubai, mwanamke gani wewe?"** Maneno haya yalimuudhi sana Kudra ambaye alitaka aheshimiwe na aendelee kufanya kazi yake ya kuwahudumia wazee akiwa huru. Hata hivyo tunamwona Suzzy akizidi kumshambulia Kudra alipomuuliza, **"…Unataka kutajirika mara moja?"** Kudra alihisi kuwa ameshambuliwa kwa njia hasi alipohusishwa na kitendo cha wizi. Kitendo hiki kilimfanya kujihisi kuwa amedunishwa. Baada ya ujumbe huo kumfikia Bw. Omar, msimamizi, alimhoji Kudra na kumhamisha katika kitengo kilichoshughulika na uhifadhi wa maiti.

Kadhalika, uso hasi wa mhusika Mwamba unashambuliwa anapohusishwa na maovu na jirani yake Kidawa kama ifuatavyo:

> **(2)** **"Wewe umemfanyia mwanangu dawa,"** Kidawa alisema. "Vipi jirani, mbona sikuelewi?" Mwamba alisema huku akiendelea kusuka ukili. **"Unajifanya wewe ni msusi kumbe ni mchawi."** "Sikuelewi Kidawa, Mwamba alisema huku ameacha kusuka ukili na kumwangalia Kidawa ambaye amegeuka kichaa. **"Hunielewi? Utanielewa. Mimi nitakwenda kukufanyia zinguo ili upate tabu kama mwanangu. Itakuwaje wewe jirani yangu ndiye wa kumsukuma mwanangu Lindo katika Dawa? Wewe tunayelala njaa pamoja,"** Kidawa alisema akionyesha ghadhabu. (Uk.43)

Kutokana na mfano wa (2), makabiliano makali yanajitokeza kati ya Kidawa na Mwadime. Kidawa alimhusisha Mwadime na maovu kwa kumwambia, **"Wewe umemfanyia mwanangu dawa."** Kidawa alimhusisha Mwadime na tabia za uchawi. Alimlaumu Mwadime kuwa alikuwa amemroga Lindo ili azame kwenye tope la dawa za kulevya. Mwamba tayari alikuwa ameshughulika katika kazi yake ila kauli za Kidawa zilivuruga makini yake katika kusuka ukili. Hakuyaamini maneno ya Kidawa. Kidawa alifoka, **"Hunielewi? Utanielewa. Mimi nitakwenda kukufanyia zinguo ili upate tabu kama mwanangu…"** Kidawa alimjuza Mwamba kuwa angemwendea kwa waganga ili amsababishie maovu kama alivyomfanyia Lindo. Bila kuusikiliza upande wa Mwamba, Kidawa alizidi kufoka, **"…Itakuwaje wewe jirani yangu ndiye wa kumsukuma mwanangu Lindo katika Dawa? Wewe tunayelala njaa pamoja."** Ghadhabu ya Kidawa iliweza kuhisika ila yote aliyoyasema yalikuwa makisio tu. Uso hasi wa Mwadime ulipata madhara kwa sababu ilimbidi aiache kazi aliyokuwa akiifanya na kuanza kujitetea kutokana na kauli za uongo zilizosemwa na Kidawa. Kulingana na nadharia ya utoupole, iwapo msemaji atambandua msikilizaji kwa jambo alilolizamia bila msikilizaji kutaka kuhusishwa, uso hasi wa

msikilizaji unapokea vitisho. Vilevile, Mwadime alikuwa anauthamini urafiki wake na jirani yake. Hakuelewa ni kwa nini Kidawa amhusishe na sifa ya kuwa mwovu.

### 3.1.2 Msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji

Faragha ya msikilizaji ni nafasi anayojipa yeye mwenyewe ambayo kwayo anajihisi huru na amehifadhika. Ni nafasi ya siri ya mtu ambayo wengine hawapaswi kuingilia. Wakati wa mazungumzo, msemaji anaweza kumuudhi msikilizaji anapoingilia faragha yake kwa kumfanya msikilizaji ahisi kuwa ameshambuliwa. Kulingana na Culpeper (1996), faragha ya msikilizaji inaingiliwa kwa sababu msemaji anataka kujua kuhusu anachokifanya msikilizaji. Nafasi ya kibinafsi ya msikilizaji inaingiliwa na hivyo kuuathiri uso wake hasi huku mahitaji yake yakipuuzwa.

Katika *Pendo la Karaha*, faragha ya wahusika inaingiliwa katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano katika mazungumzo kati ya Aminii na Kudra:

> **(3)** "... Sasa ningependa unipe pasi yako nikuwekee mahali salama," Saumu alisema. "Nitaiweka mwenyewe, dadangu," Kudra alisema. "Lakini hivyo ndivyo Bi. Mkubwa alivyoniagiza," Saumu alimwambia. "Sidhani nitakupa. Samahani," Kudra alisema. **"Mimi sitaki ubishi, ungesema kabisa na Fauziya asikulete huku. Huku ukija, basi lazima pasi yako uitoe,"** Saumu alisema akiwa amesimama na kwa **sauti ya juu** kama ambaye **alitaka kugombana**. "Dadangu, **mbona hutaki kufuata maagizo ya kazi?"** Saumu alimwuliza Kudra. "Mimi kazi hio siipendi, staki kuifanya," Kudra alisema. **"Lazima uifanye. Ikiwa hutaki kufanya, nitakufanya ufanye!"** Saumu alisema kwa hasira. (Uk.164-165)

Kutokana na mfano wa (3) tunapata kwamba Kudra alikuwa amepata kazi ya nyumba kwa Bi. Fauziya. Kudra aliifanya kazi hiyo kulingana na matarajio ya mwajiri wake. Bi. Fauziya aliifurahia kazi ya Kudra. Baada ya muda, aliamua kumhamisha Kudra kwenye *Massage Parlour*, ili akafanye kazi ya kuwakanda wateja viungo. Fauziya alimdanganya kuwa pesa zake zingekuwa maradufu. Kudra hakuwa na lingine ila kukubali kuhamishwa. Walipokelewa na Saumu, mama mwenye asili ya Kiafrika. Maisha ya Kudra yalibadilika baada ya Fauziya kuondoka. Saumu alimwagiza Kudra ampe pasi yake. Kudra alifahamu kuwa akiipeana pasi yake hatakuwa huru kuondoka iwapo hakuifurahia kazi hiyo. Kudra alihisi kuwa faragha yake ilikuwa imeanza kuingiliwa kwa kushurutishwa kuipeana pasi. Saumu alisema, **"… Huku ukija, basi lazima pasi**

**yako uitoe."** Kwa kiasi fulani, alimshurutisha Kudra kuitoa pasi. Saumu aliyasema maneno hayo kwa sauti ya juu iliyojaa ghadhabu. Saumu alimhusisha Kudra na sifa mbaya ya kukaidi maagizo alipotamka, **"Dadangu**, **mbona hutaki kufuata maagizo ya kazi?"**. Kudra alimweleza Saumu kuwa hakuipenda kazi aliyotakiwa kuifanya ila Saumu hakumsikiliza. Alizidi kumfokea Kudra kwa kusema, **"Lazima uifanye. Ikiwa hutaki kufanya, nitakufanya ufanye!"** Faragha ya Kudra inaingiliwa kwa kushurutishwa kufanya jambo kinyume na matamanio yake. Mahitaji ya uso hasi wa Kudra yalishambuliwa kutokana na kunyimwa uhuru wa kujiwekea pasi. Maneno ya Saumu yanamtishia Kudra uso wake hasi.

Vilevile, katika kudhihirisha mkakati hasi wa utoupole, vitendo vya Aminii vinaonyesha waziwazi kuwa anaiingilia faragha ya Kudra kama ifuatavyo:

> **(4)** Aminii naye alizoea kutoka kazini mapema, wakati mke wake hayuko nyumbani, kisha **anayapapasapapasa maziwa ya Kudra…**Aminii alizoea kwenda jikoni Kudra akipika na **kumgusagusa mabegani na kwingine kote mwilini.** Kudra hakupendelea tabia hii. **"Nitamwambia mama yako na mkeo."** (Uk.108)

Kutokana na mfano wa (4), maneno ya Kudra yanadhihirisha vitendo vya Aminii vya kuingilia faragha yake. Kudra anamtahadharisha Aminii kwa kumwambia kuwa angemshtaki kwa mama yake na kwa mkewe kutokana na vitendo vya kumshika maziwa yake na kwingineko mwilini. Aminii alikuwa na mazoea ya kumshikashika Kudra kwa njia ambayo hakuifurahia. Kutokana na hofu ya kuwa mwajiriwa, Kudra aliogopa kumkaripia Aminii. Kupitia maneno ya Kudra, tunafahamu kuwa alikuwa amevikinai vitendo vya Aminii anaposema, **"Nitamwambia mama yako na mkeo."** Maneno hayo yalimfanya Aminii kumpa Kudra uhuru wake kwani Aminii alihofia kuwa familia yake ingefahamu aliyokuwa akifanya. Japo kwa Kudra alihisi kuwa faragha yake imeingiliwa, hakujua la kufanya. Alihofia kuipoteza kazi. Aminii alimtaka kimapenzi ila Kudra alikataa, jambo ambalo lilimghadhibisha Aminii zaidi. Alianza kumchukia Kudra na kumwita maneno hasi kama vile kafiri, mwongo, mwizi na mzembe. Kudra alivumilia yote hata kutengwa wakati wa kula.

Vivyo hivyo, mazungumzo kati ya Kudra na Saumu yanaonyesha kuwa Saumu anaiingilia faragha ya Kudra kwa kupuuza mahitaji ya uso wake hasi, kwa mfano;

(5) **“Unaleta mchezo gani hapa? Wewe unadhani ni bora kuliko sisi? Pana wasichana warembo hapa. Ikiwa unadhani ulikuja raha, sahau. Ulikuja kufanya kazi. Ukichagua kazi ni shida yako. Mimi sitavumilia kiburi chako, Unaskia?”** “Ndiyo, ninasikia.” Kudra aliyesinasina alisema. (Uk.166)

Kutokana na mfano wa (5), Kudra hakufurahia kufanya kazi ya kumkanda mwili mwanaume aliyelipa pesa kustareheka kwenye *Massage Parlour,* kwa hivyo hakushirikiana na wenzake kuifanya kazi. Baada ya Saumu kufikishiwa ripoti, alimwita ofisini kumkabili. Kudra alimweleza Saumu kuwa hakutaka kuifanya kazi hiyo ila Saumu alimshurutisha kuifanya. Amri ya Saumu ilimsababishia Kudra huzuni. Siku nyingine, Kudra hakutaka kula. Saumu alifuatilia kujua kwa nini na kumwadhibu kwa viboko na makofi bila sababu. Saumu alitamka maneno makali baada ya kumwadhibu Kudra na kumuuliza, **“Unaleta mchezo gani hapa? Wewe unadhani ni bora kuliko sisi?”** Kudra alikuwa ameingiliwa faragha yake na Saumu kwa sababu alikuwa amekosa kula kwa hiari. Lengo la Saumu lilikuwa kumfanya Kudra ayafuate maagizo. Saumu alimfuatilia Kudra mara kwa mara kufahamu alichokifanya. Saumu aliingilia ubora wa Kudra na kumfanya Kudra ahisi kuwa alishambuliwa. Saumu alizidi kumshambulia kwa kusema, **“… Pana wasichana warembo hapa. Ikiwa unadhani ulikuja raha, sahau…”** Saumu aliingilia maumbile ya Kudra alipotaja kuwa kulikuwa na wasichana wengine warembo kuliko yeye kama njia ya kumchokoza, jambo linaloonyesha kuwa Saumu aliingilia faragha ya Kudra. Saumu alitamka maneno yake kwa lengo la kumdunisha Kudra na kumfanya afahamu kuwa hakuwa na jingine ila kufanya kazi aliyopewa.

Saumu alizidi kumshambulia Kudra kwa kusema, **“…Ulikuja kufanya kazi. Ukichagua kazi ni shida yako…”** Msikilizaji akiwa na uso hasi hapendelei kuambiwa mambo, haswa anayoyafahamu tayari. Kudra alifahamu kuwa alikuja kufanya kazi ila si katika misingi ya utumwa. Ni dhahiri kwamba Saumu anapomweleza Kudra, **“…Mimi sitavumilia kiburi chako, Unaskia?”** Kudra hakuwa na uhuru wa kuchagua. Kulikuwa na ulazimishaji katika maneno ya Saumu. Kudra alihisi kuwa alikuwa amenyimwa uhuru wa kujieleza. Hakuwa na jingine ila kulia na kukubali amri ya Saumu.

Pamoja na hayo, mazungumzo kati ya Nayrat na Kudra yanadhihirisha njia ya msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji kama ifuatavyo:

> **(6)** **“Hakuna ruhusa kusema na majirani isipokuwa kama nimekutuma mimi mwenyewe,”** Nayrat alisema kwa sauti ya **ukali** huku mishipa ikiwa imemtoka shingoni. “Nilikuwa namwamkua tu yule jirani.” Kudra alisema. **“Ulikuja kufanya kazi ama kuamkuana?”** Nayrat aliuliza. (Uk.94).

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), uso hasi wa msikilizaji huwa na mahitaji ya kuachwa huru kufanya uamuzi kuhusu mambo anayotaka. Naye Culpeper (1996) anaeleza kuwa mkakati hasi wa utoupole unadhamiriwa kwenda kinyume na mahitaji ya uso hasi wa msikilizaji. Iwapo msemaji atanyimwa uhuru na kuchunguzwa mara kwa mara atahisi kuwa faragha yake imeingiliwa. Haya yanadhihirika kupitia kutokana na mfano wa (6). Kudra alitaka uhuru wa kusema na aliotaka haswa majirani alipokuwa akifanya kazi kwa Bi. Nayrat na Bw. Aminii. Nayrat alikuwa amemuonya dhidi ya kuzungumza na majirani pasi ruhusa yake. Nayrat alitambua kuwa Kudra alikuwa ameenda kinyume na amri yake na kumweleza, **“Hakuna ruhusa kusema na majirani isipokuwa kama nimekutuma mimi mwenyewe.”** Kudra alijaribu kujitetea kuwa alikuwa akimjulia hali jirani ila Nayrat alizidiwa na hamaki. Alimuuliza Kudra swali la balagha, **“Ulikuja kufanya kazi ama kuamkuana?”** Hata kabla ya Nayrat kumkabili, Kudra alifahamu kuwa alikuwa ameivunja amri hiyo na kuomba msamaha. Aidha, uso hasi unajumuisha sifa ya msikilizaji kuchukia kuulizwa mambo. Nayrat alimfuatilia Kudra mara kwa mara kuona iwapo atalirudia kosa hilo. Kwa kufanya hivyo aliingilia faragha yake.

### 3.1.3 Kutisha.

Kulingana na Culpeper (1996), vitisho vinavyotolewa na mzungumzaji vikielekezwa kwa msikilizaji vinaweza kusababisha athari hasi kwa msikilizaji. Kutishwa kwa msikilizaji kupitia kauli zinazotamkwa na msemaji huzua hofu kwa msikilizaji.

Katika riwaya ya *Pendo la Karaha* tunapata kwamba baadhi ya wahusika wanapowasiliana wanawatolea vitisho wasikilisaji wao huku wakiziharibu nyuso zao kama ifuatavyo:

> **(7)** “**Umesema lakini hutaishi. Tutahakikisha kuwa tumekutia adabu.”** Kundi la *Kuklax Klan* liliapa. (Uk.12)

Kutokana na mfano wa (7), Kundi la *Kuklax Klan* lilikuwa likiwatisha wale ambao walikuwa wakitaka kuifichua siri yao ya ulanguzi wa madawa ya kulevya. Mzee Sanga alifahamu siri ya kundi hili. Aliificha kwa hofu kuwa maisha yake yangekuwa hatarini baada ya kutamka chochote. Mzee Sanga hakuweza kuvumilia kuiweka siri hii tena kwa sababu ya ongezeko la vijana

walioharibika kutokana mihadarati. Aliamua kuiibua siri. Wanakundi hilo waliapa kuwa wangemtia adabu kwa kutamka, "**Umesema lakini hutaishi…"** Kauli hii ilimaanisha kuwa wangemtafuta na kumuua kama njia ya kupitisha onyo kwa wengine. Uso hasi wa Mzee Sanga ulihasirika. Alihofia maisha yake. Vitisho vilizidi walipomhakikishia kifo kwa kusema, **"…Tutahakikisha kuwa tumekutia adabu."** Baadaye, kundi hili lilimtafuta na kumtoa uhai. Wengine waliofahamu kuhusiana na kundi hili la *Kuklax Klan* walifyata ndimi zao na kuyahofia maisha yao.

Kadhalika, mhusika Jannete, mmoja kati ya vijana waliolangua madawa ya kulevya anaonekana kutishwa na kuharibiwa uso hasi wake na kundi la waandamanaji katika:

**(8)** **"Muue! Muue!"** Kundi lilisema kwa hasira. (Uk.42)

Kutokana na mfano wa (8), Jannete alikuwa amekamatwa baada ya msako wa walanguzi wa madawa ya kulevya. Jannete alipelekwa polisi katika eneo la Makupa. Kwa hofu aliyokuwa nayo, Janette alikana kuwa alishiriki kulangua madawa ya kulevya. Hakuta kusema mengi ambayo yangelifanya kundi hilo lighadhabike zaidi. Kundi hii liliona kuwa Jannete hakuwapa taarifa waliyoitaka. Hawakutaka kumpa nafasi zaidi kujieleza. Hasira zilikuwa zimewapanda. Kwa hasira na sauti moja, kundi lilisema, **"Muue! Muue!"** Janette alitishwa kwa kifo. Kwa bahati nzuri, aliponea kifo kwani polisi wa kituo cha Makupa walimnasua kutokana na kundi hilo lililokuwa limepandwa na mori.

### 3.2 Mikakati wa Utoupole Ndani ya Rekodi (MUtNR)

Kulingana na Culpeper (1996), Mikakati wa Utoupole Ndani ya Rekodi (MUtNR) ni mipango wa kuwasilisha utoupole miongoni mwa wazungumzaji wenye uhusiano wa karibu. Uhusiano huu unaweza kuwa kati ya watu wanaoshirikiana katika mambo kama vile mama na baba, mjomba na shangazi, mzazi na mtoto, marafiki au hata mwajiri na mwajiriwa. Katika kudhihirisha MUtNR, kauli za msemaji zinawekwa wazi. Aidha, msemaji humwondolea msikilizaji utata wa anachonuia kukisema kwa kutumia kauli zinazoeleweka kwa urahisi kuufikisha ujumbe wake kwa msikilizaji. Nia kuu ya matamshi ya msemaji huwa ni kupitisha ujumbe. Msemaji hanuii kuushambulia uso wa msikilizaji. Aghalabu uso huo huwa hatarini kwa sababu mahitaji ya uso hayatiliwi maanani kabla ya ujumbe kumfikia mpokezi wa ujumbe huo. Msemaji anayataja mambo bila hofu ya

adhabu kutoka kwa msikilizaji. Katika kutambua MUtNR katika *Pendo la Karaha*, njia za kutumia onyo na taarifa moja kwa moja zinajitokeza.

### 3.2.1 Njia ya kutoa onyo

Onyo ni maneno ya msemaji ya kumtahadharisha msikilizaji aepuke kufanya jambo ambalo lina uwezekano wa kumdhuru. Onyo linalotolewa na mtu aliye na ujuzi wa mambo kuelekezwa asiyejua chochote ili kumuepusha na mabaya. Katika kudhihirisha Mkakati wa Utoupole Ndani ya Rekodi (MUtNR), msemaji anaweza kutumia amri ili kuwasilisha ujumbe wake. Msemaji anapotumia amri moja kwa moja anamwondolea msikilizaji uvulivuli wa kuelewa kile anachomaanisha. Msikilizaji anahisi kuwa hana namna nyingine ila kufuata amri hiyo. Msemaji anawekwa katika hali inayomfanya ahisi kuwa ameshurutishwa kufanya jambo.

Katika *Pendo la Karaha,* njia ya kutumia onyo katika kudhihirisha MUtNR imejitokeza katika mazungumzo kati ya Riziki na Kudra:

> **(9)** **"Hutoki hapa!"** Riziki alimfokea. "Mama, kwa nini umekuwa mkali? Kudra aliuliza. "Wewe ungali mtoto mdogo. Usifikirie mambo ya kazi hata yakakutanza. Kwanza fikiria masomo kisha baadaye utafikiria mambo ya kazi." Riziki alielekeza kwa matao ya chini huku amemtia mwanawe jicho la ukali. (Uk. 5)

Kutokana na mfano wa (9), Kudra alikuwa amemtajia Riziki kuwa alitamani kwenda Saudia kutafuta ajira. Mama yake alikuwa mkali. Riziki hakutaka kusikia habari zaidi kuhusiana na matamanio ya bintiye. Bila kumpa Kudra nafasi ya kujieleza, Riziki alimpa Kudra onyo aliposema, **"Hutoki hapa!"** Kutokana na onyo la Riziki, Kudra alifahamu kuwa Riziki alikuwa na sababu ya kusema hivyo na kumsikiliza. Maneno ya Riziki yalikuwa ya moja kwa moja. Kudra alifahamu bila utata kuwa mama yake alimaanisha alichokisema. Baada ya kuona kuwa ujumbe wake umemfikia Kudra, alimweleza sababu inayomfanya asimkubalie kutafuta kazi ili uhusiano wao udumu.

Kadhalika, mhusika Riziki anaonekana kumtahadharisha Kudra kwa mara ya pili kama njia ya kudhihirisha MUtNR kama ifuatavyo:

> **(10)** **"Hutaki shule, wataka nini? Kuolewa?"** Riziki alimsemesha Kudra kwa ukali. "Si kuolewa mama. Mimi nataka kazi ili nikusaidie ata wewe kujikimu." Kudra

alisema. **“Kama hutaki kusoma, hapa sikutaki na mimi, katu usipate kuniita mamako,”** Riziki alisema. (Uk.7)

Mfano wa (10) unadhihirisha kuwa Riziki alikuwa akimsisitizia Kudra kuwa alihitaji kumakinika masomoni ila Kudra aliwazia namna angetafuta ajira kwanza. Riziki alimweleza bintiye kuhusiana na umuhimu wa elimu ila maazimio ya Kudra yalikuwa tofauti. Riziki alighadhabika na kumuuliza Kudra, **“Hutaki shule, wataka nini? Kuolewa?”** Kudra alimweleza mama yake kuwa alihitaji kazi ili amsaidie kifedha. Riziki hakutaka kusikia hili. Alizidi kumpa Kudra tahadhari kwa kutamka, **“Kama hutaki kusoma, hapa sikutaki na mimi...”** Riziki alitamka waziwazi kuwa hangekubali kukaa chumba kimoja na yeyote asiyefuata ushauri wake. Kudra alielewa kuwa maneno ya mama yake yalihitaji kutiliwa maanani iwapo alinuia kuishi naye. Kuyatilia nguvu maneno hayo, Riziki alisema, **“…katu usipate kuniita mamako.”** Matamanio ya Kudra hayaafikiwi na mama yake. Jambo linaloafiki sifa kuu ya MUtNR kuwa mahitaji ya uso wa msikilizaji hayatiliwi maanani kwa lengo la kuufikisha ujumbe. Kudra anatahadharishwa kutilia maanani tahadhari aliyopewa na Riziki iwapo alitaka uhusiano wao udumu. Riziki alidhihirisha utoupole kwa kutamka maneno yenye ukali kwa bintiye bila kulegeza kamba.

Tahadhari ambazo zinadhihirishwa na Riziki zinachangia kuunda MUtNR. Utoupole unaojitokeza katika kauli za Riziki una umuhimu mkubwa kwa sababu ananuia kuirekebisha tabia ya bintiye ili abadili matamanio yake.

### 3.2.2 Njia ya kutoa taarifa

Taarifa ni ujumbe unaopitishwa na msemaji kwa msikilizaji ili kumfahamisha jambo. Ujumbe huu unaeleza mambo yalivyo waziwazi ili msikilizaji atambue uzito wa maneno ya msemaji. Katika kudhihirisha MUtNR, msemaji anaweza kutumia taarifa za moja kwa moja ili kuwasilisha ujumbe wake. Taarifa wazi za msemaji zinamwondolea msikilizaji uvulivuli wa kuelewa kile anachokimaanisha.

Mkakati wa Utoupole Ndani ya Rekodi unajidhihirisha kupitia kwa njia ya taarifa katika maneno ya Kidawa kwa Lindo kama ifuatavyo:

**(11)** **“Kama unataka kulewa, lewa kabisa, hiyo dawa ya unga ikuue tukuzike maana huna faida,”** Kidawa alimweleza Lindo kwa ghadhabu. (Uk.11)

Kutokana na mfano wa (11), Lindo alikuwa amezama katika utumiaji wa madawa ya kulevya. Kidawa alikuwa amezungumza naye mara kadhaa ila hakuibadili tabia yake. Kidawa alikuwa tayari amekinai kumrai. Ilibidi sasa ampe taarifa zilivyo bila kuyachuja maneno. Kidawa alimweleza waziwazi, **“Kama unataka kulewa, lewa kabisa…”** Kwa kutumia kinaya, Kidawa anampa Lindo taarifa kuhusu atakavyofanya. Kwamba iwapo angetaka kulewa, alewe kabisa. Kidawa anazidisha makali kwenye taarifa yake kwa kusema, **“…hiyo dawa ya unga ikuue tukuzike maana huna faida.”** Kidawa alimtajia Lindo kuwa hakudhihirisha faida yoyote. Kidawa alitamka maneno haya kwa lengo la kumpa Lindo mwamko wa kiakili ili aweze kubadilika. Maneno ya Kidawa yananuiwa kuuharibu uso wa Lindo anapoelezwa kuwa hana faida, na ikiwa yu tayari kufa afe ili azikwe.

Vivyo hivyo, njia ya kutoa taarifa inajitokeza katika kudhihirisha MUtNR kupitia maneno ya Kassim kwa Lindo kama ifuatavyo:

> **(12)** **“Nikienda kusoma, baba yako atanilipia karo?”** Lindo alimwuliza Kassim. “**Atakulipiaje? Hakukuzaa. Tena wewe ni mwanaharamu. Wafanyie watu kazi wakitajirika na wewe ukidamirika kama unyasi katika kiangazi,”** Kassim alidakia. (Uk.45- 46)

Kutokana na mfano wa (12), Lindo alikuwa amefika kwa Mwamba ili kuucheza mchezo wa bao. Kassim na Lindo walianza kuzungumza kwa mzaha. Kassim alimtaka Lindo arudi shuleni. Lindo alimuuliza Kassim, **“Nikienda kusoma, baba yako atanilipia karo?”** Lindo alifahamu kuwa Kassim alikuwa ametoroka nyumbani na baba yake, Mzee Choka, alikuwa tayari ametengana na mkewe Rehema. Kassim naye alifahamu kuwa Lindo hangeweza kurudi shuleni. Kila mmoja alionekana kuvutia kwake. Katika kujitetea, Kassim alimweleza Lindo, **“Atakulipiaje? Hakukuzaa. Tena wewe ni mwanaharamu…”** Kassim alimweleza Lindo kuwa Mzee Choka hangeweza kumlipia karo mtoto ambaye si wake. Kassim alimweleza Lindo kuwa alikuwa mwanaharamu. Huu ulikwa ukweli mchungu alioufunua Kassim kupitia kwa taarifa yake. Kulingana na MUtNR, mahitaji ya uso wa msikilizaji huwekwa kando ili kuupitisha ujumbe. Bila kujali hisia za Lindo, Kassim alimweleza Lindo waziwazi aliposema, **“…Wafanyie watu kazi wakitajirika na wewe ukidamirika kama unyasi katika kiangazi.”** Maneno ya Kassim kwa Lindo yalimfanya afikirie zaidi kuhusu maisha yake na kufahamu kuwa alihitaji kubadilisha maisha yake.

Katika hali nyingine, maneno ya Rehema kwa mwanawe, Kassim yanadhihirisha taarifa muhimu inayochangia kuwasilisha MUtNR kama ifuatavyo:

> **(13)** **"Potelea mbali! Akitaka kusoma, asipotaka kusoma ni shauri yake. Maisha ni yake. Ni yeye atakayemenyana nayo mwenyewe."** (Uk.78)

Kutokana na mfano wa (13), Kassim alikuwa ametoroka shuleni. Hakuweza kuyahitimisha masomo yake. Kassim alikuwa mwerevu sana shuleni ila wanafunzi wenzake walichangia kutoroka kwake. Alianza kutumia madawa ya kulevya. Kassim aliasi masomo akiwa katika shule ya upili ya Shimo la Tewa. Rehema, mamaye Kassim, alimbembeleza mwanawe tu kiasi cha haja arudi shuleni. Alipokataa, Rehema alisema, **"Potelea mbali! Akitaka kusoma, asipotaka kusoma ni shauri yake…"** Taarifa anayoitoa Rehema inadhihirisha utoupole kwani hajali kuhusiana na maisha ya mwanawe ya siku zijazo. Anazidisha makali maneno hayo kwa kusema, **"…Maisha ni yake. Ni yeye atakayemenyana nayo mwenyewe."** Rehema analipuuza jukumu lake kama mzazi kumwelekeza Kassim kwa njia nzuri. Kulingana na mkakati wa utoupole ndani ya rekodi, kauli za msemaji zinawekwa wazi kwa lengo la kuupitisha ujumbe. Rehema alidhihirisha kuwepo kwa MUtNR alipotamka kauli zake waziwazi ili Kassim aupate ujumbe ulivyo. Mahitaji ya uso wa Kassim hatiliwi maanani, mradi tu Rehema ameifikisha taarifa yake.

Kadhalika, tunapata maneno ya Rehema kwa Mzee Choka, mumewe, yakiwasilishwa kupitia matumizi ya taarifa na hivyo basi kudhihirisha MUtNR kama ifuatavyo:

> **(14)** "**Tafuta lako, kaka. Sitaki kusumbuliwa,"** Rehema alimwambia mzee wake. "sawa." (Uk.57)

Kutokana na mfano wa (14), Rehema aliitamka kauli yake kwa Mzee Choka kwa njia wazi kiasi kwamba Mzee Choka alielewa bila tatizo kile alichomaanisha Rehema. Aghalabu, Rehema na Mzee Choka waligombana kila wakati. Siku moja katika ugomvi wao Rehema alimwambia mumewe, "**Tafuta lako, kaka…"** Rehema alikuwa amechoshwa na ugomvi huo na kuamua kumpa Mzee Choka talaka. MUtNR unajidhihirisha kupitia uwazi wa maneno ya Rehema huku akiyapuuza mahitaji ya uso wa Mzee Choka kando. Rehema anafikia kiwango cha kumwita mumewe kaka. Rehema alieleza kuwa hakutaka kuhusiana na Mzee Choka tena alipotamka, **"…Sitaki kusumbuliwa."** Kutokana na maneno hayo, Rehema alimweleza mumewe kuwa hakutaka ndoa iliyojaa usumbufu. Uwazi wa maneno ya Rehema ulichangia Mzee Choka kuupata

ujumbe kwa urahisi kuhusu mahitaji ya mkewe. Japo kuwa Mzee Choka hakutaka kuondoka, ilimbidi aweke mahitaji yake kando na kuondoka.

Vivyo hivyo, kulikuwa na mhudumu katika hoteli iliyojulikana kama *Oak Tree*. Maneno ya mhudumu huyo yanadhihirisha MUtNR kama ifuatavyo:

> **(15)** "Nikusaidie vipi?" Kudra aliulizwa katika hoteli ya *Oak Tree* na mhudumu. "Ninatafuta kazi," Kudra alisema. "Kazi gani? Wewe ni mpishi?" "Aaa si…ni…ninaweza hiyo," Kudra alimjibu mhudumu kwa kuchanganyikiwa kwingi. **"Huna hakika dadangu ya kile ukisemacho,"** alisema mhudumu **kwa ujeuri na akafunga kiofisi** chake. (Uk.59)

Kutokana na mfano wa (15), Kudra alionekana kuwa amechanganyikiwa sana. Mhudumu alimuuliza Kudra maswali wazi ili kumwezesha kufahamu kilichomleta Kudra hapo. Kudra hakufahamu haswa kazi ambayo aliitaka kwa sababu alitaka kazi yoyote ambayo ingempa kipato. Alitumai kuwa mhudumu angempa nafasi ya kujieleza. Mhudumu aliona kuwa Kudra alimpotezea wakati. Bila kumpa muda zaidi, aliitoa taarifa kwa Kudra aliposema, **"Huna hakika dadangu ya kile ukisemacho."** Mhudumu alitaja maneno hayo waziwazi ili Kudra asimpotezee muda zaidi. Kulingana na maelezo ya MUtNR, mhudumu aliupitisha ujumbe wake bila kutilia maanani mahitaji ya uso wa Kudra. Baada ya hapo, aliifunga ofisi yake kama ishara ya kutotaka kusumbuliwa.

### 3.3 Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt)

Culpeper (1996), anaeleza kuwa Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt) ni mipango inayowekwa na msemaji ili aitumie katika harakati za kwenda kinyume na matarajio ya uso chanya wa msikilizaji. Kulingana na Brown na Levinson (1987), mzungumzaji mwenye uso chanya huwa na mahitaji kama vile kutaka kujumuishwa katika mambo, kusifiwa iwapo amefanya jambo nzuri au hata kutaka kuonyeshwa kuwa anathaminiwa. MCUt unakusudiwa kuvunja mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji kwa kuyapuuza waziwazi mahitaji hayo. Msemaji anaweza kumpuuza msikilizaji kwa kumtenga ili asihusiane naye katika jambo fulani. Katika mahusiano, msemaji anaweza kutumia kauli hasi zinazodhihirisha wazi kuwa anamchukia msikilizaji.

Njia mbalimbali zinachunguzwa katika harakati za kutambua MCUt. Njia hizi ni pamoja na msemaji kutoa kauli zenye matusi, kutafuta makabiliano na kumtenga msikilizaji.

### 3.3.1 Kutoa kauli zenye matusi

Matusi ni kauli chafu zinazotamkwa na mtu mwenye ghadhabu kwa msikilizaji ili kuiharibu sifa ya msikilizaji huyo. Lengo la msemaji ni kumvunjia msikilizaji heshima kupitia kumuudhi. Msikilizaji anapoelekezwa kauli zinazobeba matusi uso wake unatishika kwa sababu msemaji atakuwa ameenda kinyume na matarajio ya msikilizaji. Aghalabu, msikilizaji hatarajii kutolewa kauli za matusi ambazo zinatishia uso wake.

Katika *Pendo la Karaha*, njia ya matusi inajitokeza wazi kwamba Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt) inadhihirika. Kwa mfano katika mazungumzo kati ya Kidawa na Mwadime:

> **(16)** “Ni nini Jamani?” Jirani mmoja aliuliza huku akionyesha wasiwasi. “**Ni huyu bwana anajifanya msusi kumbe nyoka. Ni ziraili huyu …”** Kidawa alisema huku kipovu kikimtoka. “Wanaowasukuma watoto kwa dawa za kulevya ni hao matajiri wanaoziuza dawa. Ni hao viongozi wenu. Mnawachagua nyinyi wenyewe. Mnawafanya wabunge. Mnawafanya *madisii*, waona. **“Mwongo wewe, mwanaharamu,”** Kidawa alisema. “Mimi ningekuwa na uwezo nisingekuwa nashona mikeka basi. Ningekuwa ninakaa nyumba kama wao. Dadangu ningekuwa Nyali ama ningekuwa huko Bamburi, waona? **“Mshenzi, mchawi wewe. Mwanaharamu shika adabu …”** Kidawa alisema. (Uk.44)

Kutokana na mfano wa (16), Kidawa alikuwa ameghadhabika kiasi cha kumwelekezea Mwamba maneno machafu. Mwamba alishangaa kwa nini Kidawa alidhamiria kumtia aibu. Kulingana na MCUt, msemaji hutamka kauli hasi kwa msikilizaji ambazo zinaenda kinyume na mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji. Mwamba alitarajia kuwa Kidawa angemtambua kama jirani mwema ila Kidawa alisema, **“Ni huyu bwana anajifanya msusi kumbe nyoka. Ni ziraili huyu…”** Jirani yao aliyasikia makabiliano na kutoka nje kujionea. Kidawa alimtia Mwamba aibu mbele ya jirani huyo kwa kumfananisha Mwamba na nyoka. Kidawa aliukwaza uso chanya wa Mwamba alipotamka kuwa Mwamba alikuwa ziraili, anayeweza kuwaletea mabaya. Mwamba alijaribu kujitetea kuwa waliojishughulisha katika kuuza madawa ya kulevya ni viongozi ila Kidawa hakumpa nafasi. Isitoshe, Kidawa alimkatiza Mwamba usemi na kutamka, **“Mwongo wewe, mwanaharamu.”** Kulingana na nadharia ya upole, mzungumzaji mwenye uso chanya hutaka kushirikishwa katika kutoa uamuzi wa mambo. Kauli za Kidawa zilidhihirisha kuwa

alimshambulia Mwamba. Kidawa alifikia kiwango cha kuudhuru uso chanya wa Mwadime alipomtusi kuwa alizaliwa nje ya ndoa.

Vilevile, Mwamba alijaribu kumrejelea Kidawa kama dada ila Kidawa alizidi kumtenga huku akimtusi zaidi. Kidawa alitamka, **"Mshenzi, mchawi wewe. Mwanaharamu shika adabu …"** Ghadabu ilimchochea Kidawa kumtusi Mwamba tena. Kidawa alimwita Mwamba mtu asiyestaarabika na mwenye uwezo wa kuwaroga wengine. MCUt unadhihirika kupitia kwa Kidawa kumkosea Mwamba heshima alipomtusi, jambo ambalo liliuharibu uso chanya wa Mwamba kiasi cha kutaka kujitetea. Mwamba alimweleza Kidawa kuwa alidhihirisha tabia za mtu mwenye wazimu. Hivyo basi, Mwamba alimkomesha Kidawa kwa kumweleza kuwa angemfundisha adabu.

Vilevile mazungumzo kati ya Kudra na Hanawi yanadhihirisha njia ya matusi katika kuwasilisha MCUt kama ifuatavyo:

**(17)** **"You *slave*!"** Hanawi alimwambia Kudra siku moja alipoleta wali mbichi mezani. (uk. 135)

Kutokana na mfano wa (17), Salim alikuwa katika uhusiano wa kimapenzi na bintiye kwa jina Hanawi. Kudra alipojiunga nao, Salim alianza uhusiano wa kimapenzi naye, jambo ambalo lilimkasirisha Hanawi. Mara kwa mara, Hanawi alitafuta makabiliano na Kudra. Hanawi alikuwa na mazoea ya kumsonya na kumsemesha Kudra kwa ukali bila sababu yoyote. Katika makabiliano kati yao, Hanawi alienda kinyume na matamanio ya uso chanya wa Kudra. Hanawi alimrejelea Kudra kama mtumwa alipotamka kwa Kiingereza, **"You *slave*!"** Matusi ya Hanawi yalidhihirisha MCUt alipomrejelea Kudra kama mtu asiye na thamani. Kudra alijaribu kujitetea kwa upole kuwa yeye si mtumwa na hata kumrejelea Hanawi kama dada. Pamoja na hayo, Kudra alitamani kuthaminiwa na kukubaliwa kama mfanyikazi ila si kuchukuliwa kama mtumwa.

Katika hali nyingine, maneno ya Nayrat kwa Kudra yanaonyesha wazi matusi yanayochangiwa na tofauti ya kimamlaka na kudhihirsha MCUt kama ifuatavyo:

**(18)** **"Kelbu wewe,"** Bi. Nayrat alimwambia Kudra kila wakati alipokosea jambo dogo. (Uk.91)

Kutokana na mfano wa (18), Kudra alinyimwa kuingiliana na majirani wa Aminii na Nayrat bila ruhusa. Nayrat alipofahamu kuwa Kudra alikuwa ameanza kujuana na majirani, alimtesa. Bi Nayrat alianza kuwa mkali zaidi kwa Kudra huku akimsingizia makosa. Alimwamuru mara kwa

mara na kumpokeza matusi. Nayrat alizoea kumtusi Kudra kwa kusema, **“Kelbu wewe.”** kumaanisha kuwa alimwona Kudra kuwa na hadhi duni kama ya mbwa. MCUt unadhihirika kupitia kwa Nayrat kumdunisha Kudra, aliyetamani kuthaminiwa. Nayrat anamtishia Kudra uso wake chanya kwa kumwelekeza malalamishi na matusi kila wakati.

Vivyo hivyo, Nayrat anaonekana kupiga hatua katika kumtusi mwajiriwa wake Kudra. Hili linachangia katika kudhihirisha MCUt kama ifuatavyo:

> **(19)** **“Nenda ukalale wewe! *Lazy woman*!”** Nayrat **alimzomea Kudra** akimkodolea macho makali kama ya simba jike. (Uk.106)

Kutokana na mfano wa (19), ni wazi kuwa Nayrat alikuwa na mazoea ya kumtusi Kudra. Afya ya Kudra ilikuwa matatani. Kudra alifanyishwa kazi nyingi na Nyrat akiwa mgonjwa kiasi cha kulemewa kuendelea. Kudra alimjuza Nayrat kuhusiana na hali yake ila Nayrat hakumwonea huruma. Aidha, Nayrat anadhihirisha kukosa utu alipomtusi Kudra kwa kusema, **“Nenda ukalale wewe! *Lazy woman*!”** Matamanio ya Kudra yalikuwa kueleweka na kuthaminiwa. Nayrat alienda kinyume na uso chanya wa Kudra na kudhihirisha MCUt anapompuuza Kudra na kumhusisha na sifa ya uvivu. Vilevile, Nayrat alimwita Kudra *woman* kwa maana ya mwanamke, neno ambalo likitumiwa katika muktadha hasi kumrejelea msichana linazua maana yenye dharau.

Pamoja na hayo, mazungumzo kati ya Kassim na Lindo yanaonyesha kuwepo kwa matusi yanayochangia katika kudhihirisha MCUt kama ifuatavyo:

> **(20)** **“Mwanaharamu ni wewe ambaye mamako ananadi watoto wa watu ughaibuni kwa ajili ya ubinafsi,”** Lindo alisema. **“Nenda kauze unga, wewe fala,”** Kassim alimweleza Lindo na kuamsha hamaki zake. (Uk.46)

Kutokana na mfano wa (20), mgogoro kati ya Lindo na Kassim ulianza baada ya Lindo kufika kwa Mwamba na kuanza kutumia nguvu ili ashiriki kwenye mchezo wa bao. Kassim alimweleza Lindo kuwa zamu yake haikuwa imefika ila Lindo hakumsikiliza. Tabia ya Lindo ilimchochea Kassim kumwita mwanaharamu. Lindo alipandwa na ghadhabu na kumkabili Kassim kwa kusema, **“Mwanaharamu ni wewe ambaye mamako ananadi watoto wa watu ughaibuni kwa ajili ya ubinafsi.”** MCUt unadhihirika kupitia kwa Lindo kutoa kauli yenye tusi kwa Kassim ili kulipiza kisasi. Lindo alidhamiria kuuhasiri uso chanya wa Kassim kwa kuwa mama yake, Rehema alikuwa mbinafsi. Lindo na Kassim walitusiana kwa lengo la kuudhiana. Kila mmoja alimtambua

mwenzake kama mwanaharamu kwa sababu zake tofauti. Utani kati ya Lindo na Kassim ulizidi kiasi cha Kassim kumwingilia Lindo sana kwa tusi. Kassim alimwambia, **"Nenda kauze unga, wewe fala."** Kassim alimrejelea Lindo kuwa mjinga, kumaanisha kuwa alimdharau sana Lindo. Maneno ya Kassim yalimghadhabisha sana Lindo. Lindo na Kassim walitamkiana maneno yenye matusi yaliyoenda kinyume na matarajio ya nyuso zao chanya na hivyo basi kudhihisha kuwepo kwa MCUt.

### 3.3.2 Kutafuta makabiliano.

Kulingana na Culpeper (1996), njia ya kutafuta makabiliano inajumuisha msemaji kutafuta nafasi ya kutoelewana na msikilizaji ili waweze kukorofishana. Wasemaji aghalabu hujihusisha katika mgogoro mkali unaojumuisha maneno makali kutoka upande wa msikilizaji na ule wa msemaji. Katika *Pendo la Karaha,* njia ya makabiliano imedhihirika kati ya msemaji na msikilizaji katika kuendeleza MCUt kama ifuatavyo:

> **(21)** **"Siwezi kula chakula chako. Hujui kupika, tena wewe ni mchafu nenda koleji ufundishwe kupika,"** Hanawi alimweleza Kudra. **"Ukitaka kula, ni shauri lako. Hata ukaolewe! Utaozea kwenu sijui ukifanya nini, huwezi kuolewa na ..."** Kudra alijizuia kutamka jina hilo. (Uk.135)

Kutokana na mfano wa (21), Hanawi alitamani kupata upenyu wa kugombana na Kudra. Ilitokea kuwa wali ambao Kudra alikuwa amepika siku hiyo ulikuwa mbichi. Hanawi alisusia kula chakula cha Kudra na kusema, **"Siwezi kula chakula chako. Hujui kupika…"** Hanawi alidhamiria kuudhuru uso chanya wa Kudra kwa kuutaja udhaifu wa Kudra kuwa hakufahamu kupika. Hanawi alizidi kutafuta makabiliano kwa kutamka, **"…tena wewe ni mchafu nenda koleji ufundishwe kupika."** Kutokana na maneno ya Hanawi, tunafahamu ya kwamba Hanawi hakutilia maanani hisia Kudra. Alimweleza Kudra kuwa alikuwa mchafu na alikosa ujuzi wa kupika. Maneno ya Hanawi yalimghadhabisha Kudra aliyeshindwa kujizuia na kusema yaliyokuwa moyoni. Kudra alisema, **"Ukitaka kula, ni shauri lako…"** kudhihirisha kuwa alikuwa ameudhishwa na matamshi ya Hanawi. Kudra alizidi kutamka, **"…Hata ukaolewe! Utaozea kwenu..."** Kudra alitaka kumjuza Hanawi kuwa hakupaswa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na baba yake, Salim, ila alijizuia. Kudra alitamka kuwa Hanawi alihitaji kuolewa kwa sababu umri wake wa kuolewa ulikuwa umetimia na hakuonyesha dalili za kufanya hivyo. MCUt unadhihirika kupitia makabiliano makubwa yanayodhihirisha kuwa Hanawi alimkosea Kudra heshima. Mahitaji ya

Kudra yalikuwa kuheshimiwa na kuthaminiwa kama mwajiriwa. Hanawi aliuhasiri uso chanya wa Kudra kwa kutamka kauli za kumdunisha kila wakati.

Katika hali nyingine, ugomvi kati ya Hanawi na Kudra uligeuka na kuwa uhasama. Hanawi na Kudra walizidi kukabiliana bila woga kama ifuatavyo:

> **(22)** **"Hapa hutakaa upende usipende. Tena ukicheza nitakubinginya." "Nitakaa upende usipende."** Kudra alijibu kwa kiburi na ujeuri. **"Wewe umekuja huku kufanya kazi kisha unaleta hata ujeuri,"** Hanawi alimweleza Kudra. **"Ndiyo, nimekuja kufanya kazi, hiyo isiwe sababu ya kunidharau. Mimi ni mtu kama wewe hata kama naonekana tofauti." "Hiyo ndio sababu uliiba dhahabu na pesa ulikotoka ukaja kujificha hapa?"** Hanawi alimweleza Kudra. **"Uongo huo. Mzushi wewe…"** Kudra alisema. **"Kama si mali kwa nini unaparamia uhusiano wa mapenzi na baba?"** "Si kuparamia lolote. Aliyetaka ni babako, dadangu," Kudra alisema. **"Umeparamia, ukajifanya rahisi ndipo uvune katika mahusiano kuwili. Wewe ni mjanja kweli,"** Hanawi alimtupia Kudra kombora la matusi. (Uk.144- 145)

Kutokana na mfano wa (22), Hanawi na Kudra vilevile wanaendelea kukabiliana vikali. Katika makabiliano haya, Kudra na Hanawi wanatishiana nyuso chanya. Kudra alimtaka Hanawi amkubali jinsi alivyo ilhali Hanawi alimtenga alipotamka, **"Hapa hutakaa upende usipende…"** Hanawi alimtenga Kudra kwa kumweleza kuwa hangekubali aishi nao tena. Alimpa Kudra kitisho kwa kusema, **"…Tena ukicheza nitakubinginya."** Kudra anang'angana kujitetea kwa kusema, **"Nitakaa upende usipende."** Maneno haya yalisababisha makabiliano kwa sababu hakuna mmoja kati yao aliyetaka kushindwa. Kutengwa kwa Kudra na Hanawi kunadhihirisha kuwepo kwa MCUt kwa sababu Hanawi alienda kinyume na matarajio ya uso chanya wa Kudra.

Pamoja na hayo, Hanawi alizidi kumweleza Kudra kuwa alikuwa ameipita mipaka ya mwajiriwa aliposema, **"Wewe umekuja huku kufanya kazi kisha unaleta hata ujeuri."** Hanawi alimshambulia Kudra kwa kumgombeza na kulalamika kuwa Kudra alikuwa na ujeuri. Kudra alipoona kuwa makabiliano kati yake na Hanawi yalianza kupita mpaka, aliamua kujitetea kwa kusema, **"Ndiyo, nimekuja kufanya kazi, hiyo isiwe sababu ya kunidharau…"** Kudra alitamka kuwa hakufurahia namna ambavyo Hanawi alipendelea kumdharau. Kudra alimweleza Hanawi kuwa hata kama hadhi yake ilikuwa ya chini, alistahili kupewa heshima kwa kutamka, **"…Mimi**

**ni mtu kama wewe hata kama naonekana tofauti."** Kudra alielewa kuwa Hanawi alikuwa akimdharau kwa sababu ya hadhi yake duni. Hatimaye, Hanawi aliifichua siri ya Kudra kuwa alipokuwa akifanya kazi kwa Nayrat na Aminii, waajiri wake wa kwanza, aliwaibia na kutoroka. Hanawi alisema, **"Hiyo ndio sababu uliiba dhahabu na pesa ulikotoka ukaja kujificha hapa?"** Hanawi alimweleza Kudra kuwa angemshtaki iwapo angezidi kuhusiana kimapenzi na Salim. Kudra aliyakana madai ya Hanawi kwa kusema, **"Uongo huo. Mzushi wewe…"** Kudra alizidi kudanganya kuwa hakuwahi kuhusika na tendo la wizi katika juhudi za kujitetea. Alifahamu kuwa iwapo angekubali, mambo yangekuwa mabaya zaidi.

Makabiliano ya Hanawi kwa Kudra hayakukoma kwani Hanawi alizidi kutoa kauli zilizochochea makabiliano kuchacha. Hanawi alisema, **"Kama si mali kwa nini unaparamia uhusiano wa mapenzi na baba?**" Hanawi aliamua kumkabili Kudra kuhusiana na uhusiano wake na baba yake. Kudra alijitetea kwa kusema kuwa ni Salim aliyekuwa amemshawishi. Hanawi alidhihirisha MCUt na kumsingizia Kudra madai ya uongo aliposema, **"Umeparamia, ukajifanya rahisi ndipo uvune katika mahusiano kuwili. Wewe ni mjanja kweli."** Hanawi alitafuta makabiliano kwa kumshutumu Kudra kuwa aliingilia maisha yao. Hanawi alimlaumu Kudra kuwa alitumia ujanja huku akimhusisha na sifa ya ubinafsi. Maneno ya Hanawi yalimkasirisha Kudra. Matarajio ya uso chanya wa Kudra yaliyokuwa yamekiukwa. MCUt unadhihirika kupitia dharau na malalamishi kutoka kwa Hanawi badala ya kujumuishwa na kuheshimiwa.

### 3.3.3 Kumtenga msikilizaji

Kulingana na Brown na Levinson (1987), ili mawasiliano yawe ya kufana, ni sharti kuwe na ushirikiano kati ya msemaji na msikiizaji.  Mikakati Chanya wa Upole (MCU) itakiukwa iwapo msemaji atamtenga msikilizaji kimazungumzo. Mkakati huu unapokiukwa, utoupole huzuka. Msemaji anapomtenga msikilizaji anamfanya msikilizaji kuhisi kuwa hajathaminiwa. Kujitenga kwa msemaji na wengine katika mazungumzo kunadhihirisha kuwa hataki kwa njia yoyote kuhusika na msikilizaji. Msemaji hataki kuwa na uhusiano na msikilizaji; ilhali msikilizaji anataka ajumuishwe. Uhusiano kati ya msemaji na msikilizaji unavunjika iwapo msemaji anakosa kutenga muda wa kuzungumza na msikilizaji.

Katika *Pendo la Karaha,* MCUt inadhihirika kupitia kauli ya Riziki anapomtenga Kidawa katika mazungumzo kama ifuatavyo:

**(23)** **“Karibu, Herdaa aaa pole Rachael. Jamani hmmm Kidawa!”** Kidawa alipigwa na butwaa jinsi jina lake lilivyofutika katika kumbukizi za mwenzake. “Itakuwaje hivyo?” Kidawa alijiuliza huku akifanya bidii kumwambia mwenzake “Ahsante Riziki,” Kidawa alijibu kwa kuchanganyikiwa kwingi. Alichapuka na kuondoka. (Uk.141-142)

Kutokana na mfano wa (23), Kidawa alikuwa amejitolea kumtembelea rafiki yake wa awali aliyekuwa amehamia kwenye mtaa wa kifahari kwa jina *New Horizon.* Riziki na Kidawa walikuwa marafiki kwa miaka mingi, takriban thelathini. Riziki alihama na kumsahau Kidawa baada ya kukutana na marafiki wapya. Kidawa alipofika kwa Riziki alimkaribishwa ila walipoamkuana, Riziki alijaribu kulikumbuka jina la mgeni wake bila mafanikio. Riziki alitamka, **“Karibu, Herdaa aaa pole Rachael. Jamani hmmm Kidawa!”** Kidawa alishindwa kuamini kuwa rafikiye wa miaka mingi alikuwa amemsahau. MCUt unajitokeza kupitia kwa Riziki kumtenga Kidawa kwenye maisha yake. Uso chanya wa Kidawa ulitishika kwa sababu aliona kuwa Riziki hakuuthamini urafiki wao. Kidawa anaonekana kuathiriwa na kutengwa huku baada ya kufahamu kuwa Riziki aliwathamini sana marafiki wake wapya. Riziki hakuwa na hakika jina la mgeni wake na kubahatisha kuanzia Herdaa hadi Rachael. Hatimaye alilikumbuka jina la Kidawa. Uso chanya wa Kidawa ulikuwa umepokea madhara kwa sababu alipuuzwa na hivyo kudhihirisha MCUt.

Kadhalika, njia ya kumtenga msikilizaji inajitokeza kupitia kwa Riziki katika kudhihirisha MCUt kama ifuatavyo:

**(24)** “Habari za siku nyinyi?” Kidawa alimwuliza Riziki. **“Sawa,”** Riziki alisema huku akienda kujibu simu ya mjenzi aliyekuwa akimjengea nyumba za kukodisha huko Kisauni. **“*Ok,”*** Riziki alisema. “Yaah. Lakini usinunue saruji nyingine, ununue ya ‘Bamburi’ kwa sasa. ***Ok*…yaaa*, ok* sawa,”** Riziki alisema. (Uk.142)

Kulingana na kauli katika mfano wa (24), Kidawa alikuwa amemtembelea Riziki kwa mara ya pili. Wakati wote, Riziki alionekana kuiweka makini kwenye simu badala ya kuzungumza na mgeni wake. Riziki na Kidawa hawakuwa wameonana kwa muda. Kidawa alipomuuliza Riziki kuhusiana na hali yake, Riziki alimjibu kwa neno moja tu, **“Sawa.”** Riziki alimtenga Kidawa na kuendelea na mazungumzo yake na wajenzi kwenye simu alipokuwa akiwaeleza kuhusu saruji aliyodhamiria kununua. MCUt unajitokeza kupitia kwa Riziki kuipuuza haja ya Kidawa ya kutaka kujumuishwa. Mahitaji ya uso chanya wa Kidawa yanapuuzwa kwa sababu Riziki alimtenga

waziwazi. Riziki alichanganya maneno ya Kiingereza na viziada lugha aliposema, ***Ok*…yaaa, *ok* sawa.”** Wakati huu wote, Kidawa alikuwa akimsikiliza na kuhisi kuwa Riziki alimtenga. Riziki angetafuta muda baada ya kuzungumza na Kidawa kuwasiliana na mjenzi. Katika kudhihirisha MCUt, Riziki alidhamiria kumwonyesha Kidawa kuwa alikuwa na shughuli nyingi zisizomhusu yeye. Hii haikuwa mara ya kwanza kwa Kidawa kutaka kuzungumza na Riziki naye Riziki kujishughulisha kwa kuzungumza kwenye simu.

Vivyo hivyo, mazungumzo kati ya Kassim na Rehema yanaonyesha Kassim akimtenga Rehema na kudhihirisha MCUt kama ifuatavyo:

> **(25)** “Mwanangu, ni mimi Rehema mamako,” Rehema alisema huku pumzi zikimtoka. **“Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi? Mama yangu yuko Ujerumani,**” Kassim alisema. “Nisikilize tu, sikukatizi kunywa wala kufanya lolote la utashi wako. Lakini rudi nyumbani.” Rehema alimrai Kassim aliyetokwa na ute mdomoni. **“Nyumbani sirudi…”** Kassim alisema akitia tembe fulani nyeupe kinywani. (Uk.80)

Kutokana na mfano wa (25), Kassim alikuwa ametoroka nyumbani. Kassim hakutaka kuhusiana na mama yake kwa sababu hakupenda namna Rehema alivyoiendesha biashara ya kuwapeleka wasichana ughaibuni. Rehema alikuwa akimhitaji Kassim na baada ya muda alimtafuta. Mahitaji ya uso chanya wa Rehema ya kuthaminiwa na mwanaye tena hawakutimizwa kwa sababu Kassim aliyapuuza. MCUt unadhihirika wakati ambao Kassim hakutaka kuhusishwa na Rehema tena. Rehema alijaribu kujieleza ila Kassim alimuuliza, **“Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi? Mama yangu yuko Ujerumani,**” kudhihirisha kuwa alikuwa amemtenga kabisa mama yake. Rehema alimtaka Kassim amsikilize na arudi nyumbani ila Kassim alikataa kwa kutamka, **“Nyumbani sirudi …”** Kassim alijitenga na familia yake. Hakutaka kuhusishwa na utajiri wa Rehema aliojitafutia kutokana na kuwalaghai wasichana. Kupitia kauli ya Kassim, MCUt unadhihirika kwa sababu Rehema alitaka kukubaliwa na ila Kassim alimpuuza na kuchelea kumpa kumsamehe.

### 3.4 Mikakati ya Kuuzuia Upole (MKU)

Kulingana na Culpeper (1996), Mikakati ya Kuuzuia Upole (MKU) ni hali za kutokuwepo kwa upole katika muktadha ambao upole unatarajiwa. Brown na Levinson (1987:5) wanaeleza kuwa wazungumzaji wanapaswa kudhihirishiana upole katika mazungumzo na wasipofanya hivyo,

inachukuliwa kuwa wanaukosa mwelekeo wa kuwa wapole. Kwa ujumla, MKU ni mipango iliyoundwa na msemaji ambapo upole unaotarajiwa katika mazungumzo hautekelezwi katika miktadha fulani. Msemaji anaweza kukosa mwenendo mzuri anapohusiana na wengine wakati wa mazungumzo.

Culpeper (1996:357) anaeleza kuwa kukosa kushukuru baada ya kupewa zawadi ni njia mojawapo ya kutambua MKU. Katika *Pendo la Karaha*, tutachunguza njia ya kujizuia kujibu salamu, kujizuia kusalimu, kama njia zinazoweza kudhihirisha kuwa msemaji anajizuia kutekeleza upole wakati ambao anastahili kuonyesha upole.

### 3.4.1 Kujizuia kujibu salamu

Kulingana na Culpeper (1996), iwapo msikilizaji atasalimiwa na badala yake kujifanya kuwa hajasikia salamu hizo, atakuwa amedhihirisha MKU.

Mazungumzo kati ya Riziki na Kudra yanadhihirisha kuwa Riziki anajizuia kujibu salamu alizopokezwa na bintiye kama ifuatavyo:

> **(26)** "Habari za jioni mama?" Kudra alijaribu kumwamkia mamake kwa sauti babaifu ila **alizabwa kofi** (Uk.26)

Kutokana na mfano wa (26), Kudra ametoka nyumbani bila kumjuza Riziki, mama yake. Kudra aliporudi nyumbani, alimpata Riziki akimsubiri. Baada ya kumwamkua, Riziki hakumjibu. Kitendo cha Riziki cha kunyamaza baada ya kupokezwa salamu na bintiye kinadhihirisha MKU. Riziki alimzaba Kudra kofi kali kiasi cha kumtia uziwi badala ya kuijibu salamu. Riziki alitamka kuwa angepambana naye kwa njia zote kuundoa ujeuri baada ya kumzaba Kudra. Maneno ya Riziki yanadhihirisha kuwa alikuwa amepokea salamu za Kudra ila akachagua kuzipuuza. Riziki aliwasilisha kuwa hangelegeza kamba kwani alipania kuirekebisha tabia ya Kudra.

### 3.4.2 Kujizuia kusalimu

Hali ya kujizuia kusalimu inajumuisha mtu kujizuia kumwamkua mwenzake ilhali anafahamu kuwa anawajibu wa kufanya hivyo. Kutokana na maelezo ya mwandishi, Subira alijizuia kumsalimu Rehema baada ya kifo cha bintiye Rukia kama ifuatavyo:

> **(27)** Hadi leo, kilio cha **Subira hakijazimika**. **Mara chache, hupita hapo kwa Rehema. Hakutaka kumwamkia Rehema**. Aliona Rehema kama mwizi mwingine, hana roho ya utu. Alijali nafsi yake tu. (Uk.140).

Kutokana na mfano wa (27), Subira alikuwa bado anaumwa kwa kumpoteza bintiye aliyepelekwa ughaibuni na Rehema kuzumbua riziki. Baada ya kifo cha Rukia, chuki ya Subira kwa Rehema ilianza. Kadri muda ulivyosonga na chuki ya Subira kwa Rehema ilizidi kuongezeka. Subira alipopita kwa Rehema, hakutaka kumwamkua kwani alimwona kama mbinafsi, mwizi na mwanamke aliyepoteza utu. Kupitia kwa Subira, mkakati wa kuuzuia upole unadhihirika kupitia ugumu anaoupata wa kumsalimu Rehema.

### 3.4.3 Kujizuia kusamahe

Katika mazungumzo, kujizuia kusamehe kunahusu mshirika katika mazungumzo kuombwa msamaha na badala ya kukubali ombi hilo, anakataa. Mshirika huyo atakuwa amejizuia kutekeleza upole na maneno yake yatadhihirisha kuwepo kwa MKU.

Katika *Pendo la Karaha,* Kassim anaonekana kujizuia kutekeleza upole katika mazungumzo yake na Rehema, kama ifuatavyo:

> **(28)** "Mwanangu, mwanangu," Rehema ni kama alitaka kumpigia magoti mwanawe. "Nisamehe Mwwaaaa…" Rehema pumzi zilimwisha. **"Nikusamehe nini? Jisamehe mwenyewe kwanza…"** (Uk.80)

Kutokana na mfano wa (28), Rehema alikuwa amemtafuta mwanawe na baada ya kumpata, alimtaka Kassim arudi nyumbani. Kassim hakutaka kurudi nyumbani kwa sababu hakufurahia namna Rehema alivyokuwa akiiendesha biashara yake. Rehema alijaribu kumwonyesha mwanawe kuwa alikuwa amebadlika ila Kassim hakumwamini. MKU unadhihirika wakati ambao Rehema alimwomba mwanawe msamaha ila Kassim hakutaka kumsikiliza. Kassim alijizuia kusamehe kwa kutamka, **"Nikusamehe nini? Jisamehe mwenyewe kwanza…"** Kassim alichelea kumsamehe mama yake kwa sababu aliona kuwa Rehema alikuwa akijifanya kuwa amebadilika. Kassim alimweleza Rehema kuwa alihitaji kujisamehe mwenyewe. Rehema alikuwa na moyo wa kumwonyesha Kassim upole kwa kutaka amsamehe ila Kassim hakuwa tayari kusamehe. Kassim aliweka sharti la kusamehe kuwa Rehema alihitaji kudhihirisha utu na kubadili mienendo yake.

## 3.5 Mikakati ya Utoupole yenye Dhihaka (MUtD)

Kulingana na Culpeper (1996), kudhihaki ni njia ya kumwelekezea msikilizaji maneno yanayoonyesha wazi kuwa msemaji anamdharau. Mikakati hii inajumuisha msemaji kutumia mikakati ya kudhihirisha upole ila hadhamirii kufanya hivyo. Msemaji anaweza akadhihirisha hayo kwa kutumia kinaya kwani mikakati ya upole anayoitumia haina ukweli ndani yake. Msemaji

anayawasilisha maneno kwa njia inayodhihirisha upole ila msikilizaji akiyawazia anatambua kuwa amedhihakiwa. Mikakati ya Utoupole yenye Dhihaka (MUtD) ni mikakati inaoonyesha shambulio la uso wa msikilizaji linalojumuisha kutumia mikakati ya upole bandia, kama njia ya kuwasilisha utoupole. MUtD inaukaribu na kinaya kama alivyoeleza Leech (1983:82) kwamba ikiwa msemaji kwa njia moja au nyingine atamkasirisha msikilizaji, anapaswa kufanya hivyo kwa namna fiche. Kwa kufanya hivyo, msikilizaji ataelewa ujumbe wa msemaji unaoleta machukizo kupitia njia fiche.

Katika *Pendo La Karaha,* dhihaka inadhihirisha katika mazungumzo na mahusiano ya wahusika ili kuitambulisha MUtD. Kwa mfano:

> **(29)** "Si kwa ubaya," Kudra alijitetea walipokumbana na Saumu. **"Ni kwa nini?"** Saumu alimwuliza. "Nilitaka kuuliza habari za mamangu. Niliskia alipiga simu akinitafuta," Kudra alijibu akitathmini athari ya maneno yake kwa Saumu. **"Wewe unadhani mama yako ni bora kuliko mama zetu?"** Saumu alimwuliza Kudra huku **akimtemea mate usoni na kumfurusha ofisini.** (Uk.167)

Kutokana na mfano wa (29), Kudra alikuwa akitafuta namna ya kuwasiliana na ubalozi wa Kenya huko Dubai. Aliwauliza wasichana wenzake wamwelekeze ila hakufaulu kwani wote hawakuwa na nambari ya simu ya ubalozi huo. Saumu alitaka kujua ni kwa nini Kudra alihitaji nambari hiyo ya simu. Kudra alimweleza Saumu kuwa hakuwa na nia mbaya ya kuitafuta nambari ya ubalozi. Saumu alimuuliza Kudra, **"Ni kwa nini?"** baada ya Kudra kumficha sababu hiyo. Kudra ili aepuke makabiliano na Saumu alimdanganya kuwa alitaka kufahamu habari za mama yake. Jibu la Kudra halikumridhisha Saumu kwani alianza kumbeza kwa kusema, **"Wewe unadhani mama yako ni bora kuliko mama zetu?"** Maneno ya Saumu yanafasiriwa kuwa yanamshambulia Kudra kwa njia ya kibinafsi. Kudra hakutaka makabiliano na Saumu hivyo alinyamaza. Saumu alimfurusha Kudra ofisini na kumtemea mate kwenye uso. Kudra alitaka uhuru wa kufanya chochote alichokitaka ila Saumu alitafuta namna ya kumdharau.

Pamoja na hayo, mazungumzo kati ya Nayrat na Kudra, yanadhihirisha mkakati wa utoupole wenye dhihaka kama ifuatavyo:

> **(30)** "Mama yangu ni mgonjwa," Kudra alimweleza Nayrat aliyekuwa akijitanda hijabu ili aondoke. **"Acha tutafikiria,"** Nayrat alimweleza Kudra kwa **kumkata kauli**. "Ninasikia hawezi kupika. Anasaidiwa na jirani," Kudra alisema. **"Ngoja nitasema na mzee kisha nitakuelezea la**

> **kufanya,"** Nayrat aliyeonyesha **hakujali kitu** alimwambia Kudra. (Uk.114-115)

Kutokana na mfano wa (30), Kudra alikuwa amepokea habari kuwa mama yake alikuwa mgonjwa. Aliamua kuzungumza na waajiri wake ili wampe nafasi arudi nyumbani kumuuguza Riziki, mama yake. Baada ya kumweleza Nayrat kuhusiana na hali ya mama yake, hakuonekana kujali yaliyomkabili Kudra. Bila kujali, Nayrat alimkata, **"Acha tutafikiria."** Maneno ya Nayrat kijuujuu yanaonekana kuwa yenye upole ila anayatumia kumfumba Kudra macho asiulize mengi. Awali, walikuwa wamemkata mshahara kwa tuhuma za kumlipa wakala Rehema. Kudra hakuwa na uwezo wa kumsaidia mama yake. Alizidi kumpa Nayrat habari zaidi kuhusiana na hali dhaifu ya mamake ila Nayrat alisema, **"Ngoja nitasema na mzee kisha nitakuelezea la kufanya."** Nayrat anatumia ahadi kuwa atazungumza na Aminii ila hafanyi hivyo. Nayrat alifahamu kuwa Kudra alikuwa na jukumu la kuyaboresha maisha ya mama yake. Kwa dhihaka, Nayrat aliyapuuza mahitaji ya Kudra ya kumlipa mshahara wake ili aweze kumtumia Riziki kwa matibabu. Tabia ya Nayrat ya kumdanganya Kudra mara kwa mara inadhihirisha kuwa alipuuza kanuni ya kuonyesha huruma iliyopendekezwa na Leech (1983). Nayrat hakuonyesha hisia zozote za kumwonea Kudra huruma. Alisema kwa haraka kuwa angezungumza na Aminii kisha wampe mwelekeo zaidi. Upole anaodhihirishwa Nayrat ni upole uliojaa unafiki kwani hatimaye hawakumsaidia. Ilimbidi Kudra atafute ajira kwa Salim.

Katika hali nyingine, mazungumzo kati ya Kudra na Saumu yanadhihirisha kuwepo kwa MUtD kupitia maneno ya Saumu kama ifuatavyo:

> **(31)** "Hii kazi siitaki. Nipe pasi yangu." **"Pasi hupati na hapa huondoki ng'o!"** Saumu alimjibu Kudra. "Kazi mtu hufanya kwa hiari, mbona umekuja huku Dubai kututendea hivi?" **"Usinilaumu mimi kwanza mlaumu aliyekuleta dubai na umasikini wako. Mimi sikuja kukutafuta. Umewahi kumwona mtoto wa waziri mkuu huku? Kwa hivyo usiniletee ukali…"** Saumu aliyeonekana kwa mara ya kwanza ametishika alisema. (Uk.171)

Kutokana na mfano wa (31), mgogoro kati ya Saumu na Kudra unadhihirika. Kudra alikuwa amechoshwa na vitendo vya Saumu. Aliamua kuwa hapo *Parlour* hapamweki tena baada ya Saumu kumlazimisha kwenda nyumbani kwa Ali kushirikishana naye kimapenzi. Baada ya Ali kujitimizia haja, alimpeana Kudra kwa mwanaume mwingine. Kudra alichukua hatua ya kumkabili Saumu kuhusiana na hitaji lake la kutaka kuacha kufanya kazi kwenye *Parlour*. Kudra

alimwelezea Saumu kuwa aliitaka pasi yake ila Saumu akasema, **"Pasi hupati na hapa huondoki ng'o!"** Saumu alimdharau Kudra kiasi cha kumlazimisha Kudra kujishirikisha na ukahaba. Kutokana na maneno ya Saumu, tunapata kuwa Saumu alimchukulia Kudra kama mtumwa. Alikataa kumpa Kudra pasi yake kwa sababu alifahamu Kudra angekuwa huru kutafuta ajira kwingine. Baada ya makabiliano, Saumu alianza kutumia mkakati unaodhihirisha dhihaka kwa kusema, **"Usinilaumu mimi kwanza mlaumu aliyekuleta dubai na umasikini wako…"** Saumu anamdharau Kudra kwa umaskini wake. Saumu alitumia upole wenye dhihaka kwa kusema kuwa hakuwa na hatia ya kulaumiwa. Alizidi kumdhihaki Kudra kwa kutamka, **"…Mimi sikuja kukutafuta."** Saumu alitamka maneno hayo kwa bezo ili kumdhihirishia Kudra kuwa alijiweka katika hali hiyo mwenyewe.

Japo kuwa Saumu alikuwa akijitetea, alitumia dhihaka kuwasilisha utoupole anapotamka, **"Umewahi kumwona mtoto wa waziri mkuu huku? Kwa hivyo usiniletee ukali."** Masihara ya Saumu yalimkasirisha sana Kudra. Japo kuwa aliyoyasema Saumu yalikuwa ya kweli na kwa namna yenye upole, kinaya ni kuwa aliyatumia maneno hayo kumcheka Kudra na wenzake. Saumu alionyesha kumcheka Kudra, mwana wa maskini, aliyelalamikia kazi duni ilhali hakuwa na elimu ya kumpa kazi nzuri kama watoto wa matajiri.

Vilevile, maneno ya Rehema kwa Riziki yanadhihirisha kuwepo kwa dhihaka inayochangia kuwasilisha MUtD kama ifuatavyo:

> **(32)** "**Mwanao alienda kwa hiari yake, dadangu. Pia akiona si kuzuri, ana miguu na macho. Anaweza kurudi. Kama unachomwa na hasira nenda polisi. Nenda unishtaki".** (Uk.169-170)

Kutokana na mfano wa (32), Riziki alikuwa ameipokea simu kuwa Kudra alikuwa akisubiri kusafiri. Habari hiyo ilimpa furaha na huzuni alipokumbuka mateso ya mwanawe. Riziki alijaribu kujizuia kumkabili Rehema ila hasira aliyokuwa nayo ilimchochea kufika kwa Rehema. Riziki alikuwa na kovu lililosababishwa na Rehema kumpeleka bintiye ughaibuni kwa ajira ya utumwa. Hatimaye, Riziki alifika kwa Rehema kumkabili. Riziki alitaka kujua habari za Kudra, binti yake. Rehema naye alijifanya kuwa hakumfahamu Kudra. Hatimaye, Rehema alitamka, "**Mwanao alienda kwa hiari yake, dadangu…"** Rehema alimrejelea Riziki kama dada ila tunafahamu kuwa hawakuwa marafiki. Rehema anatumia jina hilo kama njia ya kumdhihaki Riziki. Rehema alimkumbusha Riziki kuwa Kudra alikuwa amejichagulia kwenda kutafuta ajira ughaibuni

alipotamka, **"…Pia akiona si kuzuri, ana miguu na macho. Anaweza kurudi."** Kupitia kwa kauli ya Rehema, tunapata kuwa anamdhikaki Riziki kwa kumweleza kuwa Kudra alikuwa huru kurudi nyumbani. Ukweli ni kwamba wote walifahamu kuwa kazi aliyoifanya Kudra ughaibuni ilikuwa ya utumwa. Kudra hangeweza kurudi nyumbani kwa sababu waajiri wote waliagiza kuiweka pasi yake ya usafiri.

Rehema anazidi kumdhihaki Riziki kwa kutamka, **"…Kama unachomwa na hasira nenda polisi. Nenda unishtaki."** Rehema anajitolea kumpa Riziki maoni kuwa alikuwa huru kumshtaki. MUtD unadhihirika kupitia Rehema kumwelekeza Riziki kwenda polisi kumshtaki ila Riziki alifahamu kuwa hakuna hatua yoyote ambayo polisi wangemchukua. Rehema alikuwa tayari amewahonga wamfumbie jicho na aiendeleze biashara yake. Safari ya Riziki kwenda kwa Rehema kumkabili haikuzaa matunda kwa sababu dhihaka za Rehema ziliishia kumuudhi zaidi.

Kadhalika, mazungumzo kati ya Lindo na Kassim yamesheheni dhihaka inayochangia kudhihirisha kuwepo kwa MUtD, kama ifuatavyo:

> **(33)** **"Usiniletee ulevi wako wewe Lindo,"** Kassim alisema. **"Ulevi? Ni wewe unayenipa pesa za kulewa…Eeh?"** Lindo aliuliza kwa hamaki. **"Lindo, wewe ni wazimu. Rudi usome uwe daktari,"** Kassim alimweleza Lindo huku akimwonya. (Uk.45)

Katika mfano wa (33), Lindo alifika kwa Mwamba na wakati huo, mchezo wa bao ulikuwa ukiendelea. Lindo alitaka kuanza kucheza ila Kassim hakumkubalia kwa sababu hakuwa amefika mapema. Lindo hakufurahia maneno ya Kassim kwa sababu aliona kuwa Kassim alikuwa na mazoea ya kumdhulumu. Kassim alimwona Lindo kama mlevi kwa kumweleza, **"Usiniletee ulevi wako wewe Lindo."** Makabiliano yalianza wakati huo. Lindo alimjibiza Kassim kwa kumuuliza, **"Ulevi? Ni wewe unayenipa pesa za kulewa…Eeh?"** Lindo aliliuliza swali hilo kwa mzaha kwani Kassim hakuwa na hela za kutosha kiasi cha kumpa Lindo ananulie vileo. MUtD unadhihirika kwa sababu kutokana na mzaha wa Lindo, Kassim alikasirika. Hamaki ya Kassim kutokana na dhihaka ya Lindo ilimsababisha kumtajia Lindo maneno hasi. Kassim alimdhihaki Lindo vilevile kwa kumwambia, **"Lindo, wewe ni wazimu. Rudi usome uwe daktari."** Kassim alidhihirisha dhihaka kwa kumkejeli Lindo kwani alifahamu kuwa hangepata nafasi ya kurudi shule. Kutokana na dhihaka ya Kassim na Lindo, mgogoro mkubwa ulizuka baina yao.

**HITIMISHO**

Sura hii imejikita katika kuchunguza kuwepo kwa utoupole katika *Pendo la Karaha.* Uchanganuzi wa kauli zinazodhihirisha utoupole umefanywa kulingana na mikakati ya utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996). Uchanganuzi huu ulichunguzwa kwenye mikakati ifuatayo: Mikakati Hasi ya Utoupole (MHUt), Mikakati ya Utoupole Ndani ya Rekodi (MUtNR), Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt), Mkakati wa Kuuzuia Upole (MKU) na Mikakati ya Utoupole yenye Dhihaka (MUtD). Kutegemea mifano ya kauli zinazodhihirisha utoupole katika sura hii, imebainika kuwa mikakati yote mitano ya utoupole imedhihirika kikamilifu.

Vivyo hivyo, imebainika kuwa MCUt ndiyo mikakati ilipendelewa na wahusika katika kuwasilisha utoupole. Mikakati hii imedhihirika kupitia kauli za wahusika zilizoonyesha kuelekezana matusi, kutafuta makabiliano na msemaji kumtenga msikilizaji waziwazi. MUtNR ilitumiwa haswa na wahusika waliowazidi wenzao umri kama njia ya kuadilisha, kama ilivyo kati ya Lindo na mamaye Kidawa na kati ya Kudra na mamaye Riziki.

## SURA YA NNE

## MATENDO YANAYOATHIRI NYUSO ZA WAHUSIKA KATIKA MAZUNGUMZO KATIKA *PENDO LA KARAHA*

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inachunguza matendo mbalimbali yanayochangia kuathirika kwa nyuso za wazungumzaji. Katika kuyaainisha matendo haya, tutaongozwa na mawazo yaliyopendekezwa na Brown na Levinson (1987). Tunayachunguza matendo haya ili kubainisha namna yanavyochochea kuathirika kwa nyuso za wahusika mbalimbali katika *Pendo la Karaha.* Baada ya kutambua kila kitendo, tunaangazia athari zinazoachwa kwenye uso wa msikilizaji kutokana na vitendo pamoja na kauli za msemaji. Matendo haya yanaegemezwa sifa za nyuso mbalimbali za wahusika ili kupata athari zinazozuka.

Brown na Levinson (1987) waliiendeleza dhana ya uso kutoka kwa Goffman (1967). Kulingana na Goffman, uso ni matamanio aliyonayo mtu wakati wa kuwasiliana na wengine. Wakati wote, mtu huyo huhakikisha kuwa matamanio hayo yametimizwa. Sifa za uso zinadhihirika kupitia mahusiano kati ya msemaji na msikilizaji. Katika mazungumzo, hisia za wazungumzaji zinaweza kupotea, kuimarishwa au kuboreshwa. Hisia zikiwa nzuri, uso unaimarika. Fedheha inasababisha uso kupotea. Brown na Levinson (KHJ) waliendeleza dhana ya Goffman kwa kuugawa katika sehemu mbili; uso hasi na uso chanya.

### 4.1 Uso Chanya

Kulingana na Brown na Levinson (1987), uso chanya unajumuisha mzungumzaji kutaka kuonekana anafaa mbele ya wengine. Mshiriki katika mazungumzo anatamani kutambuliwa na mwenzake, kujumuishwa katika mambo na kusifiwa iwapo amefanya jambo nzuri. Mzungumzaji anatamani kuonyeshwa upendo na uwezo wake wa kufanya jambo uheshimiwe. Katika mazungumzo, kutiwa aibu mbele ya wengine kunamsababishia msikilizaji fedheha. Katika kujiondolea uwezekano wa kutiwa aibu, mzungumzaji anatia bidii ili wengine waweza kumpongeza. Msemaji akitambuliwa na wengine anaridhika na uso wake chanya unaimarika. Aghalabu, msemaji hutaka mahitaji yake yaridhiwe na kushughulikiwa na wengine.

## 4.2 Uso Hasi

Brown na Levinson (1987) wanasisitiza kuwa uso hasi unadai uhuru wake. Mshiriki katika mazungumzo anapendelea kuachwa huru, yaani bila udhibiti wowote, kufanya uamuzi kuhusu mambo anayotaka. Aghalabu, mzungumzaji anatamani kuilinda faragha yake. Msemaji mwenye uso hasi hapendelei kusumbuliwa kwa njia yoyote ile. Iwapo pana jambo linalohitajika kushughulikiwa, mzungumzaji hatamani kushirikishwa kwa kuulizwa, kushauriwa au hata kuelezwa mambo. Isitoshe, kilicho muhimu kwa mzungumzaji mwenye uso hasi ni anachohitaji kutoka kwa wengine kama vile kuthibitishiwa mambo, kueleweka, kukubaliwa au hata kupendwa.

## 4.3 Vitisho vya uso

Brown na Levinson (KHJ) waliainisha vitisho vya uso kutegemea vitendo mbalimbali vinavyoweza kuutisha uso wa msikilizaji na ule wa msemaji. Vitisho vya uso vinadhihirika kupitia vitendo mbalimbali kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji. Aidha, kuna vitendo vinavyoweza kuathiri nyuso zote za wazungumzaji ni kama vile; kulalamikiwa, kutishwa na kusumbuliwa kila wakati. Mzungumzaji anapoelekezwa dharau na matusi hujihisi vibaya. Vilevile, udaku wa msemaji unaweza kuutisha uso chanya na uso hasi wa msikilizaji. Katika mazungumzo, hisia za msemaji zikiwa kali kiasi cha kuzua woga au aibu zinaweza kuhasiri uso wa msikilizaji. Vivyo hivyo, wasemaji wakikatizana usemi kwa njia inayodhihirisha wazi machukizo wanaweza kuharibiana nyuso zao. Culpeper (1996) alidokeza kuwa katika kuuhasiri uso, msemaji anafanya mpango kimaksudi ili atekeleze kitendo kinachovuruga matamanio ya uso wa msikilizaji.

## 4.4 Matendo yanayodhamiriwa kutisha nyuso hasi za wahusika katika mawasiliano katika *Pendo la Karaha*

Kulingana na Brown na Levinson (1987), matendo yanayodhamiriwa kuutisha uso hasi yanalenga kumwathiri msikilizaji kupitia kuudhuru uso wake. Katika kuchunguza namna nyuso hasi za wazungumzaji zinavyoathirika katika *Pendo la Karaha*, tutajikita kwenye migao mitatu kwa mujibu wa Brown na Levinson (KHJ). Migao hii ni: matendo yanayoarifu kuhusu kitendo hasi kijacho, matendo yanayoarifu kitendo chanya kinachotarajiwa kuwepo na matendo yanayoarifu matamanio ya msemaji kwa msikilizaji.

### 4.4.1 Matendo yanayoarifu kuhusu kitendo hasi kijacho.

Brown na Levinson (KHJ) wanaeleza kuwa msikilizaji anakabiliwa na shinikizo la kutenda jambo fulani. Shinikizo hili linatokana na sababu ya msemaji kumweleza msikilizaji waziwazi kuwa anamhitaji atekeleze jambo fulani. Mtendo yanayojitokeza katika *Pendo la Karaha* yanayodhihirisha msemaji kumwarifu msikilizaji kuhusi vitendo hasi vijavyo ni pamoja na kutolewa amri, kukumbushwa mambo na kutisha.

#### 4.4.1.1 Amri

Kulingana na Brown na Levinson (1987), amri ni maneno ya msemaji yanayodhihirisha kuwa anataka msikilizaji atende jambo fulani au asitende.

Katika *Pendo la Karaha,* Riziki anamwamrisha Kudra, bintiye. Kudra alikuwa amepata habari kuwa Rukia, bintiye Subira, alikuwa amepata kazi ughaibuni. Kudra alitamani kupata ajira kama Rukia. Riziki alimwamrisha bintiye kuwa hangetoka kwenda kutafuta ajira. Riziki alikuwa na mamlaka ya juu kumshinda Kudra kwa hivyo alitarajia kuwa bintiye angefuata maagizo yake bila kusita. Kudra alizidi kumdadisidadisi Riziki kwa kumwambia sababu ya kutaka kutafuta kazi. Riziki alimpa amri kuwa iwapo hakuwa radhi kusoma, angemfurusha nyumbani. Vilevile, alimweleza kuwa hangemkubalia kumwita mama tena. Uso hasi wa Kudra ulitishika. Kudra alitaka kuwa huru kuchagua kufanya atakacho ila Riziki hakumkubalia. Amri ya Riziki ilimwogofya Kudra na kumfanya alifahamu kuwa iwapo angekiuka agizo la mama yake angefurushwa nyumbani. Kutokana na amri ya Riziki, Kudra aliubadili mwelekeo wake na kufanya alivyoagizwa.

#### 4.4.1.2 Kukumbushwa mambo

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (KHJ), kukumbushwa mambo kunajumuisha msemaji kutoa kauli zinazodhihirisha kuwa anamhitaji msikilizaji kukumbuka kufanya jambo fulani kila wakati. Msikilizaji anafahamu kuwa anahitajika kutekeleza jambo fulani ila msemaji anamkumbusha kuhusu adhabu inayomkabili.

Katika *Pendo la Karaha,* Nayrat alikuwa mwajiri wa kwanza wa Kudra huko ughaibuni. Uhusiano wao ulikuwa kwenye misingi ya mwajiri na mwajiriwa. Nayrat alikuwa na uwezo wa kumfuta kazi au kumwadhibu Kudra iwapo angeenda kinyume na maagizo yake. Nayrat alikuwa amemwonya

Kudra dhidi ya kuzungumza na watu wengine bila ruhusa yake. Siku moja, Kudra alikuwa amedhubutu kuzungumza na jirani yake. Nayrat alipata habari kuwa Kudra alikuwa ameikaidi amri yake. Nayrat aliyarudia maneno yake kwa ukali kuwa alikuwa amepiga marufuku kuzungumza na majirani. Kudra alijaribu kujieleza kuwa alihitaji tu kumwamkua jirani ila Nayrat alimfokea.

Uso hasi wa Kudra ulihasirika kutokana na Nayrat kumkumbusha maagizo aliyokuwa amempa kwa kumuuliza iwapo kazi iliyomleta huko ilikuwa ya kuamkuana. Kudra alitambua uzito wa swali la Nayrat na kuomba msamaha. Kudra alihofia kuwa Nayrat angemfuta kazi iwapo angerudia kosa hilo. Uhusiano kati ya Kudra na Nayrat ulianza kuharibika alipoanza kuzuiliwa na waajiri wake kutoka nje bila ruhusa.

Katika hali nyingine, Kudra alikuwa amepata kazi chini ya ulinzi wa Saumu. Hali ya kazi kwenye *Parlour* haikumfurahisha. Kudra alikuwa amekinai kufanya kazi kwa sababu Saumu alimshurutisha kujihusisha na kimapenzi wanaume wa kila aina kinyume. Wakati mwingine, Saumu alimpiga Kudra bila sababu ili kumwogofya na kumfanya afuate maagizo. Saumu alifanya juhudi zake kuhakikisha kuwa wasichana wote wangesalia katika *Parlour* hiyo ili kumtumikia Fauziya. Kudra alipania kuiacha kazi hiyo ya utumwa. Kudra alimwendea Saumu na kumwomba cheti chake cha usafiri alichokuwa amechukua wakati ambao Kudra aliajiriwa. Badala ya Saumu kumpa Kudra cheti chake cha usafiri, alimkumbusha kuwa hangempa nafasi kuondoka. Saumu aliigusia hali ya Kudra ya umaskini na kumkumbusha kuwa alijileta mwenyewe akiambatana na mwajiri wake Fauziya. Saumu alimwekea wazi kuwa hakuhusika kwa njia yoyote kumleta Kudra Dubai kwa hivyo hakuhitaji kulaumiwa. Kwa dharau, Saumu alimkumbusha Kudra hali yake ya umaskini kwa kumtajia kuwa wana wa matajiri hakutafuta ajira kwenye maeneo kama hayo. Kupitia makumbusho ya Saumu, uso hasi wa Kudra ulitipata madhara. Kudra alihisi kuwa alishinikizwa kutenda mambo kinyume na mahitaji yale. Kudra alitaka kufanya kazi ambayo ilimpa uhuru wa kuchagua. Saumu alimlazimisha Kudra kukaa kwa kukificha cheti chake cha usafiri ili kumzuia kuondoka na kumfanya alijihisi kama mtumwa. Uhusiano kati ya Kudra na Saumu uliharibika.

#### 4.4.1.3 Kutisha

Culpeper (1996) akiwanukuu Brown na Levinson (1987) anasema kuwa kutisha ni hali ya msemaji kuweka imani kwa msikilizaji kuwa jambo fulani lenye madhara litatokea. Vitisho ni mikakati inayotumiwa na msikilizaji kwa lengo la kumdunisha msikilizaji. Kudunisha msikilizaji kunaweza

kujitokeza kupitia uchokozi wa kudhihirisha onyo kupitia kauli za msemaji zenye vitisho kwa msikilizaji. Msemaji anadhihirisha kwa msikilizaji kuwa jambo fulani litachochea kuadhibiwa kwake iwapo atalipuuza.

Katika *Pendo la Karaha,* kundi la *Kuklax Klan* liliwatisha sana wenyeji wa Mombasa. Habari kuhusu kundi hilo zilisemwa kwa mnong'ono kwa sababu iwapo zingelifikia kundi hilo, aliyesema angejipata mashakani. Kuhusiana na suala la mihadarati, wanakundi hawa walifanya lolote wawezalo kuhifadhi siri yao. Baadhi ya waliodhubutu kuitibua siri ya kikundi hiki kuhusiana na madawa ya kulevya waliadhibiwa kwa kurushwa baharini. Habari kuhusu vitisho vya kundi hili zilienezwa kama njia ya kutisha wengine waliotaka kitibua siri. Mzee Sanga, babaye Kudra na mumewe Riziki, alikuwa ameutambua ukweli kuwa kundi hili lilijihusisha na madawa ya kulevya. Ongezeko la vizazi vilivyoathirika na mihadarati pamoja na shaka ya wazazi kuhusu wana vilimchochea Mzee Sanga kuitibua siri. Alitamani kuwakomesha wanakikundi hiki ila alihofia maisha yake. Wenyeji wa Mombasa walijawa na hofu wasiweze kuzungumza kinyume kuhusu kundi hili. Hatimaye, Mzee Sanga aliifichua siri kuwa kundi hili lilihusiana na mihadarati. Kundi la *Kuklax Klan* lilipata habari kuhusu maneno ya Mzee Sanga na kutamka kuwa huo ulikuwa mwisho wake. Uso hasi wa Mzee Sanga ulizidi kuhasirika hadi wakati alipokumbana na mauti yake. Waliamua kumtia adabu kwa kumuua ili liwe funzo kwa wengine la kutojishughulisha na mambo ya wengine yasiyowahusu.

Kadhalika, Saumu alifahamu kuwa Kudra hakufurahia kufanya kazi kwenye *Parlour.* Kudra alipania kupigania haki yake ya kuwa huru na kujitetea alipokandamizwa. Jambo hili lilimfanya Saumu amtolee Kudra vitisho. Saumu alikuwa na mazoea ya kuzungumza kwa sauti ya kugombana kama njia ya kumtisha Kudra. Saumu alitumia mbinu ya kumsababishia aibu kwa kumtangazia Kudra kuwa alijiona bora kuliko wengine ila hali haikuwa hivyo. Saumu alimdunisha Kudra kwa kutamka kuwa kulikuwa na wasichana warembo kumshinda ambao hawakuringa kama yeye. Pamoja na hayo, Saumu alimtisha Kudra kwa kumweleza kuwa hangevumilia kiburi chake. Kudra alitafuta namna ya kuwasiliana na ofisi za balozi wa Kenya. Saumu alipata habari kuhusu alilonuia kufanya Kudra na kumkabili kuhusiana na tuhuma hizo. Siku moja, Saumu alimpiga Kudra viboko na makofi kiasi cha kuvunja mkono. Saumu alimcharaza Kudra takriban mara saba kwa makosa madogo madogo ili kumlazimisha afuate amri yake. Ukali wa Saumu ulisababisha

woga miongoni mwa wasichana kwenye *Parlour*. Uso hasi wa Kudra ulihasirika kutokana na dhuluma iliyotumiwa na Saumu kama vitisho vya mara kwa mara.

Isitoshe, wenyeji wa eneo la Mombasa walikuwa wamechoshwa na tatizo sugu la mihadarati. Waliamua kuandamana katika juhudi za kuwakomesha wafadhili na wauzaji wa mihadarati. Waliokamatwa walikabiliwa na tishio la kushtakiwa polisi katika eneo hilo la Makupa. Jannette, mmoja wa walanguzi wa mihadarati alikamatwa. Kundi la waandamanaji lilimfikisha polisi kwa madai kuwa Jannete aliwauzia vijana mihadarati katika eneo hilo. Subira alimkabili Jannete baada ya kutambua kuwa alikuwa na ujeuri. Jannete hakutaka kukubali makosa yake. Kundi hili la waandamanaji lilijawa na hasira. Lilipania kumwuua Jannete. Wote walitamka kwa sauti moja kuwa walitaka kumwangamiza.

Kutokana na ghadhabu ya kundi hili la waandamanaji, hofu iliwaingia wote waliotaka kujihusisha na madawa ya kulevya. Washirika wa mihadarati walipata onyo kuwa wenyeji wa Mombasa walikuwa wamekataa kuendelezwa kwa biashara ya mihadarati kwa kuwa ilikuwa tishio kwa maisha ya wenyeji hususan vijana. Uso hasi wa Jannete ulihasirika. Jannete hakutaka wakazi wa eneo hilo wafahamu kuwa alikuwa anatumia mihadarati. Alitaka ukweli kuhusiana na ulanguzi wa mihadarati ubaki kuwa siri kati yake na wenzake. Siri yake ilikuwa wazi na sasa alikabiliwa na tishio la kifo. Kundi la waandamanaji liliamua kumuua Jannete ili liwe funzo wengine waliowauzia vijana mihadarati. Kwa bahati nzuri, polisi wa eneo la Makupa walimuokoa Jannete mikononi mwa waandamanaji.

### 4.4.2 Matendo yanayoarifu kitendo chanya kinachotarajiwa kuwepo

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), matendo yanayoarifu kitendo chanya kijacho cha msemaji kwa msikilizaji yanachangia katika kumpa msikilizaji shinikizo. Msikilizaji anajipata katika mtanziko kukubali au kukataa kufanya kitendo fulani.

#### 4.4.2.1 Kutoa ahadi

Brown na Levinson (KHJ) wanaeleza kuwa msemaji anapoahidi anajitolea kumfanyia msikilizaji kitu. Msemaji anaonyesha kuwa anamhitaji msikilizaji kuweka wazi iwapo atakubali kumtendea jambo fulani. Iwapo msikilizaji hayuko radhi kumtekelezea msikilizaji agizo lake, atahisi kuwa ameshurutishwa na kufungwa kwa ahadi yake aliyotoa.

Katika *Pendo la Karaha*, hali ya umaskini ilikuwa imewaleta pamoja Mwadime na Riziki. Walishirikiana katika kutatua matatizo yaliyowakabili. Mwadime alikuwa amefiwa na bibi yake. Vilevile, Mzee Sanga, bwanaye Riziki, alikuwa ameaga. Mwadime aliuona upenyu wa kumchumbia Riziki. Kutokana na heshima ya urafiki wao, Riziki hakutaka uhusiano wa kimapenzi na Mwadime. Riziki alimfahamisha Mwadime kuwa hakuridhia uhusiano kati yao kwa sababu alitaka kumakinika kumlea Kudra, bintiye. Mwadime alitaka Riziki kumuahidi kuwa atalifikiria ombi hilo. Aidha, Riziki alihisi kuwa Mwamba alimshinikiza kumpa ahadi kuhusu jambo ambalo halikumridhisha. Riziki hakutaka kuulizwa zaidi kuhusiana na suala hilo. Uso hasi wa Riziki ulikuwa umeanza kuathiirika hivyo basi ikambidi amfahamishe Mwamba kuhusiana na msimamo wake. Riziki alimtaka Mwadime auheshimu uamuzi wake na kuudumisha ujirani mwema.

### 4.4.3 Matendo yanayoarifu matamanio ya msemaji kwa msikilizaji

Kulingana na Brown na Levinson (1987), matendo yanayodhihirisha matamanio ya msemaji kwa msikilizaji yanampa msikilizaji hofu ya kupoteza kitu alichonacho kutokana na tamaa ya msemaji. Msikilizaji anapata tabu kwa sababu anafikiria kuwa atahitajika kufanya jambo ili alinde kile kinachotamaniwa na msemaji. Msikilizaji anafahamu kuwa iwapo hatafanya jambo huenda akajuta baadaye. Msemaji aghalabu huwasilisha hisia hasi zenye uzito kwa msikilizaji ili kumfahamisha kuwa kuna ulazimishaji. Msemaji anadhihirisha wazi kuwa anapendezwa na kitu alicho nacho msikilizaji na anakitaka kwa vyovyote vile.

Matendo yanayodhihirisha matamanio ya msemaji kwa msikilizaji yanachunguzwa kwenye msingi wa Brown na Levinson (KHJ). Matendo yanayodhihirika katika *Pendo la Karaha* ni: chuki, ghadhabu na ashiki.

#### 4.4.3.1 Chuki

Kulingana na Brown na Levinson (1987), chuki ni wasilisho la hisia nzito hasi za msemaji kwa msikilizaji zinazodhihirisha wazi kuwa msemaji hapendezwi na msikilizaji.

Kutokana na *Pendo la Karaha*, chuki ya Hanawi kwa Kudra ilianza baada ya Hanawi kutambua kuwa Kudra alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Salim. Awali, Salim alishirikiana kimapenzi na bintiye kwa siri. Hanawi alitambua kuwa Kudra alikuwa ameichukua nafasi yake. Hanawi aliamua kutafuta njia ya kumfurusha Kudra huko nyumbani kwao. Hanawi alimfahamisha Kudra kuwa angeitibua siri ya wizi aliotekeleza alipokuwa akifanya kazi kwa Nayrat na Aminii ili Salim

amfute kazi. Vilevile, katika kudhihirisha chuki kwa Kudra, Hanawi alimrejelea kama mtumwa bila kujali athari za maneno yake kwa Kudra. Wakati wote, Hanawi alitafuta makabiliano. Kudra alijaribu kujitetea ila Hanawi alizidi kudhihirisha chuki kwa kumtamjia Kudra kuwa hakupendezwa na upishi wake. Uso hasi wa Kudra ulihasirika kwa sababu Hanawi alitafuta namna ya kumchokoza ila Kudra hakutaka kujihusisha katika makabiliano na Hanawi. Makabiliano yaliyotokana na chuki ya Hanawi kwa Kudra yalizidi kati yao na hatimaye Kudra aliipoteza kazi.

Vilevile, Subira alikuwa na Chuki kwa Rehema baada ya kufiwa na mwanawe, Rukia. Subira alimchukia Rehema kwa sababu Rehema alikuwa amemrai Rukia kukubali nafasi ya kazi ughaibuni alikoaga dunia. Baada ya Rukia kuaga, Rehema hakuonyesha kujali wala kumpa Subira pole. Alizidi kuiendesha biashara yake na kuwatafuta wasichana zaidi kujiunga katika kusaka ajira ughaibuni. Subira aliona kuwa Rehema alichangia katika kumsababishia Rukia kifo na hivyo kumchukulia kama adui. Subira alipopita karibu na nyumbani kwa Rehema hisia za chuki zilimgubika na kuzuia kumsalimu Rehema. Kila alipopita kwa Rehema, Subira alipatwa na majonzi na kumkumbuka bintiye, Rukia. Subira alimchukia Rehema na kumuona kama aliyekosa utu.

Kadhalika, chuki ya Suzzy kwa Kudra inadhihirika baada ya kumhusisha Kudra na uovu. Suzzy akishirikiana na wasichana wenzake kazini walimhusisha Kudra na wizi wa pesa za Niri. Walichochewa na wivu na tamaa ya kuinusuru nafasi yao ya kazi. Wazee walimthamini kwa sababu aliwahudumia vyema kuliko wafanyikazi wengine wote. Mara kwa mara walimtaka Kudra awahudumie. Kudra alikuwa mchapa kazi. Alidhihirisha utu alipowahudumia wazee, jambo ambalo liliwafanya wasichana wenzake kuanza kumchukia. Kudra akiwa kazini, alijishughulisha na kufanya kilichomleta huko. Hakutaka kujihusisha na mambo ya watu wengine. Wasichana, wakiongozwa na Suzzy, walipanga njama ya kumfitini Kudra ili aondolewe kazini. Kudra alikuwa ameanza kuifurahia kazi ila alipohusishwa na wizi, aliathirika. Uso hasi wa Kudra ulipata madhara kwa sababu furaha yake ilikatizwa ghafla na madai ya wizi. Kudra alihamishwa kutoka kitengo hicho hadi kitengo cha wafu. Uso wake hasi ulitishika kwa sababu kila uchao ndoto za kutisha zilimjia na kumkosesha amani. Kudra hakuwa na jingine ila kuendelea na kazi aliyoenda kutafuta huko Dubai na iliyompatia riziki yake.

#### 4.4.3.2 Ghadhabu

Kulingana na Brown na Levinson (1987), ghadhabu ni wasilisho la hisia hasi za msemaji kwa msikilizaji zinazomdhihirishia msikilizaji kuwa msemaji amekasirika. Kutokana na ghadhabu, kuna uwezekano wa msemaji kumtakia msikilizaji mabaya.

Katika *Pendo la Karaha,* Lindo, mwanawe Kidawa alikuwa amekataa kabisa kuacha kutumia madawa ya kulevya. Kidawa alikuwa amejaribu awezavyo kumpa mawaidha ila Lindo hakubadilika. Tabia ya Lindo ilimghadhabisha Kidawa kwa sababu mwanawe hakutaka kufuata maagizo. Kwa ghadhabu, Kidawa alisema kauli hasi kwa Lindo aliyekuwa amezama kwenye matumizi ya mihadarati. Kidawa alisema kuwa Lindo hakuwa na faida yoyote. Kidawa hakujali alivyoyachukulia mwanawe matamshi aliyomtolea kwamba hata akiaga dunia walikuwa tayari kumzika. Matamshi ya Kidawa yalimsababishia Lindo kuathirika kihisia. Uso hasi wa Lindo ulihasirika zaidi kwani tabia ya ukaidi wa Lindo ilizidi. Hakuyabadili mazoea yake ya kutumia madawa ya kulevya. Uhusiano kati ya Lindo na Kidawa uliharibika na hatimaye Lindo alifariki kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Katika hali nyingine, Kassim, mwanawe Rehema alikuwa ameamua kuacha shule akiwa katika kidato cha pili.  Rehema alijaribu kumrai mwanawe arudi shule ila Kassim hakukubali. Kassim hakubandua msimamo wake kuhusu kurudi shule na akaamua kuondoka nyumbani. Kassim alipoondoka, Rehema aliamua kuacha kumrai abadili maisha yake kwa kurudi nyumbani na vilevile arudi shuleni. Kwa ghadhabu, Rehema alisema kuwa hangejishughulisha na Kassim tena. Alisema kuwa Kassim angejichagulia iwapo alitakakusoma au la. Rehema alilipuuza jukumu lake la kuwa mzazi kwa Kassim na kumpa mawaidha kama ilivyokuwa kabla ya Kassim kuondoka nyumbani. Ghadhabu ya Rehema ilichangia katika kuudhuru uso hasi wa Kassim. Hii ni kwa sababu japo Kassim hakutaka kurudi nyumbani na kuendelea na masomo, alitamani mapenzi ya mama yake. Hatimaye, Kassim alizama kabisa katika matumizi ya mihadarati mpaka wakati Rehema alipoamua kwenda kumtafuta.

#### 4.4.3.3 Ashiki

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa ashiki ni tamaa ya mapenzi. Msemaji akiwa na tamaa ya mapenzi anawasilisha hisia nzito kwa msikilizaji zinazodhihirisha kuwa msikilizaji asipokubali

kushiriki mapenzi naye atapatwa na madhara. Msemaji aghalabu huwasilisha hamu ya kumdhuru msikilizaji kwa vyovyote vile.

Ashiki inadhihirika katika *Pendo la Karaha* kupitia kwa Aminii, mwajiri wa kwanza wa Kudra. Aminii alichochewa na tamaa ya mapenzi na kumkosea heshima mwajiriwa wake. Kutokana na ashiki, Aminii alirudi nyumbani mapema baada ya kazi na kuanza kumshika Kudra maziwa yake na kwingineko mwilini. Aminii alimshikashika Kudra kwa njia ambayo hakuifurahia kumfanya Kudra ahisi kuwa ameshambuliwa. Uso hasi wa Kudra ulihasirika pakubwa kiasi cha kumweleza Aminii kuwa angeifichua tabia hiyo kwa familia yake. Uhusiano kati ya Kudra na Aminii uliharibika kwa sababu Aminii alipania kumdhuru Kudra iwapo angeitibua siri hiyo.

### 4.5 Matendo yanavyodhamiriwa kutisha nyuso chanya za wahusika katika mawasiliano katika *Pendo la Karaha*

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa uso chanya wa mshiriki katika mazungumzo unatishika ikiwa msemaji atadhihirisha wazi kuwa hajali hisia za msikilizaji. Msemaji anaweza kupuuza mahitaji ya msikilizaji na aghalabu kumtia mashakani. Matendo yanayodhamiriwa kutisha nyuso chanya yanadhihirisha kuwa msemaji hajali kuhusu mahitaji na hisia za msikilizaji. Kutokana na matendo haya, msikilizaji anafahamu wazi kuwa mahitaji yake ni tofauti na ya msemaji.

#### 4.5.1 Maoni hasi ya msemaji kuhusu mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji.

Brown na Levinson (KHJ) wanafafanua kuwa maoni ya msemaji yanadhihirishwa kupitia matendo yanayoonyesha kuwa msemaji ana maoni mabaya kuhusu anayohitaji msikilizaji. Msemaji anaweza kuonyesha kuwa hajavutiwa na kile anachokitaka msikilizaji. Vilevile, msemaji anaweza kudhihirisha kuwa hafurahii sifa za msikilizaji na haipendi imani yake. Pamoja na hayo, msemaji anadhihirisha wazi kuwa hatamini vitu alivyonavyo msikilizaji. Msemaji hupendelea kumkosoa msikilizaji anaposema jambo na kumfanya ahisi kuwa maoni yake hayathaminiwi. Baada ya msikilizaji kufanya jambo, msemaji anaweza akalalamika kuwa jambo hilo halikutendwa vizuri na hata kumpokeza msikilizaji matusi.

Katika *Pendo la Karaha*, matendo yanayodhihirisha maoni hasi ya msemaji dhidi ya uso chanya wa msikilizaji ni pamoja na: kauli za kutoridhia, matusi, dharau na makaripio.

#### 4.5.1.1 Kauli za kutoridhia

Kulingana na Brown na Levinson (1987), kutoridhia ni hali ya msemaji kumdhihirishia msikilizaji kuwa hataki kile ambacho msikilizaji anataka. Msemaji anaweza kumdhihirishia msikilizaji kuwa hapendezwi na tabia au vitendo vya msikilizaji.

Katika *Pendo la Karaha*, kauli za kutoridhia zinadhihirishwa na Riziki kwa Kudra, bintiye. Kudra alitamani kupata ajira ughaibuni ilhali Riziki alimuonya wakati wote dhidi ya kuwa na pupa maishani. Kudra alitamani kuwa kama Rukia, bintiye Subira. Rukia alikuwa ametajirika baada ya kupata kazi ughaibuni na kuweza kumwondolea Subira hali ya umaskini. Riziki aliyapuuza mahitaji ya Kudra. Badala yake, alimpa Kudra jibu lile lile kuwa alihitaji kumakinika masomoni. Uso chanya wa Kudra ulihasirika kutokana na Riziki kukataa kuridhia matamanio yake.

#### 4.5.1.2 Matusi

Kulingana na Brown na Levinson (1987), kutusi ni kuwasilisha la hisia zinazojumuishwa katika kauli chafuchafu za msemaji kwa msikilizaji. Kauli hizi chafuchafu zinadhihirisha kuwa msemaji hapendezwi na sifa za msikilizaji. Msemaji anapomtusi msikilizaji anadhihirisha kuwa ana maoni hasi kuhusu mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji. Msemaji anaeleza wazi kuwa hapendi kitendo fulani cha msililizaji na hampi thamani yoyote.

Katika *Pendo la Karaha,* Lindo, mwanawe Kidawa alikuwa amejiingiza katika matumizi ya mihadarati. Kidawa alimshuku Mwamba kuwa alikuwa amemroga Lindo ili asiache kuitumia mihadarati. Kidawa alimtusi Mwamba kuwa alikuwa mchawi kwa kumtendea Lindo uovu. Kidawa alimshambulia Mwamba na kumtajia kuwa alikuwa amechangia katika Lindo kuzama katika matumizi ya mihadarati. Mwamba alijaribu kujitetea ila Kidawa hakumpa nafasi. Kidawa aliendelea kumtusi Mwamba hadharani akiwa kazini kwake na kumsababishia aibu. Kidawa alimwahidi Mwamba kuwa angemwombea mabaya yampate kama alivyokuwa amemfanyia Lindo. Kidawa alimtusi tena Mwamba kuwa yeye ni nyoka, ziraili, mwanaharamu, mshenzi na mchawi. Kutokana na ghadhabu ya Kidawa, povu lilimtoka mdomoni wakati wa kutamka matusi. Mwamba hakuweza kustahimili tena matusi ya Kidawa. Mwamba alijaribu kutafuta maafikiano na Kidawa ila alitambua kuwa Kidawa hakutaka kumsikiliza. Alishindwa kuelewa ni vipi rafiki yake wa miaka mingi angeweza kumhusisha na maovu bila ushahidi wowote. Mwamba na Kidawa walianza ugomvi na kurushiana matusi makali yaliyowasababisha kupoteza nyuso zao chanya.

Katika hali nyingine, matusi yanadhihirika baina ya Lindo, mwanawe Kidawa na Kassim, mwanawe Rehema. Lindo alifika kwa Mwamba na kumpata Kassim akicheza mchezo wa bao. Lindo alitaka kucheza kwa lazima ila zamu ilikuwa ya Kassim. Kwa utaratibu, Kassim alimweleza Lindo kuwa alihitaji kusubiri zamu yake ili kucheza. Lindo hakutaka kumsikiliza Kassim kwa madai kuwa alizoea kumwonea. Vitendo vya Lindo kwa Kassim vilichangia mwanzo wa matusi haya. Kassim alimweleza Lindo kuwa hakutaka uzushi wake wa kilevi. Kutokana na kutajiwa ulevi, Lindo alipandwa na hasira na kuanza mgogoro mkubwa. Kassim alimwona Lindo kama mjinga na mwanaharamu. Lindo hayakuyachukulia matusi ya Kassim kwa urahisi kwa hivyo akaamua kulipiza kisasi. Lindo alimweleza Kassim kuwa aliishi kama mwanaharamu japo alikuwa na wazazi wote. Hata hivyo, Kassim alimrejelea Lindo kama fala. Lindo alimrudishia Kassim matusi yale yale na kumfahamisha kuwa aliishi kama fala mwenyewe kwa kuyaacha maisha mazuri nyumbani kwao. Lindo na Kassim walitamkiana maneno yenye matusi yaliyoenda kinyume na matarajio ya nyuso zao chanya.

#### 4.5.1.3 Dharau

Kulingana na Brown na Levinson (1987), msemaji anapomdharau msikilizaji anamshusha hadhi ili kumdhihirishia kuwa hataki kwa vyovyote vile kujihusha na msikilizaji.

Katika *Pendo la Karaha*, Hanawi alimdharau Kudra baada ya kutambua kuwa alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Salim, baba yake. Hanawi alitafuta makabiliano na Kudra kila wakati. Vivyo hivyo, Kudra alimdharau Hanawi kwa kukubali kushirikiana kimapenzi na Salim aliyekuwa baba mzazi wa Hanawi. Salim hakuweza tena kustahimili makabiliano kati ya bintiye, Hanawi na mwajiriwa wake, Kudra. Alikuwa ameuona mgogoro uliokuwepo kati yao. Hanawi alitafuta nafasi kugombana na Kudra kila wakati naye Kudra alitafuta mbinu ya kujitetea. Japo kuwa Salim alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Kudra, aliamua kumwandikia Kudra barua na kumjuza kuwa alikuwa amemfuta kazi. Kudra alijaribu kumrai mwajiri wake kuubadili msimamo wake ila halikuwezekana. Salim alishikilia kuwa alitaka heshima kati yao idumu. Kudra aligharamika kwani uso wake chanya ulihasirika katika juhudi za kuidumisha heshima. Alielewa kuwa hakutakikana tena kufanya kazi kwa Salim na hivyo basi akaamua kuondoka bila kusababisha vurugu.

Kadhalika, Rehema alimwonyesha Riziki dharau na kumtishia uso chanya. Kudra alikuwa ameueleza ubalozi wa Kenya kuwa hali ya kazi ughaibuni ilikuwa mbaya. Juhudi za kuwanusuru wasichana kutoka eneo hilo zilianza. Riziki alipata habari kuwa Kudra angefika nyumbani. Muda alioelezwa kuwa Kudra angefika ulipita na Kudra hakutokea. Hofu juu ya mwanawe ilimkabili Riziki na kumfanya afike kwa Rehema ili kupata maelezo zaidi. Rehema alijifanya kuwa hakufahamu Kudra alikuwa nani. Isitoshe, Rehema alimweleza Riziki kuwa Kudra hakushurutiswa kwenda ughaibuni, alijichagulia mwenyewe. Japo Rehema alipuuza malalamiko ya Riziki na kumtajia kuwa alikuwa huru kwenda kumshtaki polisi. Rehema alimdharau huku akimcheka kwa sababu alifahamu kuwa polisi hawangeweza kumchukulia hatua yoyote. Uso chanya wa Riziki ulihasirika na vilevile uhusiano kati ya Riziki na Rehema kuharibika.

#### 4.5.1.4 Makaripio

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), makaripio ni matendo ya msemaji yanayohusu msemaji kumwelekeza msikilizaji maneno kwa njia kali. Msemaji huwasilisha kuwa hapendezwi na yale yanayosemwa na kutendwa na msikilizaji.

Katika *Pendo la Karaha*, Nayrat, mwajiri wa kwanza wa Kudra alikuwa na mazoea ya kumkaripia Kudra alipokosea kufanya jambo ndogo. Nayrat alimtusi kuwa yeye ni mbwa. Kupitia uwezo wa Nayrat wa kuweza kumfutwa kazi, Kudra hakuthubutu kusema lolote kwa hofu. Nayrat alimfanyisha Kudra kazi hata akiwa mgonjwa. Kudra alikuwa amemweleza Nayrat kuwa hali yake ya afya ilikuwa mbaya ila Nayrat hakuonekana kujishughulisha na hilo. Alijikaza kufanya kazi. Nayrat alipoona kuwa Kudra hangeweza kuendelea kufanya kazi, alimkaripia Kudra kwa kumwambia kuwa alikuwa mvivu na kumpa ruhusa ya kwenda kulala. Aidha, uso chanya wa Kudra ulitishika. Kudra alitaka kukubalika na Nayrat kama mwajiriwa wake na kuheshimiwa. Kukaripiwa mara kwa mara kulimfanya Kudra ahisi kuwa Nayrat hakumthamini.

### 4.5.2 Msemaji kupuuza uso chanya wa msikilizaji

Brown na Levinson (1987) wanafafanua kuwa matendo ya kupuuza uso chanya wa msikilizaji yanadhihirisha kuwa msemaji hajali kabisa kuhusu matamanio ya msikilizaji. Msemaji anachukulia kuwa anachohitaji msikilizaji hakina umuhimu wowote. Hisia za msikilizaji zinakosa kutiliwa maanani na katika mazungumzo. Msemaji aghalabu hudhihirisha nguvu zake dhidi ya

msikilizaji. Vilevile, msemaji anafurahia kumtia msikilizaji aibu. Isitoshe, msemaji hutaka kumpa msikilizaji sababu ya kumwogopa kama ishara ya kuheshimiwa.

Matendo ya msemaji kupuuza uso chanya wa msikilizaji yaliyotajwa na Brown na Levinson (KHJ) katika *Pendo la Karaha* ni pamoja na: nguvu, kuepuka mjadala, kutamka habari hasi na kuringa, kutaja mada inayosababisha mlipuko wa kihisia na kujitenga.

#### 4.5.2.1 Nguvu

Culpeper (1996) akimnukuu Brown na Levinson (1987) anaeleza kuwa utoupole unatokana na upole uliokiukwa. Culpeper anaafiki kuwa nguvu ni kigezo kinachoweza huchangia kuleta athari hasi kwenye uso wa msikilizaji. Aidha, Sadeghoghli na Niroomand (2016) nao wakimnukuu Moon (2001) wanaeleza kuwa kutambua msemaji na msikilizaji kwenye msingi wa uhusiano wa nguvu, kiwango cha kijamii na urafiki kunasaidia kutambua ufasaha wa uzito wa kauli zinazotolewa.

Katika *Pendo la Karaha,* Riziki anadhihirisha nguvu dhidi ya Kudra, binti yake. Siku moja Kudra alikuwa amechelewa kufika nyumbani mapema na alipofika alimpata Riziki akimsubiri. Kudra alifahamu kuwa alikuwa amemkosea mamaye. Ili kufidia kosa hilo, Kudra alimwamkua Riziki. Riziki alidhihirisha nguvu zake kwa Kudra alipompiga kofi badala ya kuzijibu salamu za bintiye japo kuwa alizipokea. Riziki alitamka kuwa Kudra alikuwa ameanza kufuata mwelekeo hasi na hakumtaka arudie kosa hilo. Riziki alitoa kauli kuwa iwapo Kudra angezidi kuikaidi amri yake angemfurusha nyumbani. Riziki alipania kufanya lolote ili kuhakikisha kuwa Kudra amekuwa mwenye nidhamu hata ikiwa ni kutumia mbinu ya vita. Kudra alitishika. Alifahamu wazi kuwa Riziki hakufurahishwa na tabia yake ya kuchelewa nyumbani. Vilevile, uso chanya wa Kudra ulihasirika baada ya Riziki kupuuza kujibu salamu zake.

#### 4.5.2.2 Kuepuka mjadala

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), kuepuka mjadala ni kwenda kinyume na yale yanayojadiliwa kwa kuzungumzia mengine. Tendo la kuepuka mjadala linadhihirika iwapo katika mazungumzo, msemaji atamtajia msikilizaji mambo ambayo hayamhusu. Msemaji anaweza kuepuka mjadala kwa kupuuza mambo ambayo msikilizaji anayachukulia kwa uzito na kumwathiri msikilizaji pakubwa. Msemaji anadhihirisha kuwa hamthamini ya msikilizaji. Isitoshe, msemaji hatilii maanani hofu na ugumu wa maisha unaomkabili msikilizaji.

Katika *Pendo la Karaha,* tendo la kuepuka mjadala linadhihirika kupitia kwa Nayrat. Hali ya Riziki, mamaye Kudra ilikuwa taabani. Kudra alimweleza Nayrat kuhusu ugonjwa wa Riziki na kwamba alihitajika kumtumia mamaye pesa za matibabu. Nayrat alipuuza kuwa Kudra alihitaji jibu la dharura. Nayrat aliuepuka mjadala kwa kumtajia Kudra kuwa walihitaji muda zaidi kufikiria suala hilo. Nayrat alisema kuwa angezungumza na Aminii ili wampe mwelekeo zaidi kuhusiana na suala la mshahara ila hakutaja ingekuwa lini. Kutokana na mapuuza ya Nayrat, uso chanya wa Kudra ulihasirika. Kudra alihisi kuwa mahitaji yake hayakushughulikiwa kikamilifu na waajiri wake.

Vivyo hivyo, Aminii aliepuka mjadala alipojuzwa na Kudra kuwa aliwataka wawe wakimkata nusu ya mshahara wake ili aweze kumsaidia Riziki. Aminii aliepuka mjadala uliozuliwa na Kudra na kumfahamisha kuwa walikuwa wamesahau kumkata gharama ya ndege katika mshahara wake. Maneno ya Aminii kwa Kudra yanaashiria kuwa hakumdhamini Kudra. Kando na aliyokuwa akiagiza Kudra, Aminii alimweleza Kudra kuwa hangeupata mshahara. Aminii alitumia njia ya mkato kusema kuwa walimkata mshahara bila idhini yake ili wamlipe ajenti Rehema dola elfu tano. Katika mazungumzo yao, Aminii alipuuza hisia za Kudra. Bila huruma yoyote, alimweleza Kudra kuwa pamoja na kumlipa ajenti, wangemkata mshahara zaidi kutokana na hali duni ya kibiashara. Kudra alikwazika kihisia. Uso chanya wa Kudra ulihasirika kutokana na maneno ya Aminii na kumfanya afahamu kuwa Nayrat na Aminii hawakumthamini. Kudra alitaka kujumuishwa katika uamuzi kuhusiana na mshahara wake ila haikuwa hivyo.

Katika hali nyingine, Hanawi, bintiye Salim alipokuwa akigombana na Kudra, alimweleza kuwa angetafuta namna ya kumwondoa kazini. Hanawi aliifahamu siri ya Kudra kuhusiana na alivyowaibia waajiri wake wa kwanza, Nayrat na Aminii. Hanawi alihamisha makini ya Kudra kutoka kwa Salim na kumtisha kuwa angeitibua siri ya wizi. Hanawi alipanga njama ya kumkomesha Kudra kuhusiana kimapenzi na baba yake. Vilevile, Hanawi alimtajia Kudra kuwa alikuwa na tamaa na kufaidika kutokana na mali ya Salim. Japo kuwa Kudra alitishika, alimweleza Hanawi kuwa hakufaa kuingilia uhusiano wao. Uso chanya wa Kudra ulihasirika baada ya Hanawi kuzua mjadala ulioweza kumtia mashakani.

**4.5.2.3 Msemaji kutamka habari hasi na hata kuringa.**

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa msemaji anapomtamkia msikilizaji habari zenye ujumbe hasi huwa anadhamiria kumtesa. Vilevile, msemaji anaweka wazi kwa msikilizaji kuwa

hajali chochote kuhusu hisia za msikilizaji. Aghalabu, msemaji anaweza kumringia msikilizaji kama njia ya kumuudhi.

Katika *Pendo la Karaha,* Rehema alikuwa ameendelea sana kimaisha. Biashara yake ya kuwasafirisha wasichana kwenda ughaibuni ilimpa kipato cha juu. Alimfukuza mumewe, Mzee Choka kwa sababu aliona kuwa hakumhitaji tena. Rehema alinunua mabasi na kuyapa jina "Maisha ni hiari yako," ili kuwasuta maadui wake kuwa maisha ya waliomzunguka hayakumhusu. Wenyeji wa Mombasa walifasiri kuwa Rehema hakujali kilichowatendekea wasichana aliowapeleka ughaibuni kwa ajira. Hata baada ya malalamiko magazetini, Rehema alidhihirisha kiburi chake kwa kutembea kwa maringo. Aidha, aliongeza semi nyingine kwenye magari yake kuwa waliomsema wangemsema na kuchoka kwa sababu hatimaye wangefariki. Kwenye upande mwingine, Subira aliomboleza kifo cha bintiye, Rukia, huku Rehema akifurahi. Rehema alizidi kujitajirisha na kujenga majumba katika eneo nzima la Changamwe. Kama wakala, Rehema hakujali kuhusu maisha ya wasichana aliowapeleka ughaibuni akiwemo Kudra, mwanawe Riziki. Maneno na matendo ya Rehema yalihasiri uso chanya wa Mzee Choka, Subira na Riziki. Vilevile, nyuso za wakaazi wa Mombasa zilihasirika kutokana na kiburi chake.

#### 4.5.2.4 Kujitenga

Brown na Levinson (KHJ) wanaeleza kuwa njia ya kujitenga inadhihirisha kuwa msemaji anakataa kushiriki katika mambo ya msikilizaji. Msemaji anaweza kujitenga kutokana na mambo ya msikilizaji iwapo atamkatiza usemi msikilizaji zamu yake ya kuzungumza ikifika. Vilevile, msemaji anaweza kumdhihirishia msikilizaji kuwa ameipoteza makini yake katika jambo analolisema msikilizaji.

Katika *Pendo la Karaha,* Riziki anajitenga kutokana na Kidawa, rafiki wa miaka mingi. Baada ya Kudra kupata kazi ughaibuni, maisha ya Riziki yalibadilika na kuhamia katika eneo jipya kwa jina *New Horizon*. Riziki alianza kumsahau rafiki yake Kidawa. Awali, marafiki hawa walikuwa wakishirikiana kwa mambo ila baada ya Riziki kuhama, ushirikiano wao ulipungua. Aghalabu, Kidawa alijaribu kuudumisha uhusiano wake na Riziki kwa kumtembelea. Siku mmoja, Kidawa alimtembelea Riziki. Baada ya kuamkuana, Riziki alionekana kulisahau jina Kidawa kabisa kwa sababu alikuwa amepata marafiki wapya. Siku nyingine Kidawa alijitolea kumtembelea Riziki. Kutokana na mabadiliko ya Riziki, hakupata nafasi ya kuzungumza na Kidawa kama awali. Riziki

alimpuuza Kidawa waziwazi na kuzungumza kwenye simu kwa muda mrefu na mjenzi aliyetaka kufahamu saruji ambayo angenunua. Riziki hakumpa Kidawa makini kama alivyofanya walipokuwa wakiishi katika mtaa sawa kabla ya Riziki kuhamia katika eneo jipya kwa jina *New Horizon.* Kutokana na kujitenga kwa Riziki, Kidawa alihisi kuwa uhusiano kati yao ulikuwa umeharibika. Riziki alimtenga kutokana na hali yake duni ya kimaisha na kumkwaza Kidawa kihisia. Uso chanya wa Kidawa uliharibika alipoona kuwa Riziki hakuuthamini urafiki wao.

Kadhalika, mhudumu katika hoteli maarufu kwa jina *Oak Tree* alidhihirisha kujitenga na Kudra. Hali ya umaskini iliyomkabili Kudra ilimfanya aamue kutafuta kazi. Kudra alipofika kwenye ofisi ya mhudumu, hakujua namna ya kujieleza. Alijaribu awezavyo kujieleza ila alisitasita asijue la kusema. Mhudumu alimdhihirishia Kudra waziwazi kuwa alikuwa ameipoteza makini kwa kile alichokisema. Kudra alidhihirisha kuchanganyikiwa kwingi naye mhudumu akampuuza. Bila kujali hisia za Kudra, mhudumu alimweleza Kudra kuwa hakufahamu alichokitaka huku akiifunga ofisi na kumwacha Kudra akiwa amejistaajabia. Uso chanya wa Kudra ulihasirika. Kudra alitaka kukubalika na kueleweka. Kitendo cha mhudumu kuifunga ofisi kilidhihirisha kuwa hakutaka kujihusisha kwa vyovyote vile na Kudra. Mhudumu alimfanya Kudra ajihisi kuwa hafai.

**HITIMISHO**

Katika sura hii, tumeanza kwa kujadili uso hasi na uso chanya ili kupata msingi kuhusiana na nyuso za wazungumzaji. Tumeigawa sura hii katika sehemu mbili kuu. Sehemu ya kwanza imechunguza matendo msemaji yanayodhamiriwa kutisha nyuso hasi za wasikilizaji katika mawasiliano katika *Pendo la Karaha*. Vivyo hivyo, sehemu ya pili imechunguza matendo msemaji yanayodhamiriwa kutisha nyuso chanya za wasikilizaji katika mawasiliano. Matendo hayo yamechunguzwa kwenye msingi wa Brown na Levinson (1987).

Imebainika kuwa katika mawasiliano, vitendo vya msemaji vinavyoathiri uso hasi wa msikilizaji katika *Pendo la Karaha* ni pamoja na: kuamrishwa, kukumbushwa mambo, kutishwa, kutoa ahadi, kuchukiwa, kuelekezwa ghadhabu, ashiki na chuki. Aidha, vitendo vinavyoathiri nyuso chanya katika *Pendo la Karaha* pamoja na: kupokezwa matusi, kuelekezwa kauli za kutoridhia, kudharauliwa, kukaripiwa, kudhihirishiwa nguvu, kutamkiwa habari hasi na kutengwa.

Imedhihirika kuwa katika mawasiliano, wazungumzaji hudhihirisha matamanio tofauti tofauti. Vilevile, sababu mbalimbali humchochea msemaji kutenda matendo kwa lengo la kumtimizia msikilizaji matamanio yake au kuyapuuza. Ikiwa matamanio ya msikilizaji yatapuuzwa na msemaji, uso msikilizaji utahasirika. Vivyo hivyo, ikiwa matamanio ya msikilizaji yatatiliwa maanani na msemaji, uso msikilizaji utaimarika. Isitoshe, katika mawasiliano, heshima baina ya msemaji na msikilizaji ni kigezo muhimu katika kuimarisha au kuudhuru uso.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii inajumuisha muhtasari wa tasnifu kuanzia sura ya kwanza hadi sura ya nne. Katika kuangazia sura mbalimbali, malengo ya utafiti yanachunguzwa ili kutambua iwapo yameafikiwa au la. Aidha, tunaihitimisha sura kwa kutoa mapendekezo kuhusu tafiti zijazo.

### 5.1 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti

Utafiti wetu umejikita katika malengo matatu yanayochunguzwa ili kupata matokeo ya utafiti. Malengo haya ni pamoja na: kuchunguza upole unavyodhihirika katika riwaya ya *Pendo la Karaha,* kubaini namna utoupole unavyojitokeza na kubainisha matendo yanayoathiri nyuso za wahusika katika mazungumzo katika *Pendo la Karaha.*

Lengo la kwanza linalohusu kuchunguza upole katika *Pendo la Karaha* limeafikiwa katika sura ya pili. Mikakati yote minne iliyopendekezwa na Brown na Levinson (1987) imedhihirika kikamilifu kupitia kauli mbalimbali za wahusika zenye upole na matokeo yake ni haya:

Mikakati Chanya ya Upole (MCU) ilipendelewa sana na wahusika katika kuimarisha nyuso za wenzao katika mazungumzo kupitia kwa njia ya kuwa na matumaini, kutambua mahitaji ya msikilizaji na kuyashughulikia, vitambulisho vya makundi, kutafuta makubaliano, kuepuka migogoro, kujumuisha wasemaji katika mambo na njia ya kuteua na kuchangia mada inayomvutia msikilizaji. Kauli za Subira kwa Riziki, Kidawa kwa Riziki, Rehema kwa Kudra, Riziki kwa Kudra, Kudra kwa Almasi na mazungumzo kati ya Mheshimiwa Jumbe na Spika yanadhihirisha kuwepo kwa MCU katika *Pendo la Karaha*.

Mikakati Hasi ya Upole (MHU) ilidhihirika kupitia njia zifuatazo: njia ya kuwa bila matazamio, kudhihirisha heshima baina ya wazungumzaji, kuomba msamaha na njia ya kutaja kwa jumla. Kauli za Kudra kwa Nayrat, Kudra kwa Rehema, Salim kwa Kudra, Riziki kwa Kudra, Kassim kwa Rehema, Riziki kwa Mwadime na Spika kwa Mheshimiwa Kajembe zinadhihirisha kuwepo kwa MHU. Aidha, Mkakati wa Upole Ndani ya Rekodi (MNR) ulichunguzwa kupitia njia zifuatazo: kumnufaisha msikilizaji, kushughulikia dharura, kukabiliana na tofauti za kimamlaka na muktadha wa kutoa ahadi kwa msikilizaji. Kauli za Rehema kwa Rukia, Rehema kwa Mzee

Choka, Kassim kwa Rehema, Kudra kwa Aminii na Riziki kwa Kidawa zinadhihirisha wazi kuwepo kwa MNR.

Kadhalika, Mikakati Nje ya Rekodi (MNjR) ilidhihirika kupitia njia zifuatazo: kutumia maswali ya balagha ili kuzua utata, matumizi ya kinaya na kudokeza mambo ili kuzua utata. Kauli za Zinduna kwa Rehema, Kassim kwa Rehema, Dele na Kele kwa Kudra, Jannete kwa Lindo na Kidawa kwa Lindo zinadhihirisha kuwepo kwa MNjR katika *Pendo la Karaha*.

Kadhalika, lengo la pili linahusu kubaini utoupole unavyojitokeza limeafikiwa katika sura ya tatu. Mikakati yote ya utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996) imedhihirika kikamilifu katika *Pendo la Karaha* kupitia kauli mbalimbali za wahusika na matokeo yake ni haya:

Mikakati Chanya ya Utoupole (MCUt) ilipendelewa sana na wahusika katika kuhasiri nyuso za wenzao katika mawasiliano. Njia zifuatazo zilichunguzwa katika kubaini kuwepo kwa mikakati hiyo: kauli zenye matusi, kutafuta makabiliano na kumtenga msikilizaji. Kauli za Nayrat kwa Kudra, Hanawi kwa Kudra, Kidawa kwa Mwamba, Riziki kwa Kidawa, Kassim kwa Rehema na Kassim kwa Lindo zinadhihirisha wazi kuwepo kwa MCUt katika *Pendo la Karaha*. Aidha, Mikakati Hasi ya Utoupole (MHUt) ilichunguzwa kupitia njia zifuatazo: kumhusisha msikilizaji na maovu, kuingilia faragha ya msikilizaji na kutisha. Kauli za Suzzy kwa Kudra, Saumu kwa Kudra, Aminii kwa Kudra, Nayrat kwa Kudra, Kidawa kwa Mwamba, Kundi la *Kuklax Klan* kwa Mzee Sanga na Kundi la Waandamanaji kwa Jannete zinadhihirisha kuwepo kwa MCUt.

Katika hali nyingine, Mikakati ya Utoupole Ndani ya Rekodi (MUtNR) ilichunguzwa kupitia njia zifuatazo: kutoa onyo na kutoa taarifa. Ilibainika kuwa kauli za Riziki kwa Kudra, Kidawa kwa Lindo, Rehema kwa Kassim, Kassim kwa Lindo, Rehema kwa Mzee Choka na Mhudumu wa hoteli ya *Oak Tree* kwa Kudra zinadhihirisha MUtNR. Vilevile, Mikakati ya Utoupole yenye Dhihaka (MUtD) inadhihirika kupitia kauli za Saumu kwa Kudra, Nayrat kwa Kudra, Rehema kwa Riziki na Kassim kwa Lindo zinazodhihirisha kuwepo kwa MUtD. Pamoja na hayo, Mikakati ya Kuuzuia Upole (MKU) ilichunguzwa kupitia njia zifuatazo: kujizuia kusamehe, kujizuia kusalimu na kujizuia kujibu salamu. Kauli za Riziki kwa Kudra, Subira kwa Rehema na Kassim kwa Rehema zinadhihirisha kuwepo kwa MKU katika *Pendo la Karaha*.

Tumebaini kuwa, muktadha ni muhimu sana katika kutambua kuwepo kwa utoupole. Vilevile, Imebainika kwa sio kila aina ya utoupole ni mbaya. Utoupole umeweza kuwa njia ya kuadilisha

haswa ule uliodhihirika kupitia MUtNR iwapo utoupole unatekelezwa na mzazi kwa mtoto kutegemea muktadha husika.

Vivyo hivyo, lengo la tatu linalohusu kubainisha matendo yanayoathiri nyuso za wahusika katika mazungumzo katika *Pendo la Karaha* limeafikiwa kupitia sura ya nne. Matokeo ya lengo hili ni yafuatayo:

Matendo mbalimbali ya wahusika yanachangia katika kuathiri nyuso chanya na nyuso hasi za wahusika wenzao. Baadhi ya matendo yalivyoainishwa na Brown na Levinson (1987) yanadhihirika katika *Pendo la Karaha.* Matendo ya msemaji yanayoathiri uso hasi wa msikilizaji yamebainika katika sehemu zifuatazo: kuna matendo yanayoarifu msikilizaji kuhusu vitendo hasi vijavyo kama vile amri, kukumbushwa mambo na kutishwa. Vilevile, matendo yanayoarifu kitendo chanya kinachotarajiwa kuwepo yamejitokeza kupitia kwa msemaji kutoa ahadi zinazompa msikilizaji shinikizo la kufanya jambo. Kadhalika, matendo yanayoarifu matamanio ya msemaji kwa msikilizaji kama vile chuki, ghadhabu na ashiki yamebainika kuutisha uso hasi wa msikilizaji.

Pamoja na hayo, matendo ya msemaji yanayoathiri uso chanya wa msikilizaji yamebainika katika sehemu zifuatazo: wasemaji wanawapa wasikilizaji maoni hasi kuhusu nyuso zao chanya kupitia kwa kuwatolea kauli hasi za kutoridhia mambo, kuwadharau, kuwatusi na hata kuwakaripia. Vilevile, wengine wanazipuuza nyuso chanya za wasikilizaji kupitia kwa kudhihirisha nguvu zao, kuepuka mijadala, kutamka habari hasi na kuringa pamoja na kujitenga na wasikilizaji wao.

**5.2 Mapendekezo kuhusu tasnifu zijazo**

Utafiti huu umechunguza upole na utoupole katika riwaya kwenye misingi ya mikakati ya upole iliyopendekezwa na Brown na Levinson (1987) na mikakati ya utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996). Tafiti za baadaye zinaweza kuchunguza: umuhimu wa upole na utoupole katika kufanikisha mtiririko wa matukio katika riwaya, upole na utoupole katika kuendeleza maudhui ya riwaya za mwandishi mmoja au hata changamoto zinazojitokeza katika udhihirishaji wa upole na utoupole katika riwaya. Mada kuhusiana na utoupole haijachunguzwa sana katika kazi za fasihi andishi kwa hivyo mgao huu unaweza kuchunguzwa zaidi.

## 5.3 Hitimisho

Kutokana na uchunguzi huu, imebainika wazi kuwa nadharia ya upole na nadharia ya utoupole za kipragmariki zinaweza kutumiwa kwa pamoja katika kuchunguza kazi za kifasihi na haswa riwaya. Kutegemea hali ya maisha inayowakabili wazungumzaji, msemaji anaweza kuteua mikakati mahususi ya upole au utoupole kutegemea haja yake ya mawasiliano. Katika mawasiliano, heshima baina ya msemaji na msikilizaji ni kigezo muhimu katika kuimarisha au kuudhuru uso. Imebainika kuwa wahusika waadilifu waliokabiliwa na tatizo la utoupole walitafuta mikakati mbalimbali ili kuleta ushirikiano miongoni mwao. Baadhi yao kama vile Kudra walitafuta namna mbalimbali za kuepuka ugomvi.

## MAREJELEO


Aydınoğlu, N. (2013). "Politeness and Impoliteness Strategies: An Analysis of Gender Differences in Geralyn L. Horton's Plays". *Procedia - Social and Behavioral Sciences*. 83: 473 - 482.

Bernal, M. (2008). *Do Insults Always Insult? Genuine Impoliteness versus Non-Genuine Impoliteness in Colloquial Spanish.* Pragmatics 18: 781-802.

Bousfield, D. & Miriam, L. (2008). *Impoliteness in Language.* Berlin: Mouton de Gruyter.

Brown, P. & Levinson, S. (1987). *Politeness: Some Universals in Language Usage*. Cambridge: Cambridge University Press.

Culpeper, J. (1996). *Towards an Anatomy of Impoliteness*. Journal of Pragmatics, 25, 349-367.

Culpeper, J., Derek, B., and Anne, W. (2003). Impoliteness revisited: with special reference to dynamic and prosodic aspects. *Journal of Pragmatics*, 35 (2003) 1545–1579. Imepakuliwa kutoka http://id.scribd.com.doc/20554.

Culpeper, J. (2005). Impoliteness and entertainment in the Television Quiz Show: The Weakest Link. *Journal of Politeness Research: Language, Behavior and Culture* 1, 35-72.

___________ (2011) *Impoliteness – Using Language to Cause Offence.* Cambridge: University Press.

Eelen, G. (2001). *A Critique of Politeness Theories*. Manchester: St. Jerome.

Fraser, B. (1990). *Perspectives on Politeness*. Journal of Pragmatics, 14: 219-236.

Goffman, E. (1959). *The Presentation of Self in Everyday Life*. New York: Double day.

_________ (1967). *Interaction Ritual; Essays on Face-to-face behavior*. Garden city, NY: Doubleday.

Goro, M. (2014). *An Analysis of Impolite Language used by Matatu Conductors: A case of Matatus Plying Route 32 from Nairobi City to Dandora*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Grice, H.P. (1975). *Logic and Conversation*, In Cole, P & Morgan, J. *Syntax and Semantics*, vol.3, New York: Academic Press.

Gromov, M. D. (2018). Three Novels of John Habwe: Social Criticism through "New Enlightment"? *Journal of Language, Technology and Entrepreneurship in Africa*, 9(1): 90-100.

Habwe, J. (2014). *Pendo la Karaha*. Nairobi: Moran East African Publishers Limited.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Inziani, E. (2017). *Mikakati ya Upole katika Mstahiki Meya.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Joan, L. B. (2015). *Pragmatic Analysis of Politeness Strategies in British TV Series Sherlock.* Sarjana Sastra unpublished thesis, Yogyakarta State University.

Kihara, S. (2016). *Nafasi ya Vijana katika Riwaya za Pendo la Karaha* na *Kovu la Moyoni.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kinyua, G. (2015). *Ukiukaji wa Kanuni za Upole katika Mhanga wa Nafsi Yangu.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Lakoff, R. (1973) *The Logic of Politeness; On minding your p's and q's.* Paper from the 9th Regional Meeting. Chicago Linguistic Society. Chicago Linguistic Society University.

Leech, J. (1983). *Principles of Pragmatics*. London: Addison-Wesley.

Machira, S. (2015). *Uchambuzi wa Mikakati ya Upole kama Inavyotumiwa na Wahusika Wakuu katika Tamthilia ya Mbaya Wetu.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999) *Research Methods. Qualitative and Quantitative Approaches.* Nairobi: Acts press.

Ngisirei, M. (2018). *Uchambuzi wa Upole katika Vipindi vya Sobetab Kapchi katika idhaa ya Kass FM.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Nyangi, L. C. (2017). Uchanganuzi *wa Kipragmatiki katika Filamu za Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Oruka H.O (1990). *Ethics.* Nairobi: Nairobi University.

Raitania, A. (2014). *Mikakati ya Upole katika Vipindi vya Runinga*: *Mawaidha na Bi. Msafwari katika Runinga ya Citizen*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Sadeghoghli, H. & Niroomand, M. (2016). Theories on Politeness by Focusing on Brown and Levinson's Politeness Theory. *International Journal of Educational Investigations*, 3(2), 26-39.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi* 1: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.

Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho I: Udhihirikaji wa Upole

Rukia alibanduka shuleni akawa anafanya kazi ya kuuza leso kwa Rajiv hapo bondeni, Mombasa. Hapo ndipo alipokutana na wakala akamtia maneno, "**Njoo mwanangu nikupe kazi**." Alisema Rehema kwa tabasamu tele midomoni. **"Kazi gani mama?"** Rukia alimuuliza Rehema. "Kazi ya Uarabuni, **Bi. Mdogo**. **Kazi wala sio huu utumwa wa Rajiv usiokufaidi**." (Uk.5)

"Hutaki shule, wataka nini? Kuolewa?" Riziki alimsemesha Kudra kwa ukali. "**Si kuolewa mama. Mimi nataka kazi ili nikusaidie ata wewe kujikimu."** Kudra alisema. "Kama hutaki kusoma, hapa sikutaki na mimi, katu usipate kuniita mamako," Riziki alisema. (Uk.7)

"Kama unataka kulewa, lewa kabisa hiyo dawa ya unga ikuue, tutakuzika maana huna faida," Kidawa alimweleza Lindo kwa ghadhabu. "**Usimwambie hivyo dadangu**," Riziki naye alimshauri mwenzake aliyekarambuka kwa fundo la hasira moyoni. "Ana faida gani? Hayawani huyu hasa. Alewa kokuteli. Alewa 'unga'." "**Ukimlea mwana mwema, mui pia mlee,**" Riziki alimwambia kidawa ili kumtuliza roho. (Uk. 11)

"Niambie siri ya uganga huu," Riziki alimchokoza. **"Siri dadangu wajua**. Ni yule mwanangu Rukia. Tangu apate hicho kikazi chake Dubai, ame**tu**weka vizuri. Lakini yote ni ya Mungu.**Tu**namshukuru Maulana, Subira alisema huku uso wake ukianza kutia urembo wa wazi, uking'ara kama lulu. "**Hongera dadangu, Mungu amhifadhi huko Dubai aliko. Rukia ni mtoto mwema mwenye nemsi, atachuma tende atuletee nyumbani,"** Riziki alisema akilikumbuka ombi la Kudra. (Uk.14-15)

"Ni hicho kikazi cha Dubai mama," Kudra alisema. "**Kila mtu mwanangu ana bahati yake. Usione bahati ya Rukia itakuja kuwa bahati yako, nao wakati ukifika Mungu atakuinua**." (Uk.22)

"**Karibu mwanangu**," Kudra alikaribishwa na Rehema. "**Ahsante, bibi**," Kudra alisema. "**Nikusaidie vipi mwanangu**?" Rehema alimwuliza Kudra. "Nimekuja kuulizia nafasi ya kazi huko Uarabuni, Kudra alijibu. "Je, mama na baba wameridhia hilo?" "Mama hana neno. Mimi ni mtu mzima sasa. Ninaweza kujiamulia mambo yangu mwenyewe bila kumhusisha mamangu." Kudra alisema. "**Ni kweli mwanangu, lakini ni vizuri kukubaliana na wazazi ili mambo yaende sawasawa; yaani radhi za wazee, mama. Ukikosa utaburutwa na maisha**." Rehema

alishauri akitabasamu. **"N'kutilie chai mwanangu?"** Rehema alimwuliza Kudra. "**Usijisumbue, mama,**" Kudra alijibu. "Keziah?" Rehema aliita. "Naam," sauti iliitika kutoka chumba jirani. **"Mletee mgeni angalau maji ya limau. Mwanangu usikatae kula au kunywa. Mimi ni mamako**." (Uk.22-24)

**"Mwanangu, chakula chako ni kitamu**," Riziki **aliusifu** upishi wa binti yake. "Kweli mama?" Kudra aliitikia kwa swali. "Naona utampikia mkwe wangu chakula kizuri ukiolewa," Riziki alimchokoza binti yake. "Sipendelei kuolewa mama," Kudra aliitoa kauli ambayo ilimtoa moyoni ila hakutaka mamake aijue. **"**Kwa nini? Mwanamke kuolewa ndio hatima yake, mama," Riziki alimwambia mwanawe huku akijiongeza mchuzi wa nguru. "**Sidhani hivyo mama. Si kwa ubaya**. **Mimi ninataka kazi kwanza. Mambo ya kuolewa ni ya baadaye**," Kudra alimweleza mamake msimamo wake. "**Utakavyo mwanangu. Mungu akujaaliye fungu la Baraka. Akufikishe utakako. Akupe hitaji la moyo wako. Mimi kama mamako nakupa radhi zangu mimi na za marehemu baba yako Mzee Sanga,"** Riziki alisema. (Uk.28-29)

"**Pole Dadangu**," Riziki alimweleza Kidawa aliyekuwa taabani walipofika nyumbani kwake. "**Nishapoa dadangu. Ndivyo dunia ilivyo. Ndiyo jaza yangu**," Kidawa alisema huku gharika la machozi likimshuka. (Uk.30)

"Unasikiaje hiyo widi?" Lindo alimuuliza Jannete aliyeonekana kayakaza macho. "Inapaisha juujuu. Kaka, wajua najazia kwenye 'unga' niliyoibugia asubuhi ya leo?" Jannete alisema akikohoa. "Umeitoa wapi?" Lindo alimuuliza Jannete. Jannete hakutaka maswali mengi. "**Usiniulize maswali. Subiri nijichome kwanza. Wee, usinipeleke mbiombio. Uwe mpole. Uwe mtulivu. Mimi sitaki haraka. Unataka niharibu wewe bangi, na mimi ni mtoto wa pekee wa mama yangu,"** Jannete alitua maneno akavuta moshi wa sonyo ile. "**Ala! Husikii? Mimi sipendi ujeuri wako. Ukinipeleka hivyo hii ndiyo itakuwa ya mwisho kushirikiana nawe. Ninataka niwe mwana mtulivu kama mtewa. Sitaki kufanya ujanja maishani**," Jannete alimaliza kuishauri ile bangi. "Au hiyo widi ilipandwa makaburini?" Lindo alimwuliza Jannete. "**Labda. Ni kali. Inaujeuri mwingi sana pamoja na maringo,**" Jannete alisema. "Ni nini hii?" Lindo alimwuliza Jannete. "Ni soda," Jannete alisema huku akicheka. "Mbona ni kali hivi?" "**Ina dawa kidogo ya kuulaza mwili ili uwe sawa lakini ni soda. Kwani unaogopa dawa**?" Jannete alimwuliza Lindo. "Siogopi. Mimi ni mwanamume kisawa." **"Haya basi, kama ni mwanamume maliza hii,"** Jannete alimweleza Lindo akionyesha chupa ya soda (Uk. 33-35)

“**Vipi utokako, mwanangu**?’ Mama yake Subira alimwuliza. “Sikuambulia lolote,” Subira alisema na kuishiwa na nguvu huku akianguka mikononi mwa mama yake. (Uk. 53)

“**Hutaki kwenda mwanangu**? **Nimekuchukulia hadi viza mwanangu**,” Rehema alimwambia Kudra kwa tena kwa sauti nzito akimrai. “**Sitaki**,” Kudra alionekana kama kizuka aliyemweleza bila kutaka kumsikiza kwa muda mrefu. “**Kisa mwanangu? Nina mwajiri tayari. Nauli ya ndege ishalipwa…”** Rehema alisema. **“Sitaki kwa sasa mama. Samahani.”** Kudra aliruka nje ya nyumba ya Rehema. (Uk.55-56)

“**Nina kazi nzuri mwanangu. Utaifanya miaka miwili tu kisha utatajirika. Utaweza hata kuwasaidia jamaa zako**,” Rehema aliasa. “**Naomba iwe hivyo mama. Mzee wangu hawezi kujimudu. Ananitegemea mimi kwa kila kitu; chakula, dawa na kodi ya nyumba**,” Kudra alisema. (Uk.63)

**“Mwadime, kaka mimi ni mtu mzima.”** Riziki alisema. “Uzima unakuzuia nini?” Mwadime alimwuliza taratibu huku amemtia jicho. **“Kaka, tunaweza kusaidiana lakini si hilo la kuoana,”** Riziki alisema kidogo akiwa na uzito. Mwadime anaonekana kama anayetaka kulia. “**Lifikirie kwa tuo nawe.”** Mwadime alisema. **“Hata nikifikiria jibu langu litakuwa lilo hilo,”** Riziki alimweleza Mwadime (Uk.73)

“Tunamtafuta Kassim,” Rehema alisema kwa taklifu kubwa. “Kassim hamumutoboi! Ni waangu, yaani miimi. Zinduuna unaelewa? Eeeh? Eeeeh wangu mimi,” Zinduna alisema, nusu hai, nusu mfu kwa ulevi. “Hatumtafuti masuala kwa hayo. Mimi ni mamake. Ni siku nyingi sijamwona,” Rehema alisema. “Hayuko leo, ametoka. **Ati wewe ni nani? Maama yake? Mbona ulii…muacha? Amesema hana maama?**” Zinduna alisema kisha akalala. (Uk.79)

“**Mwanangu, ni mimi Rehema mamako,”** Rehema alisema huku pumzi zikimtoka. **“Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi? Mama yangu yuko Ujerumani,**” Kassim alisema. **“Nisikilize tu, sikukatizi kunywa wala kufanya lolote la utashi wako. Lakini rudi nyumbani.”** Rehema alimrai Kassim aliyetokwa na ute mdomoni. **“Nyumbani sirudi. Kaeni na huo utajiri wenu wa kunadi watu ugenini. Mungu atawahukumu vibaya sana,”** Kassim alisema akitia tembe fulani nyeupe mdomoni. **“Mwanangu, mwanangu,”** Rehema ni kama alitaka kumpigia magoti mwanawe. **“Nisamehe Mwwaaaa…”** Rehema pumzi zilimwisha. “Nikusamehe nini? Jisamehe mwenyewe kwanza. Sitamani haya *mavolvo* yenu. Mimi ninatumia

baiskeli kama ndio kudura yangu toka kwa Mola. Mimi ni mtu, si shetani," Kassim alimweleza George na mamake walioduwaa kwa maelezo yake. (Uk.80)

**"Mzee, karibu,"** Rehema ilimtoka kauli na tabasamu midomoni. **"Asante, nimekaribia."** Mzee Choka hakuamini hayo ni maneno ya Rehema. Ni kama asali iliyotoka mdomoni mwa nyoka! Mzee Choka alikuwa mtu mpole. Mara nyingi watu walimchukulia kuwa mjinga kwa ajili ya upole huu. **"Analonifikiria mtu kwangu halinidhuru,"** alipenda kusema. **"Karibu ukae,"** Rehema alisema huku amekaa kochini. **"Ahsante," "Ngoja nipumzike kidogo tutasema, jisikie uko nyumbani. Hapa ni kwako Mzee Choka,"** Rehema alitema maneno yaliyomshtua mzee wake, wa hapo zamani. **"Jisikie uko nyumbani,"** tena akaongeza na tabasamu yake iliyofanya yale macho yake makubwa kama tochi kuwaka. **"Hapa ni kwako."** (Uk.81-82)

**"Karibu nyumbani,"** Rehema alimweleza bila kuamini mtoto huyo alikaa katika tumbo lake miezi tisa. "Sawa sawa," Kassim alisema na kucheka na kuyaweka wazi meno yake yaliyotanda ugaga mweusi. Nywele zake hazikuwa zimechanwa kabisa kwa miaka yote ya utoro wake. Hata Mzee Choka alishangaa kumwona mwanawe katika hali ile ya kutisha. **"Badilisha ndara uvae nyingine,"** "Niko sawa," Kassim alisema akicheka bila kizuio. **"Mwanagu, hauko sawa,"** Mzee Choka alimweleza kwa kumrai. (Uk. 83)

**"Nina jambo, samahani,"** Kudra alisema huku mikono yake ameiweka nyuma na kuinika uso kama inavyompasa kijakazi kama yeye. "Jambo gani?" Aliuliza Aminii huku akionyesha wasiwasi wa aina fulani. **"Ningependa muwe mkinikata nusu wa mshahara wangu ili niweze kumsaidia mama,"** Kudra alitoa ombi. "Lakini nilikwambia lazima nilipe madeni ya pesa ulizotumia kwanza" Aminii alifafanua tena. **"Pole kama nitakuudhi bwana mkubwa, lakini pia mimi ningependa kumsaidia mama yangu,"** Kudra alisema bila kutaka kuwaangalia wenyeji wake machoni asije akaambiwa hawaheshimu. **"Nitafikiria,"** Aminii alisema. (Uk.92- 93)

"Hakuna ruhusa kusema na majirani isipokuwa kama nimekutuma mimi mwenyewe," Nayrat alisema kwa sauti ya ukali huku mishipa ikiwa imemtoka shingoni. **"Nilikuwa namwamkua tu yule jirani."** Kudra alisema. "Ulikuja kufanya kazi ama kuamkuana?" Nayrat aliuliza. **"Pole, sitarudia tena,"** Kudra **aliomba radhi**. (Uk.94).

**“Salama Siti,”** Kudra alimwamkua Fatila. **“Salama,”** Fatila alijibu **kwa tabasamu**. **“Hujambo Seyyid?”** Kudra alimwamkua Suleiman huku **akishuka na kuinama kwa heshima**. “**Sijambo binti,** Suleiman alijibu huku akijaribu kumtathmini Kudra. (Uk.96)

**“Mama, kufanya faida si lazima uingie katika pato la mtu. Mimi ningependa tupate wasichana wengi zaidi iwezekanavyo na tujaribu kuwaeleza uhalisia wa maisha ya ughaibuni. Wenyewe wakiridhia ni sawa. Kisha waeleze jinsi wewe kama ajenti au wakala utakavyonufaika.”** Kassim alimwambia Rehema. “Vipi? Mbona sikuelewi **mwanangu?” “Ninasema mama, tungepnda kuwasaidia hawa wasichana kweli. Tupate watu ughaibuni walio na na kandarasi za sawa, tupate watu ambao wanataka wafanyakazi wa kweli si watumwa mama. Pole mama kama ninakukosea heshima lakini hivyo ndivyo ninavyofikiri,”** Kassim alimweleza. “Haya panga. Kisha unaelewa? Bora biashara isishuke bwana,” Rehema alisema (Uk.103)

Mama Hadija pia alimpenda Kudra sana. Katu hakutaka aondoke, hata alipoona matatizo aliyoyapitia katika nyumba ya mwanawe na mkazamwanawa, alimshauri. **“Kukasirika ni ujinga mwanangu, wasamehe wanaokukosea. Siku moja watajua.”** (Uk.106)

Hadija ndiye aliyemzima mkazamwanawe na hata mwanawe mwenyewe walipomtendea Kudra mambo yasiyofaa. Ungemsikia akisema, **“Mwanangu, huo sio mwenendo wa dini.”** (Uk.109)

“Hata mimi ni vivyo hivyo. Ila mimi ninapewa elfu mbili za Kenya. Hizo nazo utafanyia nini?” Kudra aliuliza. “Afadhali wewe. Mimi ninaomba nipewa hata shilingi moja tu,” Almasi alisema. “Shilingi moja itakufaa aje nawe?” Kudra alimwuliza Almasi aliyecheka kama kizuka. **“Za kutuliza roho yangu tu, yaani, nafsi yangu ili nisijione kama mtumwa dadangu.”** “**Pole dadangu.** Labda wanalipa maajenti, ajenti wako ni nani?” “Anaitwa Rehema,” Almasi alisema. (Uk.113)

**“Dadangu habari za Kudra?”** Kidawa alimwuliza. “**Kudra hatumsikii. Hupiga mara chache. Mkubwa wake hataki awasiliane na watu nyumbani sasa,”** Riziki alisema akiwa amejishika tama. “Kisa?” Kidawa alimwuliza akijaribu kumchua mgongo kwa maji ya mikoko. **“Nitajuaje dadangu?** Mambo ya uarabuni unayajua?” Riziki alisema akikunja uso kwa uchungu, Kidawa akimchua mgongo ili kuulainisha. (Uk.122)

***"I love you,"*** Salim alitamka maneno matatu yenye uzito. Kudra aliridhia na maisha yake yakabadilika japo Salim alimweleza alitaka ibakie siri. Hakutaka hata binti yake ajue. **"Kwa nini?"** Kudra alimwuliza kwa mshtuko huku amemtia jicho la huba. **"Binti yangu angetaka kupewa heshima yake,"** Salim alisema. **"Kwa nini haoelewi?"** Kudra alipata msingi wa kumwuliza bosi wake hapo alipokuwa amelala kitandani mwake. **"Kuolewa ni hiari ya mtu. Ataolewa wakati ambapo atataka,"** Salim alisema. (Uk.132)

"**Pole Kidawa mwenzangu. Mambo ya kazi. Nina vikazi naona vinanizidia na huu uzee nilionao**," Riziki alisema. **"Kazi ni maisha dadangu. Bila kazi mtu haishi. Sote tunategemea kazi. Hapana ubaya ukiishika pindi Mungu amekupa uzima,"** Kidawa alisema. **"Alhamisi hukuja dadangu,"** Riziki alimweleza Kidawa. "**Ni kweli. Hiyo Alhamisi kulikuwa na visanga hapa Likoni.** Wasichana na wavulana wetu walifumaniwa wakipiga picha uchi," Kidawa alisema (Uk.142)

**"Mambo yote nimesema kwenye hiyo barua. Usinisumbue kwa lolote,"** Salim alisema. **"Tafadhali Kudra, tuheshimiane. Saa moja jioni isikupate ndani ya nyumba yangu. Ikikupata itabidi niite polisi wanisaidie kukuburuta."** "**Nakushauri uondoke salama. Usichukue chochote au ufanye jambo lolote la ujinga litakalokutia katika matatizo."** (Uk.146)

"Nyinyi washenzi kweli," Kudra alipasua maneno. **"Sisi washenzi? Tutakuja kuona washenzi ni nani,"** Kudra anakmbuka Dele na Kele wakimweleza (Uk.148)

"Hapa tunashughulika na *massage,* yaani ukandaji na kunyoosha viungo vya watu … Huja wateja wa kike, vilevile huja wateja wa kiume. Wote huwahudumia. **Sasa ningependa unipe pasi yako nikuwekee mahali salama,"** Saumu alisema. **"Nitaiweka mwenyewe, dadangu,"** Kudra alisema. **"Lakini hivyo ndivyo Bi. Mkubwa alivyoniagiza,"** Saumu alimwambia. **"Sidhani nitakupa. Samahani,"** Kudra alisema. (Uk.164-165)

***"Order! Order!"*** Spika alisema huku akisimama. **"Bw. Ndugu Spika, naomba radhi kwa tabia yangu lakini imetokana na uzito wa jambo nililokuwa nikichangia,"** alisema Mheshimiwa Kajembe (Uk.172)

**"Tukate mahusiano na nchi hizi,"** alisema Mhesimiwa Jumbe akiwakilisha jimbo mojawapo la Pwani. **"Mimi nimeathirika zaidi,** katika wasichana mia sita wanaokwenda uarabuni kutafuta kazi, hamsini ndio tu wanaopata matlaba yao. Wengine hufa huko. Wengine hawalipwi, wengine hufukuzwa kazi wakaishia barabarani. **Je, itakuwaje nisizungumze? Siku zote tunauliza serikali iko wapi? Mimi binafsi Bw. Spika naona serikali imezembea jukumu lake" "Wewe unaona serikali ingefanya nini?"** Spika alimwuliza Jumbe. "Jambo la kwanza ni serikali kubuni nafasi za kazi kwa vijana hawa wanaokwenda ughaibuni kufanywa watumwa. Pili, kuzindua mradi wa kuelimisha vijani kuhusu hatari za nchi kama hizo. **Mwisho ni kusema na nchi za Uarabuni waziwazi kuwa hao vijana wanaokwenda katika nchi zao si watumwa, ni watu. Hata kama ni maskini, lazima haki zao ziheshimiwe,"** Jumbe alisema huku akipangusa jasho lililokuwa limetanda kwenye uso wake. **"Yee! Yee! Yee!"** Bunge lilivamia kwa **sauti za kumhimiza Jumbe**. **"Jambo jingine ni kuwafungulia kesi maajenti wanaowapunja vijana pesa kwa kuwapeleka nchi kama hizi. Haki ya Mwafrika lazima iheshimiwe, hata kama ni maskini. Ni watu wa Mungu! Asanteni,"** Jumbe alimaliza huku uso wake ukionyesha ghadhabu. (Uk.172)

**"Sielewi mwanangu,"** Riziki alimwambia Kudra. **"Duka la ususi katika kitengo kimoja mtakuwa na watu wa kukanda. Hata huduma ya hina, mama tutaitoa papo hapo,"** Kudra **alieleza** huku **akipima athari za maneno yake** kwa mama yake. **"Sawasawa mwanangu, kipendacho roho ni dawa,"** Riziki alimkubalia mwanawe hukuakimpa shime. (Uk.182)

### Kiambatisho II: Udhihirikaji wa Utoupole

**"Hutoki hapa!"** Riziki alimfokea. "Mama, kwa nini umekuwa mkali? Kudra aliuliza. "Wewe ungali mtoto mdogo. Usifikirie mambo ya kazi hata yakakutanza. Kwanza fikiria masomo kisha baadaye utafikiria mambo ya kazi."  Riziki alielekeza kwa matao ya chini huku amemtia mwanawe jicho la ukali. (Uk. 5)

**“Hutaki shule, wataka nini? Kuolewa?”** Riziki alimsemesha Kudra kwa ukali. “Si kuolewa mama. Mimi nataka kazi ili nikusaidie ata wewe kujikimu.” Kudra alisema. **“Kama hutaki kusoma, hapa sikutaki na mimi, katu usipate kuniita mamako,”** Riziki alisema. (Uk.7)
**“Kama unataka kulewa, lewa kabisa, hiyo dawa ya unga ikuue tukuzike maana huna faida,”** Kidawa alimweleza Lindo kwa ghadhabu. “Usimwambie hivyo dadangu, Riziki naye alimshauri aliyekarambuka kwa fundo la hasira moyoni. **“Ana faida gani? Ni hayawani huyu hasa. Alewa kokoteli. Alewa 'unga'.”** (Uk.11)

“Unafiki ulioje!” Sanga alishangaa kuona jinsi vizazi vilivyoharibika na jinsi wazazi wao walivyolia. Ibilisi alimwingia na kisha akapanua kinywa chake. Neno moja tu lilimtoka kama risasi… “**Umesema lakini hutaishi. Tutahakikisha kuwa tumekutia adabu.”** Kundi la ‘Kuklax Klan’ liliapa. (Uk.12)

“Habari za jioni mama?” Kudra alijaribu kumwamkia mamake kwa sauti babaifu ila **alizabwa kofi “Sitaki mtoto aniletee ulaghai wa pesa nane hapa. Mchana mzima hujui mtoto yuko wapi. Anataka kuanza kufuata barabara na haya mambo ambayo siyataki mimi. Eeh, na huyo mtoto anataka kula. Anataka kusoma hali anajua ni mimi tu, hana baba. Baba yake amemalizwa na hili jinamizi la dawa za kulevya. Huyu mwanangu anataka kunipa maradhi ya moyo. Hapa hakai na ujeri huo. Nitapambana naye kufa kupona!”** Riziki alisema (Uk.26)

“Hodi hapa,” mara Lindo alisema na kusukuma kilango kibovu kilchotengenezwa na matete. “Usiingie, *maze*,” Zilisema sauti mbili zilizokuwa na mkoromo kama wa vyura mtoni kwa pamoja. “Kwa nini?” Lindo aliuliza huku akiingia ndani na akicheka. **“Ni *fun* tu. Wewe fala nawe,”** ilisema sauti ya Jannete. (Uk.33)

**“Tumemleta hapa huyu mwanamke chizi. Ni muuzaji sugu wa dawa. Yeye si mlevi ila ameharibu vijana wetu,”** Kundi la waandamanaji lilidai. “Si ukweli, mimi siuzi dawa,” Jannete alijitetea vikali akiwa amezingirwa na kundi la watu wenye mori. **“Ni jeuri sana huyu mwanamke,”** Subira alisema akitaka kumkabili Jannete. **“Wauzaji dawa mmewaogopa. Wako wanaowaongoza na mnawajua.” “Ni bangi. Ni dawa. Ni kokeini anazovuta,”** kundi lilisema likionyesha hasira za wazi za kutaka kumuua Jannete. **“Muue! Muue!”** Kundi lilisema kwa hasira (Uk.42)

“Wanatuharibia watoto wetu wasisome,” Mwamba alisema siku hiyo ya maandamano. **“Watakiona,”** Kidawa alisema akikumbuka mwamawe, Lindo, aliyeanza kama muuzaji lakini ambaye aligeuka na kuwa bwege kwa kuborongwa na dawa hizo. …Siku moja Kidawa alimwendea Mwamba na kumshambulia. **“Wewe umemfanyia mwanangu dawa,”** Kidawa alisema. “Vipi jirani, mbona sikuelewi?” Mwamba alisema huku akiendelea kusuka ukili. **“Unajifanya wewe ni msusi kumbe ni mchawi.”** “Sikuelewi Kidawa, Mwamba alisema huku ameacha kusuka ukili na kumwangalia Kidawa ambaye amegeuka kichaa. **“Hunielewi? Utanielewa. Mimi nitakwenda kukufanyia zinguo ili upate tabu kama mwanangu. Itakuwaje wewe jirani yangu ndiye wa kumukuma mwanangu Lindo katika Dawa? Wewe tunayelala njaa Pamoja,”** Kidawa alisema akionyesha ghadhabu. (Uk.43)

“Ni nini Jamani?” Jirani mmoja aliuliza huku akionyesha wasiwasi. “**Ni huyu bwana anajifanya msusu kumbe nyoka. Ni ziraili huyu. Anawasukuma wanetu kwenye dawa. Si mwanangu tu, bali Watoto wengi hapa. Hata yule mtoto wa Mwadime aliyepotea. Hata sasa Mwadime hapati kumwona,”** Kidawa alisema huku kipovu kikimtoka. “Wanaowasukuma Watoto kwa dawa za kulevya ni hao matajiri wanaoziuza dawa. Ni hao viongozi wenu. Mnawachagua nyinyi wenyewe. Mnawafanya wabunge. Mnawafanya *madisii*, waona. **“Mwongo wewe, mwanaharamu,”** Kidawa alisema. “Mimi ningekua na uwezo nisingekua nashona mikeka basi. Ningekuwa ninakaa nyumba kama wao. Dadangu ningekuwa Nyali ama ningekuwa huko Bamburi, waona? **“Mshenzi, mchawi wewe. Mwanaharamu shika adabu …”** Kidawa alisema. **“Ni wewe wa kushika adabu si mimi. Kama una wazimu usije hapa kunizuzua. Nitakufundisha adabu asiyo kufundisha mumeo,”** Mwamba alisema. (Uk.44)

“Wewe Kassim unanionea siku zote,” Lindo alisema. “Nikuonee kwa nini mwenzangu?” Kassim alimwuliza Lindo. “**Wewe mwenyewe wajua. Hata kama sina uwezo, kaka usinipeleke mbio hivyo,”** maneno yalimdondoka Lindo. **“Usiniletee ulevi wako wewe Lindo,”** Kassim alisema. **“Ulevi? Ni wewe unayenipa pesa za kulewa…Eeh?”** Lindo aliuliza kwa hamaki. **“Lindo, wewe ni wazimu. Rudi usome uwe daktari,”** Kassim alimweleza Lindo huku akimwonya. **“Nikienda kusoma, baba yako atanililipia karo?”** Lindo alimwuliza Kassim. “**Atakulipiaje? Hakukuzaa. Tena wewe ni mwanaharamu. Wafanyie watu kazi wakitajirika na wewe ukidamirika kama unyasi katika kiangazi,”** Kassim alidakia. **“Mwanaharamu ni wewe ambaye mamako ananadi watoto wa watu ughaibuni kwa ajili ya ubinafsi,”** Lindo alisema. **“Nenda kauze unga, wewe**

**fala,"** Kassim alimweleza Lindo na kuamsha hamaki zake. **"Kama mimi ni fala mbona umeacha hio mali haramu? Walala mitaroni kama sisi wanaharamu?"** Lindo alimwuliza Kassim kwa msisitizo. (Uk.45- 46)

Rehema alinunua mabasi mabasi yakapewa jina, **"Maisha ni hiari yako."** Serikali nayo ilifumba macho. Haikujali kwamba vinywa vya watu vililalamika. Magazeti yalilalamika lakini Rehema alitembea Changamwe kwa madaha akisuta maadui wake kwa kiburi. **"Mtasema kisha mtachoka,"** Rehema alisema kwa kiburi. Semi nyingine aliandika kwenye magari yake. **"Semeni lakini mtachoka maana kesho hamko."** (Uk.56)

"**Tafuta lako, kaka. Sitaki kusumbuliwa,"** Rehem alimwambia mzee wake. "sawa." (Uk.57)

"Nikusaidie vipi?" Kudra aliulizwa katika hoteli ya *Oak Tree* na mhudumu. "Ninatafuta kazi," Kudra alisema. "Kazi gani? Wewe ni mpishi?" "Aaa si…ni…ninaweza hiyo," Kudra alimjibu mhudumu kwa kuchanganyikiwa kwingi. **"Huna hakika dadangu ya kile ukisemacho,"** alisema mhudumu **kwa ujeuri na akafunga kiofisi** chake. (Uk.59)

Kassim alitoroka shuleni shimo la tewa akiwa kidato cha pili. Alikuwa mwanafunzi stadi lakini wenzake walimwatrhiri hadi akakanyaga nje ya shule asirudi tena. Mama yake alimbembeleza arudi shuleni lakini alikataa na kusema, **"Potelea mbali! Akitaka kusoma, asipotaka kusoma ni shauri yake. Maisha ni yake. Ni yeye atakaye menyana nayo mwenyewe."** (Uk.78)

"Mwanangu, ni mimi Rehema mamako," Rehema alisema huku pumzi zikimtoka. **"Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi? Mama yangu yuko Ujerumani,"** Kassim alisema. "Nisikilize tu, sikukatizi kunywa wala kufanya lolote la utashi wako. Lakini rudi nyumbani." Rehema alimrai Kassim aliyetokwa na ute mdomoni. **"Nyumbani sirudi. Kaeni na huo utajiri wenu wa kunadi watu ugenini. Mungu atawahukumu vibaya sana,"** Kassim alisema akitia tembe fulani nyeupe mdomoni. "Mwanangu, mwanangu," Rehema ni kama alitaka kumpigia magoti mwanawe. "Nisamehe Mwwaaaa…" Rehema pumzi zilimwisha. **"Nikusamehe nini? Jisamehe mwenyewe kwanza. Sitamani haya *mavolvo* yenu. Mimi ninatumia baiskeli kama ndio kudura yangu toka kwa Mola. Mimi ni mtu, si shetani,"** Kassim alimweleza George na mamake walioduwaa kwa maelezo yake. (Uk.80)

Kudra alipoendelea kukaa Dubai alianza kumkosa mamake mzazi. Mwanzo alikuwa akimpigia simu akitumia simu ya mkono ya Nayrat lakini baadaye Nayrat alianza kumpa visababu vya kutotumia simu yake. Alimweleza, **"Ni ghali kumpigia simu mama huko Kenya."** 'kulikoni?' Kudra alijiuliza. "**Wajua tulisahau kukukata gharama ya ndege katika mshahara wako. Pole kama itakuathiri vibaya lakini lazima tufanye hivyo. Itabidi pia tukukate pesa za ajenti wako, mama Rehema aliyekuleta. Tulimpa elfu tano, dola za Kimarekani ili kukusafirisha huku. Sasa ninaona lazima tuzikate kwenye mshahara wako ili na sisi tusifinyike sana."** Aminii alisema, akaenda kujibu simu katika lugha ya Kiarabu. Aliporudi aliendelea, "**Pia biashara yetu haiendi vizuri. Itabidi tumekukata mshahara wako, yaani tuuteremshe kwa kiwango ambacho tunaweza kumudu**." Aminii alizungumza bila kuonyesha hasira wala furaha. "Una jambo la kuuliza?" Aminii alimwuliza Kudra akifanya juhudi za kutabasamu. "Sina jambo la kuuliza." Kudra alisema. (Uk.88)

**"Kelbu wewe,"** Bi. Nayrat alimwambia Kudra kila wakati alipokosea jambo dogo. (Uk.91)

"Nina jambo, samahani," Kudra alisema huku mikono yake ameiweka nyuma na kuinika uso kama inavyompasa kijakazi kama yeye. "Jambo gani?" Aliuliza Aminii huku akionyesha wasiwasi wa aina fulani. "Ningependa muwe mkinikata nusu wa mshahara wangu ili niweze kumsaidia mama," Kudra alitoa ombi. **"Lakini nilikwambia lazima nilipe madeni ya pesa ulizotumia kwanza"** Aminii alifafanua tena. "Pole kama nitakuudhi bwana mkubwa, lakini pia mimi ningependa kumsaidia mama yangu," Kudra alisema bila kutaka kuwaangalia wenyeji wake machoni asije akaambiwa hawaheshimu. "Nitafikiria," Aminii alisema. (Uk.92- 93)

Kudra alijaribu kujuana na majirani pale nyumbani kwa Aminii. Hakujua kuwa huko ndiko kulikowasha moto zaidi. Nayrat alipogundua jambo hilo **alimtetesha** sana. **"Hakuna ruhusa kusema na majirani isipokuwa kama nimekutuma mimi mwenyewe,"** Nayrat alisema kwa sauti ya **ukali** huku mishipa ikiwa imemtoka shingoni. "Nilikuwa namwamkua tu yule jirani." Kudra alisema. **"Ulikuja kufanya kazi ama kuamkuana?"** Nayrat aliuliza. "Pole, sitarudia tena," Kudra aliomba radhi. "**Singependa urudie tena kosa hilo,"** Nayrat alimweleza. (Uk.94).

Jioni moja Kudra alikuwa hajihisi vizuri. Licha ya kumweleza Nayrat, Nayrat hakutaka kuzingatia lolote. Alifanya kazi hadi Nayrat akaona kuwa hawezi kufanya kazi kikamilifu. **"Nenda ukalale**

**wewe! *Lazy woman*!"** Nayrat **alimzomea Kudra** akimkodolea macho makali kama ya simba jike. (Uk.106)

Aminii naye alizoea kutoka kazini mapema, wakati mke wake hayuko nyumbani, kisha **anayapapasapapasa maziwa ya Kudra…**Aminii alizoea kwenda jikoni Kudra akipika na **kumgusagusa mabegani na kwingine kote mwilini.** Kudra hakupendelea tabia hii. "Nitamwambia mama yako na mkeo." (Uk.108)

Kudra alipokea habari kuwa mama yake alikua mgonjwa, alisema na Nayrat ili wamkubalie arudi nyumbani ili kumuuguza Riziki. Nayrat hakuonekana kujali yaliyomkabili Kudra. Alimpuuza licha ya kumkatia mshahara. "Mama yangu ni mgonjwa," Kudra alimweleza Nayrat aliyekuwa akijitanda hijabu ili aondoke. **"Acha tutafikiria,"** Nayrat alimweleza Kudra kwa **kumkata kauli**. "Ninasikia hawezi kupika. Anasaidiwa na jirani," Kudra alisema. **"Ngoja nitasema na mzee kisha nitakuelezea la kufanya,"** Nayrat aliyeonyesha **hakujali kitu** alimwambia Kudra. (Uk.115)

Hanawi naye alitafuta kila sababu ya kugombana na Kudra kila siku. **Alimsonya** na hata **kumkaripia** bila sababu yoyote. **"You slave!"** Hanawi alimwambia Kudra siku moja alipoleta wali mbichi mezani. **"Mimi si slave. Mimi nina mkataba wa kazi hapa Dubai. Dadangu pia ni rafiki ya baba yako. Kama unaona uchungu, mkataze,"** Kudra alisema kwa ghadhabu. Alishangaa pia kumwita dadake. **"Siwezi kula chakula chako. Hujui kupika, tena wewe ni mchafu nenda koleji ufundishwe kupika,"** Hanawi alimweleza Kudra. **"Ukikataa kula, ni shauri lako. Hata ukaolewe! Utaozea kwenu sijui ukifanya nini, huwezi kuolewa na ...."** Kudra alijizuia kutamka jina hilo. (Uk.135)

Hadi leo, kilio cha **Subira hakijazimika**. **Mara chache, hupita hapo kwa Rehema. Hakutaka kumwamkia Rehema**. Aliona Rehema kama mwizi mwingine, hana roho ya utu. Alijali nafsi yake tu. (Uk.140).

Kidawa alikumbuka siku moja alipokwenda kumtembelea Riziki, aliyehamia kwenye mtaa ulioitwa New Horizon na kusahau kibanda chake cha awali. **"Karibu, Herdaa aaa pole Rachael. Jamani hmmm Kidawa!"** Kidawa alipigwa na butwaa jinsi jina lake lilivyofutika katika kumbukizi za mwenzake. "Itakuwaje hivyo?" Kidawa alijiuliza huku akifanya bidii kumwambia mwenzake "Ahsante Riziki," Kidawa alijibu kwa kuchanganyikiwa kwingi. Alichapuka na kuondoka. (Uk.142)

“Habari za siku nyinyi?” Kidawa alimwuliza Riziki. **“Sawa,”** Riziki alisema huku akienda kujibu simu ya simu ya mjenzi aliyekuwa akimjengea nyumba za kukodisha huko Kisauni. “*Ok,”* Riziki alisema. “Yaah. Lakini usinunue saruji nyingine, ununue ya ‘Bamburi’ kwa sasa. *Ok*...yaaa, *ok* sawa,” Riziki alisema. (Uk.142)

“**Hapa hutakaa upende usipende. Tena ukicheza nitakubinginya.” “Nitakaa upende usipende.”** Kudra alijibu kwa kiburi na ujeuri. **“Wewe umekuja huku kufanya kazi kisha unaleta hata ujeuri,”** Hanawi alimweleza Kudra. **“Ndiyo, nimekuja kufanya kazi, hiyo isiwe sababu ya kunidharau. Mimi ni mtu kama wewe hata Kama naonekana tofauti.” “Hiyo ndio sababu uliiba dhahabu na pesa ulikotoka ukaja kujificha hapa?”** Hanawi alimweleza Kudra. **“Uongo huo. Mzushi wewe. Mimi sina haja na dhahabu za watu. Kuna jambo lililonileta kutoka Afrika. Si vipuli wala si mali ya watu,”** Kudra alisema. **“Kama si mali kwa nini unaparamia uhusiano wa mapenzi na baba?**” **“Si kuparamia lolote. Aliyetaka ni babako, dadangu,”** Kudra alisema. **“Umeparamia, ukajifanya rahisi ndipo uvune katika mahusiano kuwili. Wewe ni mjanja kweli,**” Hanawi alimtupia Kudra kombora la matusi. **“Sina ujanja. Kilichompendeza baba yako kinakuumiza wapi? Wewe unajuaje anavotaka baba yako? Kama unaweza, mchagulie atakavyo,”** Kudra alisema. (Uk.145)

**“Hapa hapana mwizi, mgeni aliyekuja ndiye,”** Suzzy alisema. “Si mimi,” Kudra alisema. **“Ni wewe,”** wote walisema kwa kauli moja. Suzzy alimkodolea macho na kumweleza **“Wewe wizi umekuleta Dubai, mwanamke gani wewe? Unataka kutajirika mara moja?” “**Si mimi, dadangu,” Kudra alisema na kuangua kilio. “Ni kweli wanavyosema kuwa wewe ni mwizi?” Omar aliuliza. “Si kweli,” Kudra alisema akikumbuka mambo yalivyokuwa kwa Aminii. “Hujawahi kuwaibia watu mjini Dubai?” Omar aliuliza “Sijawahi,” Kudra alitumia nguvu zake zote kukana hata kama alionyesana wasiwasi wa wazi. (Uk.150-151)

“Hapa tunashughulika na *massage,* yaani ukandaji na kunyoosha viungo vya watu … Huja wateja wa kike, vilevile huja wateja wa kiume. Wote huwahudumia. Sasa ningependa unipe pasi yako nikuwekee mahali salama,” Saumu alisema. “Nitaiweka mwenyewe, dadangu,” Kudra alisema. “Lakini hivyo ndivyo Bi. Mkubwa alivyoniagiza,” Saumu alimwambia. “Sidhani nitakupa. Samahani,” Kudra alisema. **“Mimi sitaki ubishi, ungesema kabisa na Fauziya asikulete huku. Huku ukija, basi lazima pasi yako uitoe,”** Saumu alisema akiwa amesimama na kwa **sauti ya juu** kama ambaye **alitaka kugombana**. “Dadangu, **mbona hutaki kufuata maagizo ya kazi?”**

Saumu alimwuliza Kudra. “Mimi kazi hio siipendi, staki kuifanya,” Kudra alisema. **“Lazima uifanye. Ikiwa hutaki kufanya, nitakufanya ufanye!”** Saumu alisema kwa hasira. (Uk.164-165)

Kudra alikaa ukumbini kwa majonzi makubwa. Hata siku moja alipokuwa hali, Saumu alimwita, **akampiga makofi na viboko… “Unaleta mchezo gani hapa? Wewe unadhani ni bora kuliko sisi? Pana wasichana warembo hapa. Ikiwa unadhani ulikuja raha, sahau. Ulikuja kufanya kazi ukichagua kazi ni shida yako. Mimi sitavumilia kiburi chako, unaskia?”** “Ndiyo nimeskia,” Kudra aliyesinasina alisema. (Uk.166)

Kudra alitafuta nambari ya ubalozi wa Kenya. Kila msichana aliyemwuliza kutoka Kenya alisema hakuwa nayo. Saumu alisikia kuwa kudra alitafuta nambari. “Si kwa ubaya,” Kudra alijitetea walipokumbana na Saumu. “Ni kwa nini?” Saumu alimwuliza. “Nilitaka kuuliza habari za mamangu. Niliskia alipiga simu akinitafuta,” Kudra alijibu akitathmini athari ya maneno yake kwa Saumu. **“Wewe unadhani mama yako ni bora kuliko mama zetu?”** Saumu alimwuliza kudra huku **akimtemea mate usoni na kumfurusha ofisini.** (Uk.169).

**“Namtaka mwanangu,”** Riziki alisema huku amevuta juu buibui yake. **“Mwanao yupi?”** Rehema alisema bila kuonyesha kujali. **“Mwanangu Kudra, ulimpeleka Dubai, Sasa nasikia anafanyiwa mateso huko,”** Riziki aliteta. “**Mwanao alienda kwa hiari yake, dadangu. Pia akiona si kuzuri, ana miguu na macho. Anaweza kurudi. Kama unachomwa na hasira nenda polisi. Nenda unishtaki.** (Uk.169-170)

“Hii kazi siitaki. Nipe pasi yangu.” **“Pasi hupati na hapa huondoki ng'o!”** Saumu alimjibu Kudra. “Kazi mtu hufanya kwa hiari, mbona umekuja huku Dubai kututendea hivi?” **“Usinilaumu mimi kwanza mlaumu aliyekuleta dubai na umasikini wako. Mimi sikuja kukutafuta. Umewahi kumwona mtoto wa waziri mkuu huku? Kwa hivyo usiniletee ukali. Mimi si jamaa yako wala mwajiri wako. Mwajiri wako ni Fauziya. Ngoja akija halafu…,”** Saumu aliyeonekana kwa mara ya kwanza ametishika alisema. “Fauziya siye aliye na pasi yangu,” Kudra alimtangazia Saumu. (Uk.171)

**“Je, Afrika inapelekwa tena katika jinamizi la utumwa wa ukoloni?”** Aliuliza Kajembe ambaye alikuwa waziri aliyesimamia masuala ya wanyamapori. **“Kama si hivyo, itawezekanaje habari hizi zinapokuja, serikali haifanyi jambo lolote? Tutaendelea kustarehe huku vijana wetu wakinyanyaswa? Wakija hapa kwetu tunawapa heshima na kuwapigia magoti. Kwa**

**nini?"** Aliongezea Mheshimiwa Kajembe asisikie Spika aliyefanya bidii kumsimamisha. "*Order! Order!*" Spika alisema huku akisimama. Baadaye Mheshimiwa Kajembe aliketi huku **akionyesha hasira ya wazi**. Hata **alipiga vidoko bungeni** na Spika akamtaka kuomba msamaha.

Kuna mmoja aliyekuwa kwenye foleni aliyeitwa Jane. **Alitobolewa jicho na mtoto wa mwajiri wake.** Alitazamia kuwa mwajiri wake angempa ridhaa lakini baadaye alielezwa kuwa ilikuwa ajali ya kazini. "Mtoto hakupenda, ilikuwa ajali," Mwajiri wake alimweleza ukweli mchungu. Aliendelea kufanya kazi akifikiria kuwa mwajiri wake angefikiria tena hali yake. Hakufikiria kitu. Kila mara **alimpiga** na **kumtukana** kwa ajili ya ujinga wake na hatimaye **kumnyima chakula** na **kumfukuza nyumbani** pale **aliporushiwa pasi yake.** (Uk.175)